# Nipashe

Ijumaa Oktoba 11, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580046

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Lissu agoma kurejea, ahofia usalama wake

UKURASA 3


Biashara mahindi ya kuchoma, vipi msimu mvua, mawingu tu?

Walikoegelea, kuvuka kwa mtumbwi miaka 21, daraja lawabadilisha maisha

BUFE

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Mwalimu aliyeushika ujasiriamali bila ya kutelekeza chaki darasani

Benki Dunia: Tasaf 'imetukosha' tunaipa Sh. trilioni 1 roho nyeupe

UCHUMI

Habari katika picha

Tabianchi yageuza kilimo mahindi janga kwa washika jembe Korogwe Ukurasa 18

UKURASA 13

# Rugemalira, Seth nao wajisalimisha kwa DPP

• **Waomba** kukiri makosa ya uhujumu, wengine walipa mil. 100/- na kuachiwa...*Endelea ukurasa 2*



Wafanyabiashara Harbinder Sethi na James Rugemalira wakiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, baada ya kesi inayowakabili ya uhujumu uchumi kuahirishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MAKTABA**

## YALIYOMO


**UKURASA WA 4**

**LESENI MADINI HADI BARAZA LA MAWAZIRI**

SERIKALI imebadili mfumo wa utoaji leseni za madini na sasa zitatolewa na Baraza la Mawaziri badala ya waziri...

**UKURASA WA 7**

**JPM ATAKA MAWAZIRI WENYE MOYO WA UTUME**

RAIS John Magufuli, amesema wakati wa uongozi wake anataka mawaziri wenye moyo wa utume wa kutumikia...

**UKURASA WA 26**

**MAHAKAMA KUSIKILIZA KESI 60 KWA 'VIDEO CONFERENCE'**

MAHAKAMA ya Rufani inatarajia kusikiliza kesi 60 kwa mfumo mpya wa mawasiliano kwa njia ya picha...


## TMA yaonya mvua zaidi

UKURASA 3

# Serikali yapigilia nyundo ukomo madaraka ya Rais

• **Yasisitiza** hakuna wa kugeuza muda uliopo kikatiba, yamruka aliyefungua kesi kortini... *Endelea ukurasa 2*


**MICHEZO** **MAXIME AWAPA MCHONGO YANGA** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Kitambulisho cha NEC hakimo uchaguzi mitaa

Na Mwandishi Wetu

SIKU mbili baada ya uandikishaji wa wapigakura kwenye orodha ya daftari la uchaguzi wa serikali za mitaa kuanza, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema kitambulisho cha mpigakura hakitatumika katika uchaguzi huo.

Awali, katika mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), ulikitaja kitambulisho hicho kuwa miongoni mwa vitambulisho vinane vitakavyokubalika na kutumika.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Mahera, uchaguzi huo ambao utafanyika Novemba 24, mwaka huu, hauhusiani na tume hiyo.

Alisema ni vyema wananchi wakajitokeza kujiandikisha kwenye orodha ya wapigakura kwa kuwa bila kufanya hivyo hawataruhusiwa kupiga kura.

"Ambaye hatajiandikisha hataruhusiwa kupiga kura hata kama atakuwa na kitambulisho cha mpigakura. Uchaguzi huu hauhusiani na NEC bali Tamisemi kupitia halmashauri zake," alisema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura unaofanywa na tume kwenye mikoa mbalimbali nchini, unahusu uchaguzi mkuu utakaofanyika mwakani.

Alisema uboreshaji unaendelea kwa sasa unaendelea katika mikoa ya Tabora, Katavi na Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma ambako uboreshaji utafanyika kuanzia Oktoba 14 hadi 20, mwaka huu.

Dk. Mahera alisema uandikishaji utaendelea kwenye mikoa ya Songwe, Dodoma na Singida kuanzia Oktoba 26 hadi Novemba Mosi, mwaka huu.

**UANDIKISHAJI DAR**

Katika maeneo mbalimbali jijini uandikishaji unakwenda kwa suasua kutokana na mvua zinazoendelea kwa wananchi kushindwa kujitokeza.

Kutokana na hali hiyo, viongozi wa vyama wanatumia mitandao ya kijamii kusambaza ujumbe wa kuwataka wananchi kujitokeza kujiandikisha kwenye maeneo yao.

Diwani wa Kunduchi (CCM) Michael Urio, ni miongoni mwa viongozi ambao wanafanya uhamasishaji huo kwa kupita katika mitaa wanakoishi wananchi katika kata yake.

Alisema ameamua kufanya hivyo baada ya kuona idadi ya wanaojitokeza kujiandikisha ni ya kusuasua

INAENDELEA UK.8

# Rugemalira, Seth wajisalimisha kwa DPP

Na Waandishi Wetu

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imeelezwa kuwa mfanyabiashara, James Rugemalira ameandika barua kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), kuomba kukiri makosa yao ya uhujumu uchumi.

Pia, mmiliki wa Kampuni ya Kufua Umeme ya IPTL, Habinder Sethi, imedaiwa aliandika barua muda mrefu tangu Rais John Magufuli alivyomuelekeza DPP kutoa msamaha kwa washtakiwa wenye mashtaka ya uhujumu uchumi ambao watakiri kosa na kurejesha hasara waliyosababisha.

Wakili wa Rugemalira, Michael Ngaro, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, kuwa mshtakiwa huyo ameandika barua ya kukiri na kwamba mpaka sasa hawajapata majibu.

Ngaro aliuomba upande wa mashtaka kufanya mchakato ili wapate majibu ya barua hiyo haraka.

Akijibu hoja hiyo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simoni, alidai ni kweli wamepokea barua ya mshtakiwa wa pili (Seth) na kwamba wanaishughulikia na atapatiwa majibu.

Inadaiwa awali, Rugemalira aliandika barua ya kutaka kuonana na DPP, lakini baadaye aliamua kuandika barua ya kukiri ili kuingia kwenye makubaliano.

Hakimu Shaidi, aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 24, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

Seth na Rugemalira wako gerezani kwa mwaka wa tatu, wakisubiri upelelezi wa kesi yao kukamilika.

Washtakiwa kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 12 yakiwamo ya utakatishaji fedha na kusababisha hasara ya Dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh. 309,461,300,158.27. Kwa mara ya kwanza walifikishwa mahakamani hapo Juni 19, 2017.

Washtakiwa hao wanadaiwa kuwa Oktoba 18, 2011 na Machi 19 , 2014, jijini Dar es Salaam walikula njama katika nchi za Afrika Kusini, Kenya na India ili kutenda kosa.

Pia, inadaiwa katika mashtaka ya kujipatia fedha, kwamba kati ya Novemba 28 na 29, 2011 na Januari 23,2014 katika Makao makuu ya Benki ya Stanbic, Kinondoni na Benki ya Mkombozi, tawi la Mtakatifu Joseph, kwa ulaghai washtakiwa hao walijipatia kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dola za Marekani 22,198,544.60

INAENDELEA UK.8



Wakazi wa Mji wa Muheza mkoani Tanga, wakiangalia maji ya mafuriko yaliyozizingira nyumba katika eneo la Mto Amtico, juzi, kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Serikali yapigilia nyundo ukomo urais

Na Gwamaka Alipipi

SERIKALI imesisitiza kuwa muda wa Rais kuwa madarakani ni vipindi viwili tu na kusisitiza kuwa hakuna mtu yeyote anayeweza kubadili utaratibu huo uliopo kwa mujibu wa katiba.

Hata wakati wa uhai wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alisema enzi za utawala wake alisisitiza kuwa masuala ya ukomo wa urais ni vipindi viwili licha ya nchi kuwa katika mfumo wa chama kimoja wakati huo.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua Kongamano la Kumbukizi ya Mwalimu Julius Nyerere lililoandaliwa na Kigoda cha Mwalimu Nyerere katika taaluma za umajumui wa Afrika kwa kushirikiana na Taasisi ya Uongozi.

"Mwalimu alisisitiza masuala ya ukomo wa urais ni vipindi viwili tu licha ya nchi kuwa katika mfumo wa chama kimoja. Nasema hakuna wa kulibadili hili, tutaendelea kuwa na vipindi viwili vya urais," alisema Prof. Kabudi.

"Tusihusishe kesi iliyoko mahakamani na rais aliyepo. Huyo (aliyefungua kesi) ni raia na ana haki ya kwenda mahakamani. Mwalimu Nyerere alisisitiza ukomo wa vipindi viwili vya urais na wako waliojaribu kutaka kulibadili hilo, lakini aliwashukia kama mwewe kwa sababu aliamini hili ni moja ya misingi ya taifa," aliongeza.

Naye Mgoda wa Kigoda cha Mwalimu Nyerere, Prof. Rwekaza Mukandala, alisema mchango wa Mwalimu Nyerere katika ujenzi wa taifa la Tanzania hautasahaulika.

Alisema mwaka 1993, Mwalimu Nyerere alisambaratisha juhudi za wabunge waliotaka kuuvunja Muungano na kutaka muundo wa serikali tatu, pamoja na kuondoa ukomo wa muda wa rais madarakani.

"Mwalimu Nyerere aliamini na kusimamia kwenye fikra na misimamo, misingi ya ubinaadamu na alisimamia katika maandiko ambayo hadi leo viongozi wengi wa Bara la Afrika wanayafuata," alisema.

Prof. Mukandala alisema Mwalimu Nyerere alilipa kipaumbele suala la uongozi kwa kuanzisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na mwaka 1961 alifungua majengo ya chuo hicho na wiki moja baadaye alifungua chuo cha Kivukoni, na Chuo cha Polisi.

"Mwalimu alisema kiongozi lazima awe na sifa kuu tatu. Kwanza awe na uwezo wa kufikiri, pili awe na uwezo wa kujieleza kwa ufasaha, tatu awe mwenye kumudu vizuri kazi yake," alisema Prof. Mukandala.

"Mwalimu Nyerere alikemea mbwembwe, misafara mirefu ya magari ya viongozi, alichukia mishahara mikubwa, viongozi kuwa mabepari. Hakupenda vyeti kutundikwa ukutani, alikemea majina ya vyeo bali alipenda tuitane ndugu."

Prof. Mukandala alisema Mwalimu Nyerere mwaka 1995 alitoa mchango mkubwa wa kupatikana kwa mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Naye Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. William Anangisye, alisema Oktoba 25, mwaka huu, UDSM itatimiza miaka 58 tangu ilipoanzishwa.

Alisema kuanzia mwaka 1970 Mwalimu Julius Nyerere ndiye alikuwa Mkuu wa Kwanza wa UDSM hadi alipong'atuka mwaka 1985.

## HABARI KITAIFA



Msimamizi wa mirathi ya marehemu Dk. Daudi Balali, mkewe Elizabeth Balali, akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi baada ya kusikiliza kesi inayomkabili ya kujipatia pesa kwa njia ya udanganyifu, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Lissu agoma kurejea, ahofia usalama wake

**Na Enock Charles**

MWANASHERIA Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, amesema amesitisha mpango wake wa kurejea nchini mpaka pale atakapohakikishiwa usalama wake.

Amedai kuwa hana uhakika na usalama wake kwa kuwa waliompiga risasi hawajajulikana.

Akizungumza na chombo kimojawapo cha habari cha kimataifa alipoulizwa kuhusu mpango wake wa kurejea, Lissu alidai kuwapo kwa maneno katika mitandao ya kijamii yenye vitisho, hivyo kuleta hofu kwa usalama wake endapo atarejea nchini.

"Wale walionipiga risasi kumi na sita mchana wa saa saba katikati ya nyumba za serikali mjini Dodoma wakati wa kikao cha bunge bado wanaitwa watu wasiojulikana," Lissu alisema.

Akizungumzia kuhusu maneno katika mitandao ya kijamii yenye viashiria vya vitisho kwa usalama wake, Lissu alidai kuwapo kwa vitisho vya wazi vya baadhi ya watu kuwa atakaporudi nchini, watu hao watamshughulikia.

"Kuna maneno yanajitokeza tokeza kwenye hii mitandao ya kijamii kwamba ngoja aje mara hii hatutakosea shabaha... kuna aliyetangaza kwenye televisheni mtandaoni kwamba Lissu akija atapigwa risasi," aliongeza Lissu.

Kuhusu hali yake ya kiafya, Lissu alieleza kuwa ameshapona kabisa baada ya kukamilisha safari yake ndefu ya kimatibabu

INAENDELEA UK.8

# TMA yaonya mvua zaidi

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imesema kuanzia Novemba mwaka huu hadi Aprili mwakani kutakuwapo na mvua za juu ya wastani hadi wastani.

Imewataka wakulima, wavuvi, wachimbaji madini, Wizara ya afya, mamlaka za miji, menejimenti ya hifadhi ya chakula kuchukua tahadhari.

Imesema kutokana na mvua hizo, magonjwa ya mlipuko yanaweza kujitokeza hususani katika maeneo yanye miundombinu hafifu ya maji taka, kwenye miji, pamoja na kusababisha mafuriko.

Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agnes Kijazi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akielezea utabiri wa mvua za msimu kuanzia kipindi cha Novemba mwaka huu hadi Aprili mwakani.

Dk. Kijazi alitaja mikoa itakayokumbwa na mvua hizo ni Dodoma, Singida, Tabora, Mbeya, Songwe, Ruvuma, Njombe, Iringa, Kusini mwa Mkoa wa Morogoro, Lindi, Mtwara, Kigoma, Katavi na Rukwa.

"Mvua hizi zinatarajiwa kuanza katika wiki ya nne ya mwezi Oktoba, 2019 kwa maeneo ya Mkoa wa Kigoma na kutawanyika katika mikoa mingine katika wiki ya kwanza ya mwezi Novemba, 2019," alisema na kuongeza:

"Vipindi vya Mvua nyingi vinatarajiwa katika Novemba 2019 na Januari 2020, mvua zinatarajiwa kupungua katika baadhi ya maeneo kwa miezi ya Disemba, 2019 na Februari 2020, katika wiki ya kwanza ya Mei 2020 mvua zinatarajiwa kuwa zimeisha katika maeneo mengi ya nyanda za juu kusini magharibi na pwani ya kusini, kwa maeneo mengi ya kanda ya kati na magharibi mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya Aprili, 2020," alisema Dk. Kijazi.

Alisema kwa mazao yasiyohitaji maji mengi kama vile mahindi, maharage na mtama yanaweza kuathiriwa na hali ya unyevunyevu wa kupitiliza na maji kutuama mashambani.

INAENDELEA UK.8

# Wagonjwa 28,000 wa moyo watibiwa JKCI

**Na Joseph Mwendapole**

WAGONJWA 28,876 wenye matatizo ya moyo wametibiwa kwa kipindi cha miezi mitatu ya Julai hadi Septemba mwaka huu katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI). Hayo yalisemwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Magonjwa ya Moyo, Dk. Peter Kisenge, wakati akieleza taarifa ya kazi zilizofanywa na kurugenzi yake katika kikao cha menejimenti kilichofanyika jana katika taasisi hiyo.

Dk. Kisenge ambaye ni daktari bingwa wa magonjwa ya moyo alisema wagonjwa waliotibiwa katika taasisi hiyo, wanaume walikuwa 12,566 na wanawake 16,310 ambao 6,590 sawa na asilimia 22.8 walikuwa wagonjwa wapya.

"Tumeona wagonjwa kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na visiwani pamoja na nchi za Ethiopia, Malawi, Zimbabwe, Visiwa vya Comoro na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Wagonjwa waliotibiwa na kurudi nyumbani walikuwa 27,882 na 994 walilazwa kati ya hao 500 ni wanawake na 494 ni wanaume idadi ya vifo vikiwa ni asilimia sita," alisema Dk. Kisenge.

Pia alisema watoto waliotibiwa katika taasisi hiyo walikuwa 1,516, wa kike ni 800 na wavulana 716 kati ya hao wagonjwa 374 walikuwa wapya.

"Wagonjwa wengi tuliowaona walikuwa na matatizo ya shinikizo la juu la damu, kutanuka kwa moyo, valvu, matundu, mishipa ya damu ya moyo na magonjwa ya moyo ya kuambukizwa yanayosababisha makovu katika valvu za moyo kutokana na kupata mafindofindo kwenye tezi za koo," alisema.

Vile vile, wagonjwa waliofanyiwa upasuaji wa bila kufungua kifua na kuzibuliwa mishipa ya damu ya moyo pamoja na kuwekewa vifaa vinavyousaidia moyo kufanya kazi vizuri walikuwa 352 kati ya hao watoto 87 sawa na asilimia 24.7 na hakukuwa na mgonjwa aliyepoteza maisha.

Kaimu Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Upasuaji Dk. Anjela Muhozya, alisema wamefanya upasuaji kwa wagonjwa 153 kati ya hao 122 walifanyiwa upasuaji wa moyo wa kufungua kifua, 23 walifanyiwa upasuaji wa mishipa ya damu na wanane walifanyiwa upasuaji wa mapafu.

Changamoto kubwa wanayokutana nayo katika matibabu ya wagonjwa wa moyo, alisema ni wagonjwa wengi kufika katika taasisi hiyo, huku mioyo yao ikiwa imechoka.

Naye Cecilia Nthala kutoka Malawi ambaye mtoto wake anatibiwa katika taasisi hiyo, alishukuru kwa huduma ya matibabu ya moyo aliyoipata.

Enabel

PUBLIC TENDER Ref: TAN 133

Constructions of KALALANGABO FISHING LAND SITE

Enabel, The Belgian Development Agency, works in partnership with the ministry of Natural Resources and Tourism in implementation of Natural Resources and Management Project in Kigoma Region **(NRM LED)** is now inviting suitable and Qualified Constructors to apply for the public tender for works for the constructions of Kalalangabo fishing site in kigoma region.

Details for this tender which include Tender documents and all relevant details are available in enabel webite at: **www.enabel.be** and **https://btctanzania.wordpress.com/**

All local companies and all Contractors are invited to visits the website and apply:

215456202

# Askari 6 wafukuzwa kazi, kufikishwa mahakamani kwa tuhuma za rushwa

**Na Halima Ikunji,** TABORA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Tabora, inatarajia kuwafikisha mahakamani askari sita wa Kituo cha Polisi Igunga, Mtendaji wa Kijiji cha Isakamaliwa na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Zahanati Kijiji, kwa tuhuma za kuomba na kupokea hongo ya Sh. milioni 8.4 toka kwa wananchi akiwamo mzee wa miaka 95.

Kaimu Kamanda wa Takukuru Mkoa wa Tabora, Mussa Chaulo, akitoa taarifa kwa waandishi wa habari mkoani hapa, aliwataja askari wanaotuhumiwa kuwa ni Frank Matiko, Raphael Maliji, Paulo Mbingwa, Lucas Nyoni, Charles Masanja na Lome Laizer, wote wa kituo cha Polisi Igunga. Aliwataja watuhumiwa wengine walioshirikiana na askari hao kuwa ni Mtendaji wa Kijiji cha Isakamaliwa, Edward Kitenya na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Zahanati Kijiji cha Isakamaliwa, Juma Mwangala ambao kwa pamoja walishirikiana kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 8,450,000.

Alidai mtu aliyedaiwa rushwa hiyo ni mzee mwenye umri wa miaka 95, Ngaka Mataaluma, mkazi wa Kata ya Isakamaliwa na mwananchi mwingine, ili wasifikishwe kwenye sheria wakidaiwa kujihusisha na uchawi, uganga wa kienyeji, kumiliki silaha ya moto bila kibali na kukutwa na bangi.

Kamanda huyo wa Takukuru alimtaja mtu mwingine kuwa ni Ngaka Mataluma (81), mkazi wa kijiji hicho ambaye ni mfugaji wa ng'ombe. Alidai siku ya tukio Juni 12, mwaka huu baada ya askari hao kutoka kwa Mataluma, walifika nyumbani kwake na kumpekua wakimwambia anajihusisha na upigaji ramli chonganishi.

Alidai baada ya kukataa walimbeba hadi ofisi ya mtendaji wa kijiji na kumwamuru atoe Sh. milioni nne ili wamwachie, hata hivyo aligoma na kudondoka kwenye kiti alichokuwa amekalia.

Kamanda huyo alidai kuwa baada ya kuona ameanguka askari hao walimwambia atoe Sh. 500,000 na ndipo mwanawe mmoja aliamua kutoa Sh. 450,000, kisha wakaondoka.

Juni 12, mwaka huu, askari hao sita na viongozi wawili wa kijiji walituhumiwa kuomba na kupokea rushwa ya Sh. milioni nane.

Askari hao walirudisha fedha hizo kwa wahusika Agosti 7, mwaka huu.



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Godfrey Simbeye, akifafanua jambo kwa waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu ushiriki wa makandarasi wazawa kwenye miradi ya maendeleo. Kushoto ni Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Salum Shamte. **PICHA: JOHN BADI**

# Leseni madini hadi Baraza la Mawaziri

**Na Gwmaaka Alipipi**

SERIKALI imebadili mfumo wa utoaji leseni za madini na sasa zitatolewa na Baraza la Mawaziri badala ya waziri mwenye dhamana ya sekta hiyo.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi, alisema jana kuwa lengo la mabadiliko hayo ni kuhakikisha nchi inakuwa salama katika masuala ya madini.

"Kampuni yoyote itakayohitaji leseni ya uchimbaji, Waziri wa Madini hataweza kutoa leseni bali Baraza la Mawaziri ndilo lenye mamlaka. "Leseni za migodi hazitolewi na waziri, hadi ijadiliwe katika Baraza la Mawaziri ndipo itatolewa, mawaziri wengi wamekuwa wakiumia si kwa matakwa yao bali kwa wasaidizi wao walio chini," alisema Prof. Kabudi alipokuwa akifungua Kongamano la Kumbukizi ya Walimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

Alisema Wizara ya Madini imekuwa ndiyo wizara yenye shida ambapo mawaziri wake wengi wamekuwa wakiingia kwenye matatizo. Kuhusu maendeleo ya sekta hiyo, alisema mapato yatokanayo na madini yameongezeka kutoka Sh. bilioni 191 mwaka 2016/17 hadi Sh. bilioni 335.18 kwa sasa. "Tangu serikali ya awamu ya tano ilipoingia madarakani, ukusanyaji wa mapato yatokanato ya madini umeongezeka. Hivi sasa Sh. bilioni 335.81 zinakusanywa kutoka Sh. bilioni 191 zilizokuwa zinakusanywa mwaka 2016/17," alisema Prof. Kabudi.

Aidha, Prof. Kabudi alisema serikali itaendelea kusimamia misingi iliyoachwa na Hayati Mwalimu Julius Nyerere, ikiwamo kutofungamana na upande wowote, kuimarisha Jumuiya ya Nchi Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Prof. Kabudi alisema kizazi kinachomjua na kumfahamu Mwalimu Julius Nyerere kinazidi kupungua, hivyo kuna haja ya kuendelea kusimulia mara kwa mara ili wale ambao hawakumwona waendelee kumjua.

"Lengo la kongamano hili ni kuadhimisha miaka 20 baada ya Mwalimu. Ingawa Mwalimu amefariki dunia na hatumwoni, fikra zake bado zinaishi. Misingi aliyoiweka na kuiacha Mwalimu Nyerere bado inaendelezwa na serikali ya awamu ya tano," alisema.

Pia alisema Mwalimu Nyerere alijenga demokrasia, baada ya uhuru alifanya kazi kubwa ya kujenga taifa.

# PM aagiza watendaji kuwezesha vijana

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewaagiza watendaji katika ngazi zote kuhakikisha vijana wanawezeshwa kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Alitoa agizo hilo jana wakati akizindua maadhimisho ya Wiki ya Vijana kitaifa mwaka 2019 kwenye viwanja vya Mpilipili, nje kidogo ya mji wa Lindi.

"Vijana tushirikiane na serikali na kufanya kazi kwa bidii ili kuunga mkono jitihada za serikali yetu ya awamu ya tano inayoongozwa na John Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuwaletea wananchi maendeleo. Hatua hii itatuwezesha kama taifa tuvuke na tufikie uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025," alisema.

Alisema wakati anatembelea mabanda ya maonyesho, ameona ubunifu wa kijana ambaye ameunda mashine ya kumsaidia mtoto njiti apate joto na pia amemuona kijana mwingine ambaye amebuni mtambo wa kupukuchua magunia 100 ya mahindi kwa saa.

Pia alitembelea banda la kikundi cha vijana kutoka China, Korea Kusini, Argentina, Arzebhaijan na Tanzania ambao waliishi kwenye mazingira magumu na wakabadilika na wameamua kushiriki maonyesho hayo ili kuwabadilisha mtazamo vijana wenzao.

"Nimefurahi kuwaona hawa vijana, ninaamini watashirikiana na wenzao wa hapa kuwabadilisha vijana wa Tanzania ili wawe na fikra endelevu."

Akizungumzia mikakati ya kuwawezesha vijana kiuchumi, Waziri Mkuu alisema Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi nchini, imeanza kutoa mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba (greenhouse) katika mikoa yote na halmashauri zote nchini.

Alisema teknolojia hiyo itawasaidia wakulima kupata mazao mengi katika eneo dogo na kupata mazao bora yanayokidhi viwango katika soko la ndani na nje ya nchi. "Kwa kutumia teknolojia hii, vijana wengi watapata ajira katika sekta ya kilimo," alisema.

Waziri Mkuu alisema mkakati huo ni utekelezaji wa agizo la Chama cha Mapinduzi ambacho kinatambua kuwa sekta ya kilimo ndiyo kimbilio la wananchi wengi na kupitia ilani yake ya mwaka 2015 Ibara ya 6 (a) imeielekeza serikali "kuwawezesha wakulima kupata mafunzo ya kilimo cha kisasa, pembejeo, zana za kisasa na wataalamu wa ugani pamoja na mbinu za kuyafikia masoko ya uhakika ya mazao yao."

Wakati huohuo, Waziri Mkuu amesema serikali imeziagiza halmashauri zote nchini kutenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za vijana ikiwa ni pamoja na maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vinavyomilikiwa na vijana.


Reg. NO 136355066

TANZANIA OCEAN CRUISING AND SAFARIS LIMITED,
P.O.BOX 105092, KINONDONI,
DAR ES SALAAM-TANZANIA.

EXTRACT OF A SPECIAL RESOLUTION ON THE VOLUNTARY WINDING UP OF THE COMPANY PASSED AT THE MEETING OF THE BOARD OF DIRECTORS OF THE COMPANY HELD ON 03rd OCTOBER, 2019 AT THE COMPANY'S REGISTERED OFFICE.

At the extra –ordinary meeting of the Board of Directors of **TANZANIA OCEAN CRUISING AND SAFARIS LIMITED** held on 03rd October, 2019, at 4pm at the registered office the following Special resolution was passed and adopted namely:-

**RESOLUTIONS:**

IT WAS RESOLVED THAT the company petition by the end of this month of October, 2019 for voluntary winding up of the company in accordance with **section 335** of the companies' Act, No. 12 of 2002 with effect as soon as the same is passed by the Authority.

**IT WAS RESOLVED THAT** Since The Company Has Not Been Carrying On Any Business Nor Does It Hold Any Property, It Has Decided To Close The Company.

**IT WAS RESOLVED THAT** the Company give **NOTICE of its INTENTION TO APPLY FOR ITS DISSOLUTION in the WIDELY SPREAD NEWSPAPER and a GOVERNMENT GAZETTE NOTICE.**

**IT IS HEREBY CERTIFIED that** the above is a true extract from the Minutes of the Meeting of the Shareholders of the Company and the resolution set forth and comply with the Memorandum and Articles of Association and Regulations of the Companies Act, 2002 of the Laws of Tanzania.

**The resolution was hereby approved by the undersigned.**

..........................................
Mrs. Priscilla Peregrino (Director)

..........................................
Mr. Peter Kwame Assanful (Directo

115457002

# Waziri apiga marufuku maonyesho holela

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, amezipiga marufuku taasisi zilizo chini ya wizara hiyo kila moja kuandaa maonyesho yake na kwa wakati wake, amezitaka ziungane na kuandaa kwa pamoja.

Akifunga juzi maonyesho ya wajasiriamali yaliyofanyika Manispaa ya Singida, Bashungwa alisema mjasiriamali anapokwenda kwenye maonyesho hajui mipaka ya taasisi hizo.

Pamoja na ushauri huo, alionyesha masikitiko yake kwa baadhi ya taasisi za wizara kutoshiriki kwenye maenyesho hayo.

"Lakini jambo ya kusikitisha sikutegemea katika maonyesho haya nisikute ushiriki wa CARMATEC, TIRDO, TEMDO, TANTRADE na BRELA," alisema.

Bashungwa alisema wajasiriamali hao wanaozalisha viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati wanapokwenda kutafuta huduma serikalini hawajui SIDO inaishia wapi, TIRDO inaishia wapi.

"Lakini kwa sababu ya mazoea, nasisitiza taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, zijenge utamaduni wa kushiriki katika maonyesho hayo muhimu.

"Watumie salamu zangu nataka kila mkurugenzi wa taasisi hizi aeleze ni kwa nini hajashiriki katika maonyesho haya. Tutoke kwenye tabia za zamani ya kufuatwa na wananchi ofisini. Hizo zama zimepitwa na wakati," alisisitiza.

Bashungwa aliweka bayana kwamba katika maonyesho hayo, wajasiriamali na wanaviwanda wapatao 567 kutoka mikoa 25 ya Tanzania Bara na nchi mbili za jirani, walijihusisha na utengenezaji wa bidhaa za uhandisi na teknolojia, usindikaji wa vyakula, mboga na matunda, uzalishaji wa bidhaa za ngozi, sabuni na dawa za usafi, nguo na mavazi.

Akimkaribisha Waziri kufunga maonyesho hayo, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, alisema mkoa huo ulivuka lengo la kutekeleza agizo la serikali la kujenga viwnda 100 kwa mwaka na baadaa ya kujenga viwanda 220.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO), Prof. Elifas Bisanda, alimhakikishia waziri kwamba shirika litaendelea kuwawezesha wanaviwanda kupata mashine mbalimbali na kutoa mafunzo kwa kulenga uhitaji wa soko.

Prof. Bisanda alibainisha pia kuwa vituo vya uendeahaji teknolojia vinaendelea kuzalisha mashine ili kusisimua uanzishaji wa viwanda mijini na vijijini kwa kutumia malighafi zinazopatikana katika maeneo husika na pia kutumia fursa ya uwapo wa umeme katika maeneo mengi ya vijijini.



Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Bima ya Britam, Raymond Komanga (kulia), akiwakabidhi taulo za kike, wanafunzi wa Shule ya Sekondari Chanzige, iliyopo wilayani Kisarawe, mkoani Pwani jana, baada ya wafanyakazi wa kampuni hiyo, kukabidhi msaada wa taulo hizo kwa uongozi wa wilaya. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kanyasu aonya wafugaji kushambulia wahifadhi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amelaani vikali tabia ya wafugaji kuwajeruhi, kuwashambulia na kuwaua wahifadhi wanapotekeleza majukumu katika maeneo yao ya kazi.

Kanyasu alikemea hayo jana wilayani Kaliua mkoani Tabora alipokuwa akizungumza na Watumishi wa Hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori ya Isawima kutokana na kifo cha Ofisa Wanyamapori, Pasaka Orwa, kilichotokea hivi karibuni.

Ofisa huyo aliuawa hivi karibuni alipokuwa katika Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya wakati wa operesheni ya kuondoa wafugaji waliokuwa wamevamia katika jumuiya hiyo.

Inadaiwa kuwa ofisa huyo alipoteza maisha baada ya kushambuliwa kwa kupigwa na fimbo sehemu za usoni na kichwani na baadaye kupelekwa katika kituo cha afya cha Kaliua na badaye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tabora ya Kitete ambako baada ya siku moja alifariki dunia.

Akizungumzia mauaji hayo, Kanyasu alituma ujumbe mzito kwa wafugaji kuwa waache tabia ya kuingiza mifugo ndani ya hifadhi na kuwa kifo hicho kiwe cha mwisho kutokea.

Alisema serikali haitakubali kuona maofisa wake wanauawa katika maeneo yao ya kazi huku wafugaji wakiendelea kutamba kwa kuingiza kuingiza mifugo ndani ya hifadhi.

"Kwa yeyote atakayethubutu kufanya tena kitendo hiki, tutakuwa wakali mara 10 zaidi," alisisitiza.

"Hatuwezi kulima kila sehemu, hatuwezi kulisha mifugo kila sehemu na hatuwezi kujenga kila sehemu. Hii itakuwa si nchi lazima maeneo ya hifadhi yaheshimiwe."

Kanyasu pia alitumia fursa hiyo kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kumkamata mmoja wa watuhumiwa aliyedaiwa kushiriki katika tukio hilo.

Hata hivyo, aliwataka polisi wasiishie kumkamata mfugaji huyo tu badala yake wakamatwe wale wote walioshiriki kumshambulia ofisa wanyamapori huyo na pia sheria ifuate mkondo wake ili iwe fundisho kwa wafugaji wote walioshiriki katika ukatili huo

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Abel Busalama, alimweleza Naibu Waziri kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa alipokwenda kupatiwa matibabu katika hospitali baada ya kuonekana ana jeraha ya risasi katika paja.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wakati wa kujiandikisha uchaguzi S/Mitaa ni sasa

**UANDIKISHAJI** wa wapigakura kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ulianza Jumatatu na unatarajia kumalizika Oktoba 14.

Baada ya uandikishaji kumalizika, hatua iyakayofuata ni kampeni ambazo zitafanywa na vyama vya siasa ambavyo vitasimamisha wagombea kwa ajili ya uchaguzi huo ambao utafanyika Novemba 24, mwaka huu.

Hii ni fursa adhimu kwa kila mtu mwenye sifa ya kushiriki kwa maana ya kupigakura kwa ajili ya kuwachagua viongozi wanaowataka kuongoza mitaa, vijiji na vitongozi kwa miaka mitano ijayo.

Hata hivyo, kwa siku za kwanza za uandikishaji, imeonekana kuwa katika maeneo kadhaa nchini wananchi hawajajitokeza.

Katika Jiji la Dar es Salaam kwa siku mbili mfululizo, wananchi wameendelea kusuasua kujiandikisha.

Sababu zilizoelezwa na baadhi ya viongozi katika mitaa mbalimbali ya jiji hilo ni mvua zinazoendelea kunyesha zimesababisha watu wengi kushindwa kujitokeza.

Katika maeneo mengi vituo vilionekana kuwa wazi, huku wananchi wakijitokeza mmoja mmoja. Kwa mfano Mkoa wa Morogoro unatarajia kuandikisha wapigakura 1,423,111, watu 203,553 walikuwa wameandikishwa siku ya uandikishaji ulipoanza juzi.

Pamoja na taarifa za kujitokeza kwa watu wachache kujiandikisha katika siku za mwanzo baada ya uandikishaji kuanza, tunaamini kuwa siku nne zilizobaki watu wengi wenye sifa za kupiga kura watajitokeza na kujiandikisha ili kutimiza haki yao ya kikatiba ya kuwachagua viongozi wanaowataka.

Kuwapo kwa mvua ni changamoto kwa baadhi ya watu kwenda kujiandikisha, lakini hilo lisiwe kikwazo cha kutojiandikisha. Tunasema hivyo kwa kuwa bila mtu kujiandikisha mhusika atakuwa amekosa fursa ya kuwachagua viongozi anaowataka. Ikumbukwe kuwa mtu asipopiga kura, atakuwa amechangia pengine kupatikana kwa viongozi wasiofaa kwa kuwa kama angepiga kura, kura yake ingebadilisha matokeo, hivyo wenye sifa wapige kura.

Aidha, kwa kufanya hivyo, ni kuondokama na baadaye kulalamika na kujutia kuwa kama angepiga kura viongozi wasiofaa wasingechaguliwa.

Tunawakumbusha viongozi wa madhehebu ya dini na mamlaka nyingine husika kutimiza wajibu wao wa kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kwenda kujiandikisha katika vituo vilivyopangwa kwa ajili hiyo.

Jambo moja ambalo kila mmoja anapaswa kulielewa ni kuwa uchaguzi wa serikali za mitaa una umuhimu mkubwa, kwa sababu viongozi wanaopatikana ndio wenye dhamana na wajibu wa kuwahudumia wananchi moja kwa moja katika maeneo yao. Pamoja na mambo mengine viongozi hao ambao ni wenyeviti wa mitaa, vitongoji na vijiji pamoja na wajumbe wao, wanahusika kusimamia sheria, maendeleo na kusikiliza kero pamoja na kuzipatia ufumbuzi kwenye maeneo yao.

Ili kuwapata viongozi wenye sifa za kusimamia maendeleo na kutatua kero mbalimbali, wananchi wanatakiwa kujiandikisha na kupiga kura baada ya kusikiliza mikutano ya kampeni zao.

Bila shaka wananchi watajitokeza kuwasikiliza katika kampeni kuhusu mipango na mikakati yao ya kuleta maendeleo, na hatimaye siku ya uchaguzi kuchagua wanaofaa. Lingine la msingi ni kuwa watakaochaguliwa wawe ni watu waadilifu, wazalendo na wenye kutenda haki kwa watu wote bila kujali itikadi zao za kisiasa, dini na mambo mengine ya kubaguana.

Tunaamini kuwa Wizara ya Tamisemi itausimamia uchaguzi huo kwa haki hatika hatua zote kuanzia kujiandikisha, kampeni, upigaji kura na kutangaza matokeo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Uchafu tabia za watoto tunaendaje nayo Kivule?

Na Yasmine Protace

**UKATILI** wa kijinsia umekuwa ukipingwa katika maeneo mbalimbali nchini, kutokana na kukiuka haki za mtu anayefanyiwa ukatili huo.

Katika kupambana na matukio hayo, serikali imeweka madawati katika vituo vya afya, pale anapofanyiwa mtu matendo hayo, anapaswa kupatiwa huduma muhimu za kimatibabu.

Ni jambo ambalo kero yake sasa inahusu sehemu kubwa ya umma. Kuna asasi mbalimbali zimekuwa zikilaani matukio hayo na kuamua kutoa elimu kwab jamii jinsi ya kujikinga nayo.

Pamoja na jitihada hizo za serikali, bado kuna baadhi ya jamii nao watoto wanaofanyiwa matukio hayo na wamekuwa wakishindwa kutoa ushirikiano kwa polisi wakikumbatia dhana ya 'kumalizana wenyewe' huku wakijua wanamuumiza aliyetendewa kitu hicho.

Diwani wa Kata ya Kivule jijini Dar es Salaam, Willson Mollel, anakiri kupata taarifa chafu katika kata yake na kwamba wanachukua hatua ya kutoa elimu mbalimbali na akisema kuna hatua.

Mollel anasema katika moja ya shule zilizoko katika kata yake, mwanafunzi wa sekondari alituhumiwa dhidi ya vitendo hivyo kwa mtoto wa shule ya msingi wa kata nyingine.

Cha kushangaza, inadaiwa mwanafunzi wa shule ya msingi aliyetendewa amehamishiwa mkoa tofauti na anaendelea na masomo na aliyeathiriwa, kwa sasa hafiki shule, jitihada za kumtafuta zikiendelea.

Inadaiwa kijana anayetuhumiwa kutenda kosa haishi na wazazi wake wawili na simu ya mzazi wake inaelezwa haipatikani kwa sasa.

Malalamiko ni kwamba, mtoto huyo kuhamishwa na kutoweka ni kitendo cha makisa, kwa sababu ni kumpotezea haki yake.

> **Pamoja na jitihada hizo za serikali, bado kuna baadhi ya jamii nao watoto wanaofanyiwa matukio hayo na wamekuwa wakishindwa kutoa ushirikiano kwa polisi wakikumbatia dhana ya 'kumalizana wenyewe' huku wakijua wanamuumiza aliyetendewa kitu hicho.**

Kwa nini hivyo? Malalamiko yako ikiwamo kutoka kwa Diwani Miolle, akilalamikia tabia mbaya kwa vijana wadogo, ikiwamo uvutaji bangi.

Diwano Mollel anasema kuna wakati uongozi wa polisi kituo cha Stakishari Ukonga, uliwaita madiwani wote wa kata zinazozunguka eneo hilo, pamoja na wenyeviti wa serikali za mitaa, kujadili jinsi ya kutokomeza uvutaji bangi katika maneo yao.

Mwalimu wa shule ya sekondari iliyopo katika Kata ya Kivule, anasema 'vijiwe' vya bangi ni vingi na vinachangia kuwaharibu wanafunzi.

Anasema, pia kuna baadhi ya majengo ambayo hayajakamilika, kwamba ni tatizo linalokaribisha uvunjaji sheria kwa watoto.

Mwalimu anakiri kulijua tukio chafu lililowakuta wanafunzi wao, ikiwa matunda ya kazi ya klabu za wanafunzi inayoratibiwa na jumuiya anayoitaja kwa kifupi, GDSS, kwamba ilitoa taarifa ya mwanafunzi kulawitiwa na mwanafunzi mwenzake. Smulizi yake ni kwamba, baada taarifa hiyo, walimhoji mwanafunzi huyo na akakubali kuwa aliwavutisha bangi watoto watano wa shule ya msingi na ndipo alipowalawiti kwa zamu.

Anasema pamoja na mwanafunzi huyo kukiri, alipotea shule na mpaka sasa hajaonekana.

Kwa mujibu wa mwanaharakati Selemani Bishagazi, matukio ya ulawiti mengi yanatokana na mfumo wa maisha uliopo.

Anataja mojawapo ni wavulana kulala chumba kimoja na wengine kulala na ndugu zao wa jinsia moja.

## HABARI KITAIFA

# JPM ataka mawaziri wenye moyo wa utume

**Na Mary Geofrey**

RAIS John Magufuli, amesema wakati wa uongozi wake anataka mawaziri wenye moyo wa utume wa kutumikia wananchi na siyo wananchi kwenda kwa viongozi.

Alisema wakuu wa mikoa nao wamekuwa wakifanya kazi bila kuchoka wala kupumzika katika kuhakikisha wanashughulikia kero za wananchi.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi katika Uwanja wa Azimio, wilayani Mpanda mkoani Katavi katika mwendelezo ziara zake mkoani humo.

Alisema kazi anayofanya ni kusimamia na kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mpinduzi (CCM) na kutokana na kazi nzuri inayofanywa na serikali imemaliza tatizo la wanachama wake kupigwa mawe walipokuwa wakivaa sare za chama hicho.

Alisema ilifika wakati wanaovaa sare ya kijani walikuwa wakipondwa mawe, lakini sasa hawapondwi mawe, "leo atokee wa kuwaponda mawe eeeh!"

Alimuagiza Mkuu wa mkoa huo, Juma Homera, kuhakikisha anashughulikia kero zote za wananchi ambazo zinatokana na dhuluma.

Rais Magufuli pia aliagiza kuanzia Jumatatu wiki ijayo Shirika la Ndege (ATCL), lianze kupanga safari na kwenda mkoani Katavi katika Uwanja wa Ndege Panda hata kama ni safari moja kwa wiki.

"Waziri naomba uwaambie watu wa ATCL kuanzia Jumamosi waanze kupanga safari za ndege kuja Mpanda, na mimi siondoki Mpanda mpaka nipande ndege," alisisitiza.

Alisema awali walikuwa na changamoto ya uwanja kuwa mdogo, lakini kwa sasa umefanyiwa maboresho hivyo ndege zinaweza kutua eneo hilo la kuchochea utalii katika mkoa huo.

Aliwataka kujenga hoteli kwa ajili ya kukuza uchumi wa wananchi wa mkoa huo na kuchangamkia fursa za kufanya biashara mbalimbali ikiwamo ya kuuza dhahabu.

Kadhalika, aliwaagiza Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (Tanapa), kupeleka maji katika eneo wanakoishi viboko katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi ambao kwa sasa hawana maji ya kutosha.

"Tanapa Mchimbe bwawa, mjaze maji ili viboko wakae humo kwa sababu ukimkamua ng'ombe anatakiwa kula majani na hawa viboko muwawekee maji kwa maana wamekaukiwa hadi wamepasuka. Kuanzia kesho (leo) muanze kusombelea maji mpeleke eneo la Viboko," Rais Magufuli alisema.

Vile vile, alisema hatoacha kuelezea mafanikio yanayofanywa na serikali katika miradi mbalimbali ya maendeleo kwa sababu ndio kipimo cha kujipima katika maendeleo.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akitazama chupa yenye dawa za kulevya, alipotembelea banda la Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya baada ya kufungua maadhimisho ya wiki ya Vijana Kitaifa kwenye Viwanja vya Mpilipili mjini Lindi jana. Kushoto ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Ajira, Vijana, Kazi na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama na wa pili kulia ni Kamishna wa Kinga na Tiba wa Mamlaka hiyo, Peter Mfisi. **PICHA: OWM**

# Sheria ya Ajira yalalamikiwa

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI Mtendaji wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Dk. Aggrey Mlimuka, amesema wanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika Sheria ya Ajira ya Mwaka 2004 zinazohitaji kufanyiwa mabadiliko ili kuleta tija kwa waajiri.

Akizungumza na waandishi wa habari katika maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja, Dk. Mlimuka, alisema sheria hiyo imewabana waajiri katika saa za kufanya kazi.

Alisema kwa sasa sheria inamtaka mwajiriwa kufanya kazi kwa saa 45 kwa wiki jambo ambalo linawanyima waajiri muda zaidi wa kuzalisha.

Katika sheria hiyo, alisema inawataka waajiri kuwalipa fedha za muda wa ziada kwa wafanyakazi waliozidisha muda wa kazi badala ya kuwapa muda wa kupumzika.

Pia katika sheria hiyo inaamuru kutoa fidia kubwa kwa wafanyakazi walioachishwa kazi kutokana na sababu mbalimbali. Vile vile, alisema kulingana na uchumi wa sasa kufunguliwa na kufungwa kwa biashara ni kitu cha kawaida ingawa sheria inalazimisha ukiwa na biashara ama la, kubaki na wafanyakazi na kuwalipa jambo ambalo linawaumiza. Alisema Wiki ya Huduma kwa Wateja, watapokea mrejesho kutoka kwa wanachama wao namna wanavyotoa huduma zao.

Watapokea pia mapendekezo ya namna bora ya kuboresha huduma zinazotolewa na chama hicho kwa wanachama wake.

# Asilimia 70 ya miji haijapangwa nchini

**Na Salome Kitomari**

ASILIMIA 70 ya miji nchini haijapangwa, huku serikali ikiandaa programu ya taifa kurasimisha na kuzuia ukuaji wa makazi holela 2013-2023.

Hayo yalibainishwa juzi jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendelea ya Makazi, Angela Mabula, wakati wa kongamano la siku ya miji endelevu lililoandaliwa na Ubalozi wa Ufaransa kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kuondoa Umaskini (Repoa).

Alisema kiwango hicho kimeanza kupungua kufikia asilimia 53 hadi 58 kutokana na juhudi za serikali za kushirikisha sekta binafsi katika upangaji na upimaji majiji.

"Programu hiyo inalenga kuzuia ongezeko la makazi holela mijini, kuwekeza kwenye huduma za kiuchumi na kijamii ili kuboresha maisha ya wakazi wa maeneo hayo na kuongeza usalama wa milki za ardhi," alisema.

Waziri huyo alisema hadi Julai vipande vya ardhi 699,791 vilikuwa vimerasimishwa katika mamlaka mbalimbali za upangaji nchini, huku mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 2,195 imeandaliwa.

"Katika kuwezesha usalama wa milki jumla ya vipande vya ardhi 320,277 vimehakikiwa na kupimwa kwa ajili ya kutoa hakimiliki za kimila. Jumla ya hati 146,084 zimeandaliwa na kugawiwa wamiliki," alisema.

Kwa mujibu wa Mabula, miji ya Tanzania inakuwa kwa kiwango cha asilimia 5, ambao hauendani na upatikanaji wa huduma muhimu za afya, elimu, usafiri wa umma pamoja na miundombinu ya umeme na barabara.

Alisema ukuaji wa miji unakabiliwa na changamoto za ongezeko kubwa la idadi ya watu lisilokwenda sambamba na upatikanaji wa huduma muhimu, ongezeko la makazi yasiyopangwa katika maeneo hatarishi na yaliyojengwa kwa shughuli za umma.

Nyingine ni uhaba wa nyumba za kuishi zenye bei nafuu, mafuriko wakati wa mvua, uchafuzi wa mazingira na hali ya hewa unaosababishwa na utupaji ovyo wa taka ngumu na utiririshaji wa maji machafu na umaskini utokanao na watu kukosa ajira.

Mabula alisema ili kuongeza kasi ya upangaji na upimaji wa miji, serikali imejenga mazingira ya kuwezesha sekta binafsi kushiriki katika eneo hilo, na jumla ya kampuni za upangaji 67 zimesajiliwa na bodi ya maofisa miji na kampuni 84 za upimaji ardhi zimesajiliwa na bodi ya wapima ardhi.

"Serikali imeweka mazingira mazuri kwa waendelezaji milki kushiriki katika ujenzi wa nyumba za kupangisha na kuuza kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa nyumba za kuishi na biashara," alisema.

HABARI KITAIFA

# Kitambulisho cha NEC hakimo uchaguzi mitaa

INATOKA UK. 2

na hairidhishi na vile walivyotarajia.

Urio alisema katika Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002, inaonyesha kuwa idadi ya wananchi katika kata hiyo ni zaidi ya 100,000 na kwamba wanategemea kwamba idadi ya watakaojiandikisha haitapungua sana.

**ACT-WAZALENDO WASAMBAZA UJUMBE**

Chama cha ACT-Wazalendo nacho kimeamua kutumia mitandao ya kijamii kuhamasisha uandikishaji huo.

Uhamasishaji katika chama hicho, unaoongozwa na Kiongozi wake Mkuu, Zitto Kabwe ambaye ameamua kutumia mitandao ya Instagram na mingineyo kufanya kazi hiyo ya uhamasishaji.

"Je, umejiandikisha kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa 2019? Muda umewadia, tutumize yale tunayoyasema, ya kuwa tunataka serikali ya wananchi inayotokana na wananchi, ni muhimu kujiandikisha ili uweze kupiga kura," ilisema sauti ya Zitto ambayo amerekodi na kuweka kwenye akaunti zake za mitandao ya kijamii.

Katika akaunti hizo za Zitto, pia amerekodi sauti ya Naibu Kiongozi wa Chama hicho, Juma Duni Haji, ambaye naye anafanya uhamasishaji huo.

"Mwananchi nenda kajiandikishe ili uwe sehemu ya kushiriki kikamilifu katika mabadiliko tunayoyataka Watanzania. Mabadiliko hayawezi kutokea kama wewe mwananchi hujashiriki katika uchaguzi. Mabadiliko hayaanzi mjini au kwenye serikali za mtaa, yanaanza kwako. Wewe ndiye unayeishi kwenye mtaa, ndiye utakayeleta mabadiliko bora ya serikali ya mtaa," anahamasisha Duni Haji.



Mchuuzi wa mihogo ya kukaanga akifagia kuondoa maji yaliyotuama katika eneo lake la biashara, Mazense, kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Rugemalira, Seth wajisalimisha kwa DPP

INATOKA UK. 2

na Sh. 309, 461,300,158.27.

Vile vile, washtakiwa wote wanadaiwa kuisababishia serikali hasara na inadaiwa walitenda makosa hayo Novemba 29, 2013 katika Benki ya Stanbic tawi la kati Kinondoni, kwa vitendo vyao waliisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani 22, 198, 544.60 na Sh 309,461,300,158.27.

Kati ya Novemba 29, 2013 na Januari 23, 2014 maeneo tofauti ya Dar es Salaam kwa pamoja walidaiwa kutenda kosa la kutakatisha fedha kwa kuchukua fedha kutoka BoT ambazo ni Dola za Marekani milioni 22.1 na Sh. bilioni 309.4, wakati wakijua fedha hizo ni zao la kujihusisha na genge la uhalifu.

**WAACHIWA HURU**

Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Arusha, Rose Ngoka, jana aliwaachiwa huru washtakiwa watatu waliokuwa wanakabiliwa na kesi ya utoroshaji madini ya Sh. milioni 958, baada ya kulipa faini Sh. milioni 100 na fidia Sh. milioni 10.

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Ngoka alisema kulingana na makubaliano ya Mkurugenzi wa Mashitaka nchini (DPP),

mshtakiwa wa tatu, Bakari Kunga, aliyehukumiwa kulipa Sh. milioni 110 kwa awamu saba, ameshalipa awamu ya kwanza Sh. milioni 10 ya faini na fidia Sh. milioni 10 na kubakiza Sh. milioni 90, mahakama imemwachia huru.

Ngoka alisema pamoja na kumwachia huru, mshitakiwa huyo atatakiwa kulipa Sh. milioni 15 kila mwezi na kuhakikisha anamaliza kulipa fedha hizo Aprili 10, mwakani.

"Pamoja na kuachiwa huru, mahakama imeamuru hati ya nyumba yake namba 125 yenye hati namba 11394 iliyoko Kitalu E eneo la Njiro Jijini Arusha itaendelea kushikiliwa na DPP hadi atakapokamilisha kulipa fedha hizo," alisema.

Hakimu Ngoka alisema endapo mshtakiwa huyo atashindwa kulipa fedha hizo, DPP atachukua uamuzi kwa sababu anao uwezo kisheria wa kufanya hivyo.

Kwa upande wa washtakiwa Latifa Mwarengwa na Josephat Shayo, alisema wamelipa Sh. milioni 45 kila mmoja, hivyo mahakama kuwaachia huru.

Kabla ya hukumu hiyo kutolewa, Mawakili wa Utetezi Anold Ojare na Said Amour, waliiambia mahakama hiyo kuwa upande wa Jamuhuri na utetezi waliushakubaliana kuwa fedha hizo zilipwe kwa awamu saba na tayari washtakiwa wameshatimiza makubaliano hayo, hivyo kuomba mahakama iwaachie huru.

Washtakiwa hao walikuwa wakikabiliwa na kesi ya kutorosha madini kilo 31.59 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 416,577.58 sawa na Sh. milioni 958

Madini hayo yalikuwa aina ya tanzanite, sapphire, spinel, ruby, tourmaline, tsavorite, grossular na Aquamarine na yalikuwa yakitoroshwa kwenda nchini Kenya yakiwa kwenye gari namba T.645 DBY aina ya Suzuki Swift.

**Imeandikwa na Beatrice Shayo, Dar es Salaam na Cynthia Mwilolezi, Arusha**

# Lissu agoma kurejea, ahofia usalama wake

INATOKA UK. 3

iliyoanza tangu Septemba 9, mwaka juzi jijini Dodoma na baadaye jijini Nairobi na nchini Ubelgiji alikokamilisha matibabu yake, hivyo kueleza kuwa sio sababu tena ya kuendelea kumuweka nje ya nchi.

Gazeti hili lilimtafuta Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola ili kufahamu mikakati ya serikali ya kiusalama kwa Lissu, lakini alielekeza atumiwe ujumbe mfupi wa maandishi.

Hata hivyo, alipotumiwa hakujibu mpaka gazeti hili linakwenda mtamboni.

Alipoulizwa Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Simon Sirro, msaidizi wake alidai kuwa Mkuu huyo yupo kwenye kikao, na kutaka atafutwe baadaye, lakini alipotafutwa alidai bado yuko kwenye kikao, na hadi tunakwenda mitamboni hakupatikana.

Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Robert Boaz, naye alidai yupo kwenye kikao na mpaka gazeti linakwenda mitamboni.

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, alipoulizwa kuhusu hatua zinazochukuliwa na chama hicho kuhusiana na usalama wa Lissu, alidai yupo msibani, hivyo kutaka atafutwe baadaye.

Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho Bara, John Mnyika, ambaye alielekeza atafutwe Mkuu wa Habari na Mawasiliano, Tumaini Makene, ambaye aliahidi kutoa taarifa kuhusu suala hilo, lakini mpaka tunakwenda mtamboni taarifa hiyo haikuwa tayari.

Lissu ambaye awali alinukuliwa na vyombo mbalimbali vya habari akisema angerejea nchini Septemba 9, mwaka huu, aliahirisha uamuzi huo kwa madai ya kutoruhusiwa na madaktari wake kurejea nchini, na kwamba alitakiwa kumwona kwa mara ya mwisho Oktoba Mosi na 8 mwaka huu.

# TMA yaonya mvua zaidi

INATOKA UK. 3

"Magonjwa ya wanyama na uharibifu wa miundombinu ya kilimo vinaweza kujitokeza kutokana na mvua zisizotarajiwa, malisho na upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo na wanyama pori vinatarajiwa kuwa vya kuridhisha katika maeneo mengi," alisema.

Alisema utabiri unaonesha kutakuwa na maji ya kutosha na ziada katika maziwa na mabwawa hali inayotarajia kuchangia kuongezeka kwa chakula cha samaki, kuongezeka kwa uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya uvuvi.

"Wavuvi wanashauriwa kufuatilia pia utabiri wa hali ya hewa unaotolewa mahususi kwa matumizi katika maziwa makuu na bahari," alisema Kijazi.

Kijazi alisema ni vema maghala ya kuhifadhia chakula yaimarishwe katika ngazi mbalimbali ili kuwa na nafasi ya kutosha kuhifadhi ziada ya chakula kitakachozalishwa.

Alisema ni vizuri kuandaa na kusambaza viwatilifu vya kutosha kwa wakati ili kukabiliana na ongezeko la wadudu waharibifu mashambani na kwenye maghala ya kuhifadhi chakula.

Alisema wachimbaji wa madini hususani wadogo wanashauriwa kuwa makini kwani ongezeko la maji katika udongo linaweza kusababisha maporomoko ya ardhi na maji kujaa kwenye migodi.

Alisema upatikanaji wa maji kwa ajili ya umwagiliaji na matumizi ya nyumbani unatarajiwa kuwa mzuri.

Alisema Mamlaka za miji na Jiji zinashauriwa kuchukua hatua stahiki kuhakikisha kuwa mifumo ya njia za kupitisha maji zinafanya kazi vizuri ili kuepusha maji kutuama na kusababisha mafuriko, uharibifu wa miundombinu na vifo.

HABARI KITAIFA

# Walimu waomba kuboreshewa mazingira

**Beatrice Philemon**

WALIMU wa shule za sekondari jijini Dar es Salaam, wameiomba serikali iboreshe mazingira ya kufanyia kazi.

Mambo hayo ni ofisi, nyumba za walimu, maslahi bora kwa walimu vijana na motisha kwa walimu ili kuvutia vijana wengi kufanya kazi ya ualimu na kusaidia walimu kutoa elimu bora kwa wanafunzi.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu.

Hayo yalisema na Katibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Wilaya ya Ilala, Vicky Kibona, alipokuwa akichangia mada kuhusu chama hicho kina mkakati gani wa kuvutia vijana katika taaluma ya ualimu katika maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani.

Alisema ili kuvutia vijana wengi kuingia katika fani ya ualimu, serikali ijitahidi kuboresha maslahi ya walimu, kutoa mishahara kwa wakati, kutoa motisha kwa walimu na hii itasaidia kwa kiasi kikubwa walimu wengi kujikita zaidi kufundisha watoto, kutoa elimu bora na kusaidia walimu kukidhi mahitaji yao.

"Uwezi kumfundisha mwanafunzi kama mfukoni huna hela wala mazingira ya shule siyo mazuri kwa sababu muda mwingi unawaza jinsi ya kupata fedha ili kukidhi mahitaji yako," alisema.

Pia walimu waliomba posho za walimu ziende kituoni mapema kabla mwalimu hajaajiriwa ili akifika kituoni akute posho yake ili kuondoa usumbufu wa kusubiri posho.

Pia waliiomba serikali itoe mafunzo kwa walimu ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknologia, wafanye kazi kwa ufanisi na kuboresha fani zao.

"Katika suala la mafunzo, walimu wanaona wamesaulika hawapati mafunzo ya mara kwa mara," alisema.

Alisema utoaji wa mafunzo ya mara kwa mara kwa walimu, motisha na mshahara kutolewa kwa wakati, utasaidia vijana wengi wapende fani hiyo, CWT itaendelea kuzungumza na serikali ili iboreshe mazingira ya walimu.

Akizungumzia maadili ya ualimu, aliomba vyuo vikuu vifundishe maadili ya ualimu kwa sababu walimu wengi wanashindwa kuendana na maadili ya ualimu ndiyo maana fani ya ualimu haithaminiwi.

Naye Meneja Mkuu wa Jukwaa la Shule Direct, Iku Lazaro, aliwaomba walimu wa shule za sekondari nchini kutumia jukwaa la "Shule Direct' kufundisha wanafunzi na pia wanafunzi kusoma masomo mbalimbali.

Mpaka sasa Jukwaa la Shule Direct limefikia zaidi ya walimu 30,000 wanaolitumia kufundisha masomo mbalimbali kwa kufuata mtaala wa elimu.

"Mwalimu yeyote Tanzania anaweza kutengeneza nyenzo ya kufundishia na kujifunzia na 'kupublish' kwenye jukwaa letu na walimu na wanafunzi wakaweza kusoma," alisema.

Alisema wametoa mafunzo ya Tehama kwa walimu katika shule mbalimbali walizotembelea na kufikia halmashauri za wilaya 10 ikiwamo mikoa ya Kigoma, Iringa, Unguja na Pemba na zaidi ya walimu 30,000 wanatumia jukwaa la Shule Direct.

"Jukwa la Shule Direct linatoa fursa ya wanafunzi kujifunzia tofauti na kutegemea mwalimu mmoja na fursa kwa walimu kutumia teknolojia ya Tehama kufundishia,"alisema.

Vile vile wameweza kufikia watu wenye ulemavu wa kusikia na kutoa kompyuta katika shule tatu za sekondari katika mkoa wa Njombe ili waweze kujifunza Tehama, lakini kutumia jukwaa letu kujifunza masomo mbalimbali.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya TPB, Sabasaba Moshingi (wa pili kushoto), akikabidhi sehemu ya mifuko 100 ya saruji pamoja na matofali 1000, vyenye thamani ya Sh. milioni 3.5 kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Nduruma, Hilda Zoya, kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike shuleni hapo, Kata ya Moshono, mkoani Arusha juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Fursa ya elimu hadi chuo kikuu

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wamefunguliwa fursa ya elimu kwa watoto wao kusoma hadi chuo kikuu, baada ya Benki ya DCB kuzindua akaunti maalumu ya akiba ya mpango wa elimu.

Akaunti hiyo inajulikana kama DCB SKONGA ikilenga kumhakikishia mteja kuweka akiba na uhakika wa elimu ya mtoto wake hadi chuo kikuu.

Akizungumza katika uzinduzi wa akaunti hiyo jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya DCB, Godfrey Ndalahwa, alisema: Ni akaunti maalum ya akiba inayompa mteja fursa ya kuweka akiba kila mwezi ili kutimiza malengo aliyo jiwekea huku mteja akihakikishiwa elimu ya mtoto wake hadi chuo kikuu."

Alisema wanaamini katika kutoa fursa zenye tija kwa wateja wao na Watanzania kwa ujumla kwa kuja na bidhaa nzuri zinazowapa tija na faida lukuki.

Alisema kumekuwapo na changamoto kubwa sana katika jamii inayowazunguka pindi mzazi/mlezi anayetegemewa na familia anapoteza maisha au kupata ulemavu wa kudumu, kwani watoto wengi wanashindwa kuendelea na masomo.

"Hii imetengeneza hofu kwenye familia nyingi. Kutokana na changamoto hizi, tumekuja na bidhaa hii maalum ya mpango wa elimu itakayomwezesha mtoto/watoto kusoma hadi kumaliza elimu yao ya chuo kikuu bila ya shida yoyote," alisema na kuongeza:

Akaunti hii maalum ya akiba inamwezesha mteja kuweka akiba kidogo kidogo kila mwezi kulingana na mpango na gharama za masomo ya mtoto wake."

Naye Mkurugenzi wa Biashara, James Ngaluko aliongeza: "Kupitia bidhaa hii ya DCB Skonga mteja anaweza kuchagua mpango wa aina mbalimbali wa kuweka akiba pamoja na muda wa uwekezaji kulingana na umri, gharama na muda wa masomo ya mtoto wake.

# RC akemea taarifa za udanganyifu lishe

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MKUU wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali (mstaafu) Emmanuel Maganga, amewataka wakuu wa wilaya na wakurugenzi kuepuka kutoa taarifa za udanganyifu.

Maganga alitoa rai hiyo wakati akizungumza kwenye kikao cha tathmini ya utekelezaji wa mkataba wa lishe kwa mwaka 2018/19 jana katika ukumbi wa mkoa, Mnarani mjini hapa.

Alisema wakuu wa wilaya, waganga wakuu, wadau wa maendeleo, Shirika la IMA World Health, USAID Boresha Afya na wakurugenzi wanatakiwa kuacha kutoa taarifa za udanganyifu.

Aliwataka wakurugenzi wote kuhakikisha wanatenga Sh. 1,000 kwa kila mtoto chini ya miaka mitano kila mwaka. "Eneo ambalo limetuangusha zaidi ni la kutenga Sh. 1,000 kwa kila mtoto. Hilo ndilo lilituteremsha sana ingawa wanasema fedha si msingi wa maendeleo. Bila fedha mambo mengi hayaendi, fedha mnazo wakurugenzi za safari sasa mnashindwaje kutenga Sh. 1,000 kwa kila mtoto chini ya miaka mitano? Hii mikataba tunayoingia ni utamaduni mpya kwa Tanzania lakini kwa nchi zingine ni jambo la kawaida," alisema. Mkuu wa Mkoa alisema kiwango cha udumavu ni asilimia 42.3 kwa maana kwamba katika watoto 100 watoto 42 kwa mkoa wa Kigoma wana udumavu.

"Kama hali ni hiyo taifa hilo linakwenda wapi? Tumeambiwa mtoto asipopata lishe bora katika siku za mwanzo 1,000, huyo hakuna kupona atakuwa mjinga tu hata ungefanyaje. Sasa sisi tumepewa dhamana kwa maana ya wataalamu kusaidiana na wananchi wala si jambo la ajabu," alisema.

Ofisa Lishe Mkoa wa Kigoma, Naomi Rumenyela, alisema lengo kuu la kikao hicho ni kupeana mrejesho wa utekelezaji wa mkataba wa lishe ili kubaini maeneo ya kuwekewa mkakati.

## Makonda azindua mfumo kupokea kero

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amezindua mfumo wa kuwawezesha wananchi kuwasilisha kero na changamoto walizonazo kwa kutumia simu ya mkononi au kompyuta.

Huduma hiyo itawezesha watendaji kupata ujumbe na kutoa majibu ndani ya muda mfupi kwa lengo la kuokoa muda na gharama za usafiri kufuatilia changamoto.

Makonda alizindua mfumo huo jijini humo na kusema kuwa ameamua kuanzisha mfumo huo baada ya kubaini wananchi wengi wamekuwa wakifika kwenye ofisi za umma na kuzungushwa muda mrefu.

"Nimeamua kuzindua mfumo huu kwa sababu nimebaini kuwa wananchi wanapewa majibu ya kupigwa kalenda mara njoo kesho pasipokujua kuwa wamepoteza muda na nauli zao kufuata huduma wanazotaka," Makonda alisema.

Makonda alisema mfumo huo utakuwa ukipokea taarifa za malalamiko ya watendaji wasiowajibika kuanzia ngazi ya mtaa, kata, wilaya hadi mkoa na taarifa zitawafikia viongozi wote.

"Taarifa zitawafikia viongozi wote kwa wakati kuanzia mimi mwenyewe, Mkuu wa Wilaya husika, Mkurugenzi, Katibu Tawala na Mkuu wa Idara na zitafanyiwa kazi kwa wakati," Makonda alisema.

Kadhalika, Makonda aliwahimiza wananchi kutumia mfumo huo kueleza kero zote zinazowakabili ikiwamo afya, barabara, elimu, maji, umeme, miradi inayokwama pamoja na kutoa taarifa pindi wanapobaini uhalifu kwenye mitaa yao.

Alisema wananchi watatoa taarifa zao kwa kutuma ujumbe mfupi wa maneno kwa kuandika neno DSM kisha eleza changamoto zako kisha tuma kwenye namba 11000 au ingia kwenye Website www.malalamiko.dsm.go.tz na ujumbe utapokelewa mara moja na kupewa mrejesho.

# NEMC kushushia rungu wanaotiririsha majitaka

**Na Enok Charles**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limetoa onyo kwa wote ambao wamekuwa na tabia ya kutapisha vyoo hasa katika kipindi hiki cha mvua.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema tabia hiyo imekithiri miongoni mwa wananchi hali inayochangia kuibuka kwa magonjwa ya milipuko.

"Baadhi ya wananchi wamekuwa na tabia ya kutapisha vyoo vyao hususani katika kipindi cha mvua za vuli au masika hali inayosababisha mlipuko wa magonjwa kama kipindupindu na homa za matumbo, tunawaonya watu hao kuacha tabia hiyo mara moja," alisema. Onyo hili pia limewagusa wamiliki wa viwanda ambao wamekuwa na tabia ya kutiririsha maji machafu kwa kuyaelekeza kwenye mito, mabonde au makazi ya watu ambayo yamekuwa na kemikali zenye sumu zinazoweza kuathiri watu na viumbe vya majini.

"Ukiondoa utapishaji wa majitaka majumbani, lakini viwanda navyo vimekuwa vikizalisha maji machafu yenye kemikali za sumu ambazo zimekuwa na madhara zaidi kwa wananchi na viumbe vya majini, tunawataka waache mara moja au wafaute taratibu za Dawasa kwa kuyatibu kwanza hayo maji kabla hayajatelekezwa kwenye mito," alisema.

Alizitaja hatua zilizochukuliwa mpaka sasa katika kudhibiti utapishaji wa maji taka kuwa ni kukutana na viongozi wa halmashauri nchini ili kutengeneza kanuni na taratibu ambazo zitachangia kutokomeza utapishaji na utirirshaji wa taka zenye sumu kwenye makazi ya watu, mito na mabonde.

"Tumeshachukua hatua kadhaa katika kudhibiti wenye viwanda na watu wanaotiririsha maji taka ambapo kwa Dar es Salaam tumeshasambaza maofisa wa mazingira 100 na pia tumeongea na viongozi wa halmashauri kwa lengo la kutengeneza kanuni na taratibu za usimamizi." Aidha, alisema kuwa, madhara yanayotokana na tabia hiyo ya utiririsha majitaka na yale yenye kemikali zenye sumu ni pamoja na serikali kutumia gharama kubwa kuwahudumia waathirika wa kadhia hiyo.

"Madhara ya maji haya sio kwamba yanasababisha magonjwa tu kwa wananchi na viumbe vingine, bali hata serikali imekuwa ikitumia gharama kubwa katika matibabu ya wagonjwa na hata katika kuyatibu maji ya mito kwa usalama wananchi na mifugo."



Ofisa wa Ubalozi wa Marekani, Bibi Brinille Ellis (kushoto), akimkabidhi moja ya picha za matukio mbalimbali ya Hayati Baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere, zilizotolewa na ubalozi huo, kwa Kaimu Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa, Dk. Gwakisa Kamatula, jijini Dar es Salaam jana, kama sehemu ya kumuenzi katika kumbukizi ya miaka 20 ya kifo chake. **PICHA: MAKUMBUSHO YA TAIFA**

# Marekani yamuenzi Mwalimu Julius Kambarage Nyerere

**Na Mwandishi Wetu**

UBALOZI wa Marekani nchini umetoa picha za ziara za kihistoria za Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere nchini Marekani kwa Makumbusho ya Taifa.

Picha hizo zimekabidhiwa kwa Makumbusho ya Taifa jana na Ofisa wa Ubalozi anayeshughulikia Masuala ya Umma, Brinille Ellis.

Picha hizi ambazo ni tangu miaka ya 1960 zinaonyesha jinsi Tanzania ambavyo imekuwa ikishirikiana na nchi ya Marekani.

Ellis alisema kuwa picha hizo zimekabidhiwa kwa Makumbusho ya Taifa kama sehemu ya kumuenzi Mwalimu Nyerere wakati wa kumbukumbu ya kifo chake miaka 20 iliyopita. Ellis alisema vile vile msaada wa picha hizo zilizo katika ubora wa hali ya juu unalenga katika kuimarisha ushirikiano wa muda mrefu uliopo kati ya Tanzania na Marekani. "Tunatoa picha hizi kwa ajili ya kumuenzi Mwalimu Nyerere na kwa ustawi wa ushirikiani wetu na Tanzania," alisema bibi Ellis. Aliongeza kuwa jozi ya picha zilizotolewa katika Makumbusho ya Taifa Dar es Salaam itatolewa pia katika Makumbusho ya Mwalimu Nyerere iliyoko katika Kijiji cha Mwitongo, Butiama. Moja ya picha hizo inawaonyesha Rais wa zamani wa Marekani, Kennedy na Waziri na Mwalimu Nyerere katika Ikulu ya White House jijini Washington DC Septemba 17, mwaka 1961.

Picha nyingine inamwonesha kiongozi wa harakati za kupigania haki za raia, Dk. Martin Luther King Jr, akizungumza na Mwalimu Nyerere katika dhifa iliyoandaliwa na Rais Kenndy huko Washington DC Julai 16, 1963. Picha nyingine ya miaka ya karibuni ni ile inayomwonyesha Rais mstaafu wa Marekani, Jimmy Carter, akimkaribisha Rais mstaafu wa Tanzania, Mwalimu Nyerere, Atlanta, Georgia, Marekani Mei 8, 1998 mwaka mmoja kabla ya kifo chake.

Akizungumza wakati wa kupokea picha hizo jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa, Dk. Gwakisa Kamatula, aliushukuru Ubalozi wa Marekani kwa picha hizo ambazo zitaongeza ufanisi wa maonyesho yanayomhusu Mwalimu Nyerere katika Makumbusho hiyo.

"Tunawashukuru wenzetu wa Marekani kwa mchango wa picha hizi, maana zimekuja katika wakati mwafaka tunapokumbuka miaka 20 tangu kifo cha Mwalimu Nyerere," alisema Dk. Kamatula.

Alisema msaada huu unaonyesha jinsi Mwalimu alivyoweka msingi mzuri wa mashirikiano kati ya Tanzania na mataifa mbalimbali duniani.

# Taasisi, mashirika binafsi waaswa

**Na Allan Isack**, ARUSHA

TAASISI, mashirika binafsi na asasi za kiraia, zimetakiwa kushirikiana na serikali ili kujenga jamii bora na taifa lenye maendeleo.

Wakizungumza katika mkutano uliofanyika jana mkoani hapa na kuwakutanisha wakurugenzi wa taasisi hizo, walisema kuna haja ya kujenga ushirikiano na mshikamano ili kujenga taifa imara na la kiuchumi.

Mkurugenzi wa Shirika la Ujamaa Community Resources, Marcos Nandei, alisema mashirika hayo, yanapaswa kujenga uhusiano mzuri na serikali ili kuwahudumia wananchi.

"Kila taasisi au shirika likifanya mambo yake binafsi bila kushirikiana na serikali au wao kwa wao ni vigumu kupiga hatua za kimaendeleo katika harakati ya kuhudumia jamii," alisema Nandei.

Hata hivyo, alisema kuna umuhimu kwa mashirika hayo na taasisis hizo, kutengeneza agenda ambazo zitawafanya kuwa na sauti moja wakati wa kufanya mazungumza na serikali kwa mstakabali wa taifa la Tanzania.

Alieleza katika mkutano huo, mashirika na taasisi hizo, zitajengewa uwezo wa kiutaalamu na kiutendaji wakati wa kutoa uhuduma kwenye jamii inayowazunguka.

Alisema awali kulikuwapo na changamoto kwa baadhi ya taasisi hizo, kuwa na matumizi mabaya ya rasilimali na kutokuwa na uratibu mzuri wa shughuli zinazofanyika kwenye jamii.

Katibu Mtendaji wa Tasisi ya Angonet, Peter Bayo, alisema awali kulikuwapo na mashirika na taasisi ambazo zilikuwa zikiomba fedha kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kusaidia jamii, lakini fedha hizo zilikuwa hazifiki kwa walengwa.

"Tumejaribu kuyahimiza mashirika na taasisi hizi kama wanahudumia jamii basi wafanye hivyo, pia kama hawawezi kutoa huduma kwa umma bora wakatafute kazi nyingine za kufanya na unapokwenda kufanya kazi hiyo ni vizuri kuzingatia kanuni na taratibu za nchi," alisema Bayo.

Alisema matarajio yao baada ya kumaliza mkutano huo, watakuja na msimamo wa pamoja utakaowawezesha kushirikiana kati ya mashirika, taasisi hizo na serikali. Waliiomba serikali kuondoa baadhi ya kanuni na sheria mpya ambazo zimeonekana kuwa kikwazo kwa mashirika na taasisi hizo, wakati wa usajili.

Blandina Nkini ambaye ni Mratibu wa Mashirika na Taasisi Binafsi Mkoa wa Arusha, alisema endapo taasisi na mashirika hayo watatunganisha nguvu na serikali wataweka mpango mkakati wa kutoa huduma kwa kiwango kikubwa kwa jamii.

Alisema baadhi ya mashirika hayo, yamekuwa yakilalamika kuwa serikali imekuwa ikiwaminya upande wa utendaji kazi wao. "Serikali haiwaminyi hata kidogo ninacho fahamu mimi wameshindwa kuelewa baadhi ya tafsiri na ufafanuzi wa sheria hivyo wanapaswa kuzielewa na kuzingatia miongozo hiyo," alisema Nkini.

Pia alisema baadhi ya mashirika yamekuwa siyo waaminifu ndio maana serikali imeyaweka kwenye wizara moja ili iweze kuyafuatilia na kufanya tathmini ya utendaji kazi wao.

"Hapo mwanzo mashirika haya yalikuwa yamesajiliwa katika wizara mbalimbali hivyo, walikuwa wakitumia mwanya huo kufanya mambo kinyume cha sheria," alisema.

## Takukuru yaonya kubebana uchaguzi

**Na Jaliwason Jasson**, MANYARA

TAASISI ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (Takukuru) mkoani Manyara imewaonya watendaji wa umma kuacha kubebana wakati wa kutoa huduma na katika uchaguzi wa serikali za mitaa ili wananchi wapate viongozi sahihi.

Hayo yalisemwa jana mjini hapa na Naibu Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Isdory Kyando, wakati akitoa taarifa ya utendaji ya taasisi hiyo kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, mwaka huu, kwa waandishi wa habari.

"Viongozi wa serikali waache kubebana maana kubebana kumepitwa na wakati na wale viongozi wanaofumbiana macho wanasababisha huduma kuzorota," alisema Kyando.

Aliwataka viongozi msimu huu wa uchaguzi wa serikali za mitaa wasikubali kununuliwa ili waweze kupatikana viongozi bora watakaosimamia haki za wanyonge.

Kyando alisema kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa, taasisi hiyo imepokea malalamiko 134 kutoka kwa wananchi na kati ya hayo, 96 yalihusiana na makosa ya rushwa na 38 hayakuhusiana na tuhuma za rushwa.

Alisema serikali za mitaa, yaani ofisi za vijiji na kata ndio zimeongoza kwa kulalamikiwa kwa kuwa na malalamiko 40, watu binafsi (15), mabaraza ya kata (13), idara ya afya (11) idara ya elimu (10), viongozi wa kisiasa (8), halmashauri za miji na wilaya (6) na NSSF (3).

Alisema taasisi yake inafanya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ambayo ina thamani ya Sh. bilioni 30 na miongoni mwa miradi hiyo ni wa maji Tumati, Sh. bilioni 1.1, ujenzi wa makao makuu ya Halmashauri ya Mbulu Sh. bilioni 4.7, ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Simanjiro, Sh. bilioni 1.6 na zaidi ya Sh. milioni 400 za ruzuku katika shule za msingi.

Pia aliomba wananchi kuwafichua matapeli ambao wanaongezeka kwa kuwapigia watu simu na kujitambulisha kuwa wao ni maofisa wa Takukuru na kuwataka wananchi wawaripoti ofisi za taasisi hiyo ili kukomesha tabia hiyo.



Balozi wa Uingereza nchini Tanzania, Sarah Cooke, akizindua kisima cha Sh. milioni 25, kilichojengwa na Shirika la HakiElimu kwa ufadhili wa Serikali ya Uingereza kwenye Shule ya Sekondari Mukulati wilayani Arumeru. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

## Uingereza yafadhili wanafunzi kisima cha majisafi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANAFUNZI zaidi ya 800 wa Shule ya Sekondari Mukulati, wilayani Arumeru wameondokana na changamoto ya kutembea umbali wa kilomita nane kutafuta maji baada ya Shirika la HakiElimu kuwakabidhi kisima cha majisafi walichojenga kwa Sh. milioni 25 shuleni hapo.

Akikabidhi kisima hicho jana mbele ya Balozi wa Uingereza nchini, Sarah Cooke, kwa uongozi wa shule hiyo, Mkurugenzi wa Shirika la HakiElimu Tanzania Dk. John Kalage, alisema kisima hicho kimejengwa kwa ufadhili wa nchi ya Uingereza kupitia ubalozi huo nchini.

Alisema kati ya fedha hizo HakiElimu wametoa Sh. milioni 20 na wananchi Sh. milioni tano na kufanikisha uondoaji changamoto ya ukosefu wa majisafi shuleni hapo.

Dk. Kalage alisema lengo la kuwafadhili maji hayo ili kuondoa adha ya kutafuta maji umbali mrefu hasa wanafunzi wa kike ambao walijikuta wanafanya vibaya katika masomo sababu ya changamoto hiyo.

"Wanafunzi hawa wa kike wapo 84 ambao wanalala bweni, lakini tangu wajengewe kisima hiki wameondokana na adha hii na kujikuta wakifanya vizuri katika masomo sababu muda waliokuwa wanatumia kufuata maji wanatumia kujisomea na kufanya vizuri kuliko wavulana," alisema.

Alisema ubalozi huo umekuwa msaada mkubwa nchini kupitia shirika hilo kwa kuboresha mazingira ya elimu kwenye shule 127 wanazozifadhili nchini na kuleta mwamko mkubwa wa elimu hasa jamii za wafugaji na pembezoni.

Alisema kwa Mkoa wa Arusha wanasaidia shule nane kati ya 127 zilizopo nchini, sekondari zikiwe nne na msingi nne, lengo likiwa kumkomboa mtoto wa kike katika elimu na kuongeza idadi yao kuanzia shule za msingi na sekondari.

"Tunawekeza zaidi katika elimu kwa mtoto wa kike ionekane ya thamani na kuongeza idadi yao kwa kuwa miaka ya nyuma watoto wa kike shule za msingi na sekondari walikuwa wachache ikilinganishwa na wakiume, lakini tangu tuanze miradi hii ya HakiElimu tumeongeza ufaulu na idadi yao pia," alisema.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari Mukulati, Vitalis Nada, alishukuru ujio wa balozi huyo ambaye alifika kujionea kisima hicho na mazingira ya shule ili kuona fedha wanazotoa zinavyotatua changamoto katika jamii.

"Kweli sisi tumefurahi sana kwa kuwa maji haya yamesaidia watoto wa kike kuongeza ufaulu, lakini sasa wanajiamini kutokana na elimu wanayopatiwa na HakiElimu kupitia klabu tulizonazo shuleni hapa," alisema.



Wauza mkaa wakiwa wamejipumzisha chini ya mti majira ya mchana katika eneo la Kata ya Tinde, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini jana, wakiwa safarini kupeleka bidhaa hiyo, Shinyanga Mjini. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Magereza yaokoa jahazi mradi maji

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

KIKOSI Kazi cha Jeshi la Magereza kimepelekwa katika mradi wa maji wa Munge, Wilaya ya Siha kwa ajili ya kuongeza nguvu ya uchimbaji wa miundombinu ya maji na ufukiaji wa mitaro.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya Kampuni ya Mbesso Construction Ltd kushindwa kukamilisha mradi huo kwa wakati.

Jana, Kaimu Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini (Ruwasa) Wilaya ya Siha, Mhandisi Joyce Bahati, aliieleza Nipashe kuwa uamuzi huo ulifikiwa na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo.

"Ni kweli kamati ilipendekeza kwamba Magereza ipewe kazi hiyo ya uchimbaji na ufukiaji wa mitaro, lakini tunavyoongea hivi sasa tayari mkandarasi huyo amejenga tangi la maji pamoja na vilula sita. Mradi huo ukikamilika tunatarajia uwanufaishe zaidi ya wananchi 3,000 wa Kijiji cha Munge."

Kwa mujibu wa mhandisi huyo, mradi huo una ukubwa wa umbali wa kilometa 18 unaigharimu serikali Sh. milioni 750.

Mradi huo ulianza kujengwa Oktoba 15, mwaka jana, na ulitakiwa kukamilika Septemba 15, mwaka huu lakini umesongezwa mbele baada ya mkandarasi huyo kusuasua katika uchimbaji wa mitaro.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, alisema wamefikia uamuzi huo kwa vile wanaamini kwamba kukamilika kwa mradi huo kutawapunguzia kero hasa wananchi wa jamii ya wafugaji ambao husafiri umbali mrefu kufuata maji kwa kutumia punda.

Agosti, mwaka huu, Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, aliagiza kukamatwa na kuwekwa mahabusu Mkurugenzi wa Kampuni hiyo kutokana na kutoa maelezo ya uongo juu ya mradi wa maji unaoteklezwa katika Kijiji cha Munge, Kata ya Donyomoruwa.

# Waungana kupambana na ukatili wa kijinsia

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KATA 28 za Mkoa wa Kilimanjaro zinazokabiliwa na changamoto kubwa ya matukio ya ukatili wa kijinsia, kukosekana kwa usawa wa kijinsia, uminywaji wa haki za binadamu na uongozi wa kitabaka, zimeanza kutengeneza nguvu ya pamoja ya kutetea wanawake kupambana na ukatili huo.

Akitoa taarifa jana kwa Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Kilimanjaro, Hilda Lauwo, Mratibu wa mradi wa ujenzi wa nguvu ya pamoja kutetea wanawake na watoto na kupambana na ukatili wa kijinsia mkoani humo, Veronica Ollomi, alisema walengwa watakaofikiwa wako katika halmashauri saba.

Mradi huo wa majaribio wa mwaka mmoja, unatekelezwa na Shirika la kiraia la Kwieco, kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania (WFT). Maeneo yaliyolengwa ni Halmashauri za Wilaya ya Moshi na Manispaa ya Moshi, Siha, Rombo, Mwanga, Same na Hai.

"Ujio wa mradi huu ni chachu kwa wanawake kwa sababu tunalenga kujenga uelewa na uwezo juu wa masuala ya usawa wa kijinsia, haki za binadamu na uwezeshaji wa wanawake na wasichana kwenye jamii ili kuongeza ujuzi wa kupambana na ukatili wa kijinsia na ukiukwaji wa haki za binadamu kwenye jamii.

"Lakini mradi huu unakwenda kuimarisha na kusimamia majukwaa na mitandao ya wanawake ambayo tayari yameshaundwa ndani ya mkoa ili kuendelea kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia kwa ajili ya kuhamasisha haki za binadamu, usawa wa kijinsia, uongozi na kujengea uwezo wanawake na wasichana," alisema Ollomi.

Alisema shughuli zitakazotekelezwa ni kufanya mafunzo kuhusu jinsia, msaada wa kisheria, uongozi, demokrasia na misingi ya utawala bora kwa wanawake, wanaume, viongozi wa serikali, viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa dini na viongozi wa jadi.

Mratibu huyo alisema meelezo bayana kwamba lengo la kuja na nguvu ya pamoja ni kusaidia vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwenye jamii kupambana na ubaguzi wa kijinsia na kushiriki kwenye uchaguzi ujao wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji utakaofanyika Novemba 24, mwaka huu.

Akiwasilisha mada kuhusu dhana ya uongozi, mwezeshaji wa mradi huo, Peter Mashingia, alisema yako mabadiliko ya muda mfupi yatakayojitokeza kama vile kuongezeka kwa idadi ya wasichana, wanawake na vijana viongozi kama mawakala wa mabadiliko katika jamii na kuongezeka kwa uelewa wa masuala ya jinsia na ukombozi wa wanawake kimapinduzi kwa jamii.

Pia alisema katika mabadiliko ya muda mrefu, wasichana watajengewa uwezo wa kuwa na sauti na ujasiri wa kusimama kuzungumzia haki zao.

Kata zenye changamoto na ambazo zitanufaika na mradi huo ni Njoro, Shirimatunda, Pasua, Bomambuzi na Kiboriloni (Manispaa ya Moshi), Kibosho Magharibi, Old Moshi Magharibi, Kirua Vunjo Kusini na Mwika Kaskazini (Moshi).

Zingine ni Kirua, Sanya Juu, Biririi na Gararagua (Siha), Ubetu Kahe, Mraokeryo na Nanjara (Rombo), Mwanga Mjini, Mgagao, Lembeni na Kighare (Mwanga), Kisima, Stesheni, Same na Ruvu (Same) na Mnadani, Machame Mashariki, Bomang'ombe na Kia (Hai).

# Mwanamke auawa kwa kukanyagwa na tembo

**Na Godfrey Mushi,** MWANGA

SIKU chache baada ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (Tawiri), kuanza kuwadhibiti tembo wanaovamia mara kwa mara makazi ya watu na kuharibu mazao mkoani Kilimanjaro, tembo mmoja anadaiwa kusababisha kifo cha mkazi wa Kijiji cha Ngulu, wilayani Mwanga.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Modest Mvungi, alisema jana kuwa aliyepoteza maisha kutokana na kujeruhiwa kwa kukanyagwa na tembo kwenye maeneo mbalimbali ya mwili ni Majabu Lemahuna.

Lemahuna wakati anavamiwa na tembo na kuuawa, alikuwa akichukua kuni za kupikia nje ya nyumba yake.

"Huyo mwanamke aliyeuawa na tembo alivunjwa miguu, mikono na kusababisha kupoteza fahamu majira ya saa 2:20 asubuhi," alisema.

Baadhi ya majirani waliodai kushuhudia tukio hilo, akiwamo Asia Shana, walisema kuwa mwanamke huyo wakati anatoaka nje na kisha kujeruhiwa hadi kufikwa na mauti, hakujua kuwa tembo hao wako karibu na nyumba yake.

Kutokana na tukio hilo, Mvungi ameiomba Wizara ya Maliasili na Utalii kuwaondoa tembo hao ili kunusuru maisha ya wananchi wa kijiji cha Ngulu.

Wiki mbili zilizopita, Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alisema Mkuu wa Wilaya jirani na Mwanga alitoa taarifa ya kupokea timu ya wataalamu wa Tawiri kutoka Kanda ya Kaskazini iliyoongozwa na Dk. Edward Kohi.

Baadhi ya wananchi wa Kata ya Vumari, waliieleza timu hiyo kuwa kuna wimbi kubwa la makundi makubwa ya wanyama kuingia na kuvamia maeneo ya makazi na mashamba ya wananchi kila wakati.

Tembo hao wanadaiwa kuingia kwa makundi na kuvamia mashamba, nyumba na maghala ya akiba za vyakula vya aina mbalimbali hasa nafaka kama mahindi, mtama na viazi vitamu.

Mazao mengine yanayovamiwa mashambani au bustanini ni miwa, maboga, matikiti maji, matango na bustani zilizoko kandokando ya mito.



Ukurasa 20

Biashara mahindi ya kuchoma, vipi msimu mvua, mawingu tu?



Ukurasa 14

Walikoogelea, kuvuka kwa mitumbwi miaka 21, daraja lawabadilishia maisha



Ukurasa 19

Mwalimu aliyeushika ujasiriamali bila ya kutelekeza chaki darasani

BUFE

Ijumaa Oktoba 11, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



# Benki Dunia: Tasaf 'imetukosha' tunaipa Sh. trilioni 1 roho nyeupe

**Na Elizabeth Zaya**

TANZANIA imo katika nchi zilizofanikiwa kutekeleza kwa kishindo Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii(Tasaf), kauli inayothibitishwa na Benki ya Dunia (WB), mdau anayeunga mkono mpango huo.

Wiki hii Benki hiyo imetoa mkopo wa masharti nafuu wa Sh. trilioni 1.035 kwa serikali ya Tanzania kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa kipindi cha pili cha Awamu ya Tatu ya Tasaf.

Mkurugenzi Mkazi wa WB, Bella Bird, anasema benki hiyo ilipitisha wazo la kuwezesha mpango huo wa pili kwa kishindo, baada ya kuona mafanikio makubwa awamu inayomalizika.

"Nilipo 'present paper' (kuwasilisha andiko) ya mpango huu kwa Benki ya Dunia, ulipitishwa kwa kishindo na hii imetokana na kazi kubwa ambayo imefanywa na serikali ya Tanzania katika kutekeleza miradi yake,"anasema Bella Bird.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

**Habari katika picha**



Ukurasa 17

**Tabianchi yageuza kilimo mahindi janga kwa washika jembe Korogwe** Ukurasa 18

UCHUMI

# Walikoogelea, kuvuka kwa mitu
# miaka 21, daraja lawabadilishia

• Biashara sasa ni bodaboda • Bei viwanja juu, shule zajaa • Kijiji mpakan



Picha mbili, zinazoonyesha tofauti ya uvushaji kabla ya kuwa na daraja kwa miaka 21 na baada ya kujengwa daraja jipya. **PICHA: YASMINE PROTACE**

**Yasmine Protace,** Mkuranga

WENGI wanakikumbuka vyema kijiji ambacho msimu wa mvua kama ilivyo sasa ni sharti kuvuka kwa kuogelea na kinababa na kinamama wanavua nguo zao.

Kwa bahati mbaya, mfumo wa mahitaji kama ya bidhaa hata elimu inaegemea nga'mbo ya pili ya kijiji, ambako ni Dar es Salaam, wakati kijiji hicho kinachoitwa Mlamleni, kiko katika Wilaya ya Mkuranga Mkoa wa Pwani.

Kijiji hicho kilisahaulika kwa takribani miaka 21, kwa kukosa daraja la kuinusuru na kero yenye sura ya janga, hata kuwafanya watumie mitumbwi ya asili kuvuka kwenda upande mwingine, pale mvua zinaponyesha sasa.

Nayo si huduma ya bure, kuna tozo kubwa kwa wakazi hao masikini. Leo hii ni simulizi ya mafanikio wakiwa na daraja linaloshika sura ya mkombozi kwa wakazi wa kata hiyo

Kutokana na kijiji hicho kutokuwa na daraja na kuwafanya watu kuvushwa kwa mitumbwi ya asili, kipindi ambacho mvua inanyesha na baadhi ya wakazi waliogelea kutoka kijiji hicho hadi jijini Dar es Salaam.

Mitumbwi isiyo salama, ilifikisha hatua wanafunzi wanaosoma

> **Watoto wake hawakwenda shule kwa kuhofia vivuko kutokuwa salama na sasa ombi lake serikali iwajengee zahanati, kituo cha polisi na kuongeza shule.**



# mbwi maisha

## i Dar, Mkuranga





ng'ambo ya Dar es Salaam, kuisitisha safari ya shule.

### MWENYEKITI KIJIJI

Mwenyekiti wa Kijiji hicho kilichoanzishwa mwaka 1977, Amir Mbambar, anasema ni hali iliyosababisha wananchi kuingiwa woga, pale walipovushwa.

Anakumbuka mvua za elnino zilizonyesha mwaka 1998, zilisababisha kuharibika daraja lililokuwa kiungo cha Tambani na Mbande, jijini Dar es Salaam. Tangu hapo mvua ilisababisha usumbufu mkubwa, hasa katika kipindi cha mvua.

"Baada ya mvua kubwa za 'elnino' kunyesha kulisomba daraja, hali hiyo inaleta shida kwa wanakijiji pale mvua zinaponyesha palipokuwa na daraja kujaa maji na kusababisha wanakijiji kutumia mitumbwi ya asili kuvushwa au kuogelea kwa watu wasio na uwezo," anasema.

Anaongeza watu walivushwa na mtumbwi kwa nauli ya Sh. 500 na wanafunzi Sh.200 na wale wasio na fedha walilazimika kuogelea hadi upande wa pili.

Mwenyekiti huyo anasema, mbali na kutumia usafiri wa mitumbwi ya asili au kuogelea, wapo baadhi walitumia usafiri wa bodaboda kutoka tambani hadi Chamazi kwa kulipa nauli ya Sh.7000, kupitia njia ya Msongola.

Azungumzia daraja, akisema ujenzi umekamilika baada ya kuanza kazi mwaka jana, akitamba sasa kuna neema ya kuwapo magari kutoka kijijini Tambani hadi Kariakoo, nauli yake ni Sh. 700.

Mbambar, anasema ongezeko la watu linazidi kuongezeka. Wakati awali idadi ya kaya ilikuwa 3000 sasa imefika 4000, kukiwapo jumla ya wakazi zaidi ya 10,000.

Mwenyekiti Mbambar, anasema awali bei ya viwanja kijijini ilikuwa Sh. milioni 1.5, sasa imepanda hadi Sh. milioni 2.5.

Sambamba na hilo, anazungumzia umeme kwamba sasa upo katika vitongoji viwili kati ya vitano vilivyopo.

### CHANGAMOTO

Anasema kuna haja ya kuangaliwa miundombinu inayotakiwa kuboreshwa kutoka Mbande hadi Tambani na kijiji hakina zahanati bado inajegwa, hali inayowafanya wakazi kufuata huduma hizo jirani, jijini Dar es Salaam.

Anataja mradi wa shule ya msingi kwamba wamefanikiwa kujenga vyumba vya madara saba, lakini shule hiyo darasa moja linatumiwa na watoto zaidi ya 200 kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi walioko.

### WANAKIJIJI

Jamila Juma, mkazi wa Tambani anasema kukamilika daraja hilo kumezaa matunda wakisahau maisha ya kuogelea kwenda mna kurudi kazini,

"Hili daraja lilichukuliwa na maji, halikutengenezwa. Mvua ziliponyesha tunalazimika kupanda mitumbwi ya asili alafu unalipa kiasi cha 500,"anasema.

Shaban Ally, ni dereva wa bodaboda anayesema kipindi ambacho mvua zinanyesha wamekuwa wakipakia wateja kwa kuwatoza zaidi ya Sh. 2000, kwa kuwatoa Mbande stendi hadi Tambani katika kivuko.

Anasema, katika msimu wa mvua na pasipokuwapo mvua, zamani walifanya biashara ya kuwavisha abiria, kuwatoa upande mmoja hadi mwingine.

Ally anasema, biashara hiyo sasa imekuwa ngumu kutokana na wanakijiji kutumia zaidi bodaboda bila ya kikwazo.

Hamida Jumanne, mkazi wa Tambani, ni mchuuzi wa mboga, anasema changamoto ya kutokuwapo daraja, kuliwafanya baadhi ya wafanyabiashara wasio na uwezo kuogelea kwenda upande wa pili.

Anasema: "Kuvushwa na mitumbwi ya asili unalipa Sh. 500 kwa kwenda na kurudi. Sasa mtaji wa biashara ni mdogo tunalazimika kuogelea.'Anaongeza, daraja limesaidia kuwarahisishia hata wasipopanda daladala wanapita darajani kwa kipindi cha mvua na hata pasipokuwa na mvua.

Aweza Moshi, mkazi wa Tambani, anasema kuwapo daraja kumewasaidia watoto kuhudhuria masomo kipindi cha mvua na pasipo mvua.

Anasema, watoto wake hawakwenda shule kwa kuhofia vivuko kutokuwa salama na sasa ombi lake serikali iwajengee zahanati, kituo cha polisi na kuongeza shule.

Mkazi mwingine, Amina Fodi, anasema mvua ziliponyesha, suala la kuogelea kuliwafanya baadhi ya wanawake na wanaume kupata fangasi kutokana na kuyakanyaga maji kila mara walipotoka Tambani na kwenda na Dar es Salaam.

James Gayo, ni mwanafunzi wa shule ya Msingi Chamazi anayekiri daraja limewasaidia sana kufika shule siku zote katika kipindi ambacho mvua ikinyesha, kwani awali walishindwa kwenda shule kwa sababu ya kuhofia mitumbwi ya asili haikuwa salama.

### MVUSHAJI MTONI

Hamadi Jabir, ni mmoja wa walioajiriwa kuvusha watu, anasema kwa siku walilipwa Sh. 7,000 kwa ajili ya uvushaji, katika biashara iliyoingiza faida wastani wa Sh.30,000.

Anataja changamoto walizopata ni kukanyaga maji na kupata magonjwa ya fangazi, huku katika uchumi wa sasa anasema biashara kwao ndio imeisha baada ya kujengwa.

### WAZIRI ULEGA

Mbunge wa Mkuranga, Abdallah Ulega, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Mifugo, anasema baada ya kumalizika ujenzi kwa daraja, umewafungua wakazi wa Mkuranga na Chamazi kulitumia daraja hilo.

Anasema ni utekelezaji wa ahadi ya Rais Dk. John Magufuli, aliyehidi kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha daraja hilo.

Ulega anasema, zimetumika zaidi ya Sh. milioni 50 na hivyo, wakazi wana wajibu wa kulitunza daraja lidumu.

# Msuguano kampuni za simu, China, Marekani



Marais, Xi Jinping wa China na Donald Trump wa Marekani. **PICHA: MTANDAO.**



Simu aina ya Apple. **PICHA: MTANDAO.**

**Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Biashara wa Marekani, Wilbur Ross, ameshambulia utendaji wa China katika biashara na kusifu uhusiano wa kiuchumi kati ya Marekani na Australia.

Anasema hayo, huku kukiwapo vita vya biashara vikiendelea kati yake na China.

Ross aliuambia mkutano wa biashara mjini Sydney, Auzstralia kuwa Rais Donald Trump, hakutaka kutumia ushuru kuilazimisha China kubadili utendaji wake, lakini anahisi ilikuwa muhimu.

Matamshi hayo yanakuja wakati maofisa wa Marekani na China wanajitayarisha kurejea katika mazungumzo ya biashara mjini Washington.

Uamuzi wa Rais Trump mwaka jana kuweka ushuru dhidi ya bidhaa za China, umetikisa masoko ya dunia na kuongeza hali ya wasiwasi kuhusiana na mwelekeo wa uchumi wa dunia hivi sasa na baadaye .

Pia, katika hatua tofauti, kampuni ya simu za mkononi ya Apple imeondoa katika simu zake 'app' ambayo inasaidia wanaharakati wa Hong Kong kufahamu walipo polisi, kutoka katika mauzo yake ya mtandaoni, baada ya gazeti la serikali ya China kuishutumu kampuni hiyo kusaidia tabia zilizo kinyume na sheria.

Kampuni hiyo ya Apple hivi karibuni imepata shinikizo la kuwa upande wa serikali ya China dhidi ya waandamanaji wanaopinga serikali, wakati gazeti la chama cha kikomunisti la Peoples Daily, kinasema jana kuwa app hiyo inasaidia vitendo kinyume na sheria.

Gazeti hilo liliuliza iwapo kampuni ya Apple inasaidia 'wahuni' wa Hong Kong. Wanaharakati wa Hong Kong wanalalamika kwamba viongozi wa China na Hong Kong wanamomonyoa utawala wa mji huo na haki za raia zilizoahidiwa na mkoloni wa zamani Uingereza. **DW**

UCHUMI

# Benki Dunia: Tasaf 'imetukosha' tunaipa Sh. trilioni 1 roho nyeupe

## • Bosi: Wageni foleni kwetu kujifunza • Januari mapya ikiwamo mtaji wake



Mkurugenzi Mtendaj wa Tasaf, Ladislaus Mwamanga,(aliyevalia suti jeusi)akiwa na wajumbe wa Kamati ya Utendaji wa Tasaf, wakiangalia nyaraka na Dk, Dorothy Gwajima…. katika ziara zao za kutembelea kaya masikini. **PICHA ZOTE: ELIZABETH ZAYA**

**INATOKA UK.13**

Anasema, katika kutathmini utekelezaji mpango wa kwanza wa Tasaf unaomalizika, walitumia mkaguzi ambaye hafungamani na upande wowote kufanya kazi hiyo.

### BOSI TASAF

Mkurugenzi Mtendaji wa Tasaf, Ladslaus Mwamanga, anasema mafanikio hayo yamevutia wageni kutoka nchi mbalimbali wanaofika kujifunza kwao, akitaja baadhi ni kutoka Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Nigeria.

Mwamanga anataja siri za Tasaf kufanikiwa ni pamoja mifumo mizuri iliyopo ya utekelezaji, ikiwamo ushirikishwaji wa jamii.

Siri nyingine anataja ni kufanya malipo kwa walengwa kwa wakati, kufanyika tathmini ya kila mara na ufuatiliaji wa karibu maeneo kunapotekelezwa mpango anaongeza: " Serikali nayo imechangia kufanikiwa kwake."

Mwamanga ansema, katika kipindi cha kwanza cha mpango kitakamilika mwishoni mwa mwaka huu na kuanza kwa kipindi kingine

> **"Dhumuni la mpango katika kipindi cha pili ni kuwezesha kaya masikini kutumia fursa ya kujiongezea kipato kupitia miradi mbalimbali inayoendeshwa na Tasaf.**



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Dotto James na Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia, Bella Bird, wakitia saini mkopo kwa Tanzania wiki hii kwa ajili ya Awamu ya Tatu ya Tasaf. **PICHA: MTANDAO.**

cha pili cha utekelezaji wa mpango huo hadi mwaka 2023.

Kwa mujibu wa Mwamanga, taratibu zote za kuanza kipindi cha pili zimeshakamilika, ikiwamo kuandaa miongozo iliyozinduliwa baada ya wajumbe wa Kamati ya Utendaji wa Tasaf kuteuliwa na Rais Dk. John Magufuli.

Ni kamati itakayosimamia mipango yote kwa kutoa maelekezo, kusimamiwa kwa karibu yote yaliyoagizwa na serikali.

Mwamanga anasema kwa sababu azma ya serikali ni kusaidia wananchi wake, katika kipindi hicho cha pili cha mpango, mbali na mkopo kutoka WB, imetenga fedha kutoka vyanzo vyake vya ndani.

Anasema madhumuni ya mpango wa pili, ni kuwezesha kaya masikini kutumia fursa za kuongeza kipato na huduma za kijamii na kiuchumi, kuwekeza katika kuendeleza watoto wao.

"Utekelezaji wa mpango utahusisha miradi ya kutoa ajira ya muda kwa kaya za walengwa wenye uhitaji, ili kujikimu na kuanzisha miradi ya kuongeza kipato na kujikita katika uzalishaji," anasema.

Mwamanga anasema, kuweka akiba na kuanzisha miradi ya ujasiliamali vitapewa kipaumbele katika kipindi hicho kuhakikisha kaya zinazoishi katika hali hiyo, zinapata stadi za elimu ya utunzaji fedha na hatimaye kupata fursa ya kukopa katika taasisi za fedha, kukuza uchumi wa kaya zao.

Anaeleza imani yake kwamba itasaidia kuboresha maisha ya watoto wanaohudhuria kliniki na walioko shuleni na wanaoishi katika mazingira magumu.

"Mpango sasa uko tayari kuanza utekelezaji wake, utatanguliwa na elimu kwa jamii kuhusu taratibu za mpango na baadae utambuzi wa kaya zinazostahili kufikiwa katika vijiji, mitaa nchini," anasema na kuongeza: "Utatekelezwa katika halmashauri zote 187 nchini, Bara na Zanzibar."

### UTEKELEZAJI ULIVYO

Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Shaaban Seif Mohamed, anasema mpango huo umesaidia sana kwa upande wa Zanzibar na miradi mbalimbali iliyoibuliwa na wananchi imetekelezwa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dotto James, anasema awamu hiyo ya pili italenga utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya kutoa ajira za muda kwa kaya masikini, ikiwamo ujenzi wa shule, zahanati, barabara za kijamii na uchimbaji mabwawa ya maji.

"Fedha hizi pamoja na kwamba zitaenda kuzisaidia kaya masikini ambao ni wazee wasiojiweza kufanya kazi na wengine wanaofanana na hao, pia kundi jingine litakalonufaika ni kaya masikini ambazo hazina uwezo, zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi," anasema na kuongeza:

"Hawa watashiriki katika shughuli za kijamii hususani ujenzi wa madarasa, shule za msingi na sekondari, ujenzi wa vituo vya afya, zahanati ikiwamo barabara za kijamii miradi ya maji hususani kuchimba mabwawa ya maji.

"Kwa hiyo baada ya kufanya kazi hizo watakuwa wanapewa ujira. Tumepata uzoefu kwa wenzetu wa Ethiopia wanafanya hivyo na wamefanikiwa sana,"

Pia, anasema ni kuziwezesha kaya kuongeza rasilimali za lishe, kujihusisha zaidi na kazi za uzalishaji, kukuza uchumi wa eneo unapofanyika utekelezaji na kuendeleza watoto kwa kuwekeza katika lishe na shuleni.

Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji ya Tasaf, Dk. Moses Kusiluka, amempongeza Rais John Magufuli kwa jitihada za kupambana kuwakomboa wanyonge na kukubali mkopo huo kwa ajili ya kusaidia kutokomeza umasikini nchini.

Akizungumza baada ya kusaini mkataba huo, Katibu Mkuu Wiraza ya Fedha na Mipango, Doto James, alisema katika awamu ya pili mpango huo umelenga zaidi katika kuimarisha miundombinu ya shule, afya na maji.

Alisema dhumuni la mpango katika kipindi cha pili ni kuwezesha kaya masikini kutumia fursa ya kujiongezea kipato kupitia miradi mbalimbali inayoendeshwa na Tasaf.

Alisema awamu hiyo ya pili ya mpango italenga zaidi katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya kutoa ajira za muda kwa kaya masikini ikiwamo ujenzi wa shule, zahanati, barabara za kijamii na uchimbaji wa mabwawa ya maji.

Fedha hizi pamoja na kwamba zitaenda kuzisaidia kaya masikini ambao ni wazee wasiojiweza kufanya kazi na wengine wanaofanana na hao, lakini pia kundi jingine litakalonufaika ni kaya masikini ambazo hazina uwezo, zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi,"alisema na kuongeza:

"Hawa watashiriki katika shughuli za kijamii hususani ujenzi wa madarasa, shule za msingi na sekondari, ujenzi wa vituo vya afya, Zahanati ikiwamo barabara za kijamii miradi ya maji hususani kuchimba mabwawa ya maji, kwa hiyo baada ya kufanya kazi hizo watakuwa wanapewa ujira. Tumepata uzoefu kwa wenzetu wa Ethiopia wanafanya hivyo na wamefanikiwa sana,"alisema.

Alisema serikali ya awamu ya tano imekubali kuendelea na mpango huo ili kupata matokeo mazuri zaidi ya kupunguza umasikini nchini kwa kuongeza uchumi wa kaya kupitia uzalishaji wa kipato.

Pia alisema ni kuziwezesha kaya hizo kuongeza rasilimali za lishe, kujihusisha zaidi na kazi za uzalishaji, kukuza uchumi wa eneo unapofanyika utekelezaji na kuendeleza watoto kwa kuwekeza katika lishe na shuleni.

Alisema mpango huo unatarajiwa kufika mwaka 2023, na kwamba umeongeza nguvu katika juhudi za serikali za kupunguza umasikini wa kipato kwa wananchi wake.

# Biashara katika picha



Meneja Mkuu wa Masoko wa kampuni ya Azania Group, Joel Laiser, akizungumza na wageni waalikwa na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa bidhaa zao mpya za sabuni za unga za King Limau na Marhaba, jijini Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**



Meneja Uendeshaji wa Benki ya NBC Tawi la Morogoro, Joceline Msuya (wa tatu kulia), akishikana mikono na Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro, Dk. Francis Semwene, wakati akimkabidhi msaada wa Madawa yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 9, mjini Morogoro juzi, kwaajili ya kusaidia hospitali hiyo na nyingine zenye uhitaji vilivyotolewa na benki hiyo. **NA MPIGAPICHA WETU**



Mfanyakazi wa benki ya NBC, Singida, Rachel John, akizungumza na mkulima na mtengenezaji wa mvinyo wa zabibu, Wendece Hombolo alipotembelea banda la benki hiyo, katika maonesho ya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), yaliyofanyika mkoani humo mapema wiki hii. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

UCHUMI

# Tabianchi Korogwe imegeuza kilimo mahindi janga kwa washika jembe

• Asilimia tisa tu ndio walioambulia • Bei yapaa debe Sh. 5000 hadi 9000 • DED: Mlime mihogo; miaka 4 vilevile

**Na Jenifer Julius**, KOROGWE



Hivi ndivyo hali ya mahindi ilivyokuwa Juni mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

WAKATI jua linaanza kuchomoza kuelekea Magharibi, Gerephasi Kaojo (45) tayari yupo Lujela, eneo maalum kwa ajili ya kilimo cha mahindi. Ilimchukua dakika 45 'kukata' mwendo wa takribani kilometa moja na nusu alifika eneo hilo.

Ikiwa ni siku yake ya mwisho ya kuvuna, hakuamini anachokipata kutoka katika ekari tatu za shamba alizolima. Anasogea hatua tatu nyuma ili aone vizuri na kujiridhisha kabisa kuwa ni 'guta' moja tu sawa na gunia mbili za mahindi kweli?

Hapo kijasho chembamba kinamtoka na macho yaliyobadilika rangi kuwa ya njano, analazimika kugeuka huku na kule akitafuta ushahidi katika mashamba ya jirani zake na mara moja anapata jibu, hakuna tofauti.

Ikiwa ni mwaka wa nne sasa tangu aachane na kilimo cha mahindi cha biashara na kujikita kulima kwa ajili ya chakula, Gerephasi anazidi kukatishwa tamaa na mdororo wa mavuno unaoongezeka mwaka hadi mwaka.

Wakati akiendelea na shughuli ya mavuno ya mahindi katika shamba lake, Gerepasi anamweleza mwandishi wa makala hii aliyekwenda kutembelea mashamba hayo, kwamba kukosekana kwa mvua za kutosha, ndio chanzo cha msiba alionao.

Mara ya mwisho kupata mavuno mazuri ilikuwa mwaka 2014, alipolima ekari tatu na kupata magunia 20, huku hali ikiwa mbaya kadiri miaka inavyosogea. Mwaka huu katika ekari tatu alizolima ameambulia gunia mbili tu.


Gerephasi sio peke yake anayelia na kadhia ya mavuno kidogo katika kijiji cha Kilole, kilichopo katika Kata ya Kwangumi, ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, mkoani Tanga.

Mkulima mwingine ni Devota Marach, mama wa watoto watatu, anayesema amekataa kuendelea na kilimo cha mahindi, baada ya kuingia hasara kwa kurudia kulima na kuambulia patupu.

"Tulipanda mwezi wa Pili (Februari) kama kawaida ya kilimo cha mahindi, mvua zikanyesha kidogo mbegu zikaoza, tukalazimika kurudia tena kupanda mwezi wa Tano (Mei) mvua ikanyesha kubwa kupitiliza, matokeo yake haya sijapata kitu. Sasa siwezi kurudia tena hii hasara, bora nifanye kitu kingine," analalmika Devotha.

Tofauti na waliorudia kupanda mara mbili, wapo waliokata tamaa ya kurudia kupanda mbegu zilivyooza mara ya kwanza, kutokana na kukosa pesa za kununua mbegu na kuandaa mashamba kama anavyoelezea Modesta Semkiwa.

> "Naishauri serikali isambaze maji katika mashamba ya mahindi kwa kutumia skimu ya umwagiliaji, kama ilivyofanya kwenye mashamba ya mpunga kwa kuwa maji yapo ya kutosha kwenye Mto Ruvu.




"Nilikata tamaa kwa sababu sikuwa na pesa za kurudia kupanda. Kwa sababu hapo ni kama unaanza upya, ulipie kukatua, ununue mbegu, uwezo huo sina kwa kweli, huu mwaka ni wa njaa kwa upande wangu."

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kwangumi, Mathew Msanga, anathibitisha kuwa katika asilimia 85 ya wanakijiji waliolima zao la mahindi mwaka huu, waliovuna japo kidogo ni asilimia tisa tu. Hiyo ina maana asilimia 91 wameambulia patupu.

Kutokana na hali hiyo, walilazimika kuandika ripoti ya hali iliyotokea na maofisa kilimo wa wilaya waliwatembelea kujionea hali ilivyo.

### MABADILIKO TABIANCHI

Ofisa Kilimo wa Kata ya Kwamgumi, Hamisi Mndeme, anaelezea athari za mabadiliko ya tabianchi kuwa chanzo kikuu cha kutopata mavuno, akitoa sababu za mvua kutotabirika.

"Kawaida mvua za kupandia zinanyesha katikati ya mwezi wa Pili (Februari) hadi wa Tatu (Machi), lakini mwaka huu zimenyesha kidogo sana ambazo hazikutosheleza kukuza mahindi," anafafanua.

Hata hivyo, anawashauri wanakijiji wasikate tamaa kwa kilimo, kwani kama ilivyo shughuli yoyote ina faida na hasara zake.

Anasema, mtu anapokosa mwaka huu anaweza kupata mwakani kwa kuwa inajulikana kwamba hali ya hewa ni kitu ambacho hakiwezi kuzuilika.

### CHAKULA BEI JUU

Ingawa, inaelezwa kwamba kukosekana mavuno ya mahindi ya kutosha hakujaathiri hali ya upatikanaji wa chakula, bei ya mazao hasa mahindi imepanda katika kijiji hicho hadi kufikia Sh. 12000 kwa debe moja bei ya jumla, kutoka Sh. 5,000 waliozoea zamani.

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Mji Korogwe, Jumanne Shauri, anasema ametuma timu ya wataalamu wa kilimo katika kijiji hicho kuelimisha wananchi kulima mazao yanayohimili ukame, kama vile mihogo ili kuepuka baa la njaa.

"Chakula kipo cha kutosha, ingawa kimepanda bei, wakati tunatafuta njia mbadala ya kupambana na adha hii ya mavuno," anasema Shauri.

### NINI KIFANYIKE?

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa huo, anashauri kutumiwe teknolojia ya skimu ya umwagiliaji katika mashamba ya mahindi ili wanakijiji waondokane na kilimo cha zamani cha kutegemea mvua ambacho kinaoneakana kufeli.

"Naishauri serikali isambaze maji katika mashamba ya mahindi kwa kutumia skimu ya umwagiliaji, kama ilivyofanya kwenye mashamba ya mpunga kwa kuwa maji yapo ya kutosha kwenye Mto Ruvu.".

Kwa mujibu wa Ripoti ya Majaribio ya Mwaka ya Kilimo na Mifugo kwa mwaka 2016/2017, Mkoa wa Tanga unashika nafasi ya pili kwa eneo kubwa la ulimaji zao la mahindi kitaifa ukiwa na hekta 494,683 sawa na asilimia 8.2, ikiongozwa na Tabora yenye hekta 690,340 sawa na asilimia 11.4 ya hekta za mikoa yote.

Mwezi Agosti mwaka huu, jopo la Watafiti wa Kisayansi wa Athari za mabadiliko ya Tabianchi (IPCC), ilitoa ripoti yake ya tatu kuhusu mwenendo wa athari za mabadiliko ya tabianchi, ijulikanayo kama:

"Ripoti maalum juu ya mabadiliko ya hali ya hewa, jangwa, uharibifu wa ardhi, usimamizi endelevu wa ardhi, usalama wa chakula, na mtiririko wa gesi chafu katika mazingira ya duniani."

Ripoti hiyo ilifafanua kuwa duniani kote, wakulima wadogo wameathirika na mabadiliko ya hali ya hewa ikiwamo kuongezeka kwa joto, kutotabirika mvua, hali inayoathiri utunzaji mazao yao na uzalishaji wa wanyama, hivyo kutishia usalama wa familia zao, mapato na ustawi wa taifa lao.

BIASHARA

# Mwalimu aliyeushika ujasiriamali bila ya kutelekeza chaki darasani

- Amelikamata jembe, uwakala, sheria
- Awaachia neno waajiriwa wanaosusua



Shamba la mwalimu likihudumiwa na wasaidizi wake. Picha ndogo; mwalimu Othiniel Mnkande, akionyesha tikitimaji shambani kwake. **PICHA: SABATAO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

UJASIRIAMALI ni shughuli maarufu inayoshikilia mihangaiko ya watu wengi nchini, wakiwamo wafanyakazi wa taasisi za umma na binafsi kwa kutambua ni vigumu kutegemea mshahara tu kuendesha maisha.

Mbali na kipato, wafanyakazi wanafanya ujasiriamali ili kujizoesha kumiliki fedha na kufanya biashara kuwawezesha kumudu maisha baada ya kustaafu.

Othiniel Mnkande, yumo katika orodha. Ni mwajiriwa aliyeamua kujiingiza katika ujasiriamali, huku akisema kwamba lengo lake ni kujiandaa kwa ajili ya maisha ya baadaye.

Akizungumza na Nipashe wiki hii, Mnkande anasema yeye ni Mwalimu na Meneja wa Shule ya Sekondari Efforts, iliyopo mjini Bagamoyo mkoani Pwani, pia katika sura ya pili ni mjasiriamali.

"Mfanyakazi anatakiwa kuwa mjasiriamali.Vinginevyo akipewa kiinua mgongo anaweza kujikuta kikaisha, maisha yakawa magumu kutokana na ukweli kwamba, hakuwa na uzoefu na ujasiriamali," anasema Mnkande.

Anasema, ni lazima mwajiriwa afanye kazi kwa bidii bila ya mkono wa wizi kwa muda wa mwajiri wake, huku akiendelea na ujasiriamali kama kawaida, akiisistiza: "Vinginevyo asipokuwa makini, anaweza kuharibu kazi." Endelea kufuatilia mzungumzo ya Mwalimu Mnkande na Nipashe:

**SWALI: Ulianza ujasiriamali lini?**

**JIBU:** Nilianza tangu mwaka jana nikiwa na mtaji wa Sh. milioni 10 kwa kununua vyakula mikoani na kuuzia shule nne kwa kutumia vijana wangu wanne ninaosaidiana nao.

Kadri siku zinavyokwenda, ndivyo ninavyojiongeza na sasa nina shamba la ekaro tatu ambazo nimepanda matikiti maji na nimekuwa nikivuna matikiti 2,000 katika kila ekari na kuuzia shule na watu wengine.

Kilimo cha matikiti nilikianza mwanzoni mwa mwaka huu na sasa ninajiandaa kuvuna kwa mara ya tatu, kwani kilimo cha matunda haya huwa kinachukua miezi mitatu tu yanakuwa tayari kuvunwa.

Kimsingi, biashara inakwenda vizuri, ingawa sioni umuhimu wa kutaja kiasi cha fedha ambacho nimeshaingiza tangu nijiingize kwenye ujasiriamali.

Lakini, jambo la msingi ambalo kila mwajiriwa anayeingia kwenye ujasiriamali ni lazima alizingatie, ni kutoiba muda wa mwajiri wake.

Ni muhimu kufanya shughuli zako bila kuingilia muda wa mwajiri. Ukifanya hivyo, maana yake ni kuharibu kazi na mwisho wake ni kufukuzwa.

**SWALI: Unawezaje kufanya ujasiriamali bila ya kuiba muda wa mwajiri wako?**

> **"Kabla ya kufika huko, nilihitimu kidato cha nne mwaka 1998 katika Sekondari ya Chalao iliyopo Same mkoani Kilimanjaro, kisha nikajiunga na Ikizu Sekondari mkoani Mara na kuhitimu mwaka**

**JIBU:** Mbona ni rahisi tu! Kwanza kama nilivyokuambia, nina vijana wangu ninaosaidiana nao katika shughuli zangu za ujasiriamali, pia mimi huwa ninaungana nao siku za mwisho wa wiki.

Ninafanya hivyo, kwa sababu sitaki kuingilia muda wa mwajiri wangu na sehemu zote mbili, kazi zinakwenda kama kawaida. Hivyo, hakuna haja ya mfanyakazi au mtumishi kuogopa kufanya ujasiriamali wa kibiashara akiwa katika ajira.

Mfanyakazi anaweza kuwa mwekezaji huku akiendelea kuvuna gawio pasipo kuiacha ajira, maisha yakaendelea bila tatizo, ili mradi asiibe muda wa mwajiri wake tu.

**SWALI: Hebu fafanua kidogo, ujasiriamali ni nini?**

**JIBU:** Inawezekana jibu langu lisiwe sahihi moja kwa moja, lakini wataalam wa masuala ya uchumi wanasema ujasiriamali ni uwezo wa akili na ubunifu wa mtu kutambua fursa, kuendelea, kuipangia mkakati na hatimaye kuthubutu na kuiweka katika uhalisia.

Vilevile, ujasiriamali waweza kuwa ni kuzalisha bidhaa na mwisho wa siku kuitafutia soko na kuifanya itambulike kwa watumiaji, hivyo ndivyo ilivyo hata katika kilimo na biashara nyingine.

Mimi nilitambua hilo na kulifanyia kazi na sasa ninafanya biashara ya kuuza mazao ya chakula, pia kufanya kilimo cha tikitimaji kwenye shamba langu la ekari tatu lililopo Bagamoyo.

Pia, nina mpango wa kuanzisha kilimo cha mpunga, mahindi na ufugaji wa kuku kwenye shamba langu la ekari saba lililopo Kibaha.

Hatua hii itanifanya niache kununua chakula mikoani kwa ajili ya shule, badala yake nitakuwa ninachokuwa hicho nitakacholima na kuuzia shule. Ninapofikiria biashara huwa ninaangalia ile, ambayo itanifanya niwe mfanyabiashara wa kweli au mwekezaji na kuniunganisha na kuwa mtu aliyejiajiri baada ya kustaafu kazi hapo baadaye.

**SWALI: Mbali na ualimu na ujasiriamali, wewe ni nani katika jamii?**

**JIBU:** Mimi ni mwanasheria, ambaye nilihitimu digirii ya sheria katika Chuo Kikuu cha Bagamoyo mwaka 2016 na nilifanya hivyo ili kupata ujuzi zaidi wa mambo ya sheria.

Kabla ya kufika huko, nilihitimu kidato cha nne mwaka 1998 katika Sekondari ya Chalao iliyopo Same mkoani Kilimanjaro, kisha nikajiunga na Ikizu Sekondari mkoani Mara na kuhitimu mwaka 2001.

Baadaye mwaka 2004 hadi 2006 nilisoma Chuo cha Ualimu cha Eckernforde kilichopo Tanga na kupata Diploma ya Ualimu, kisha mwaka 2009 alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tawi la Iringa (MUCE) na kuchukua Digirii ya Ualimu.

Baada ya hapo, mwaka 2013 niliajiriwa na Shule ya Sekondari, White Lake iliyopo Changanyikeni, jijini Dar es Salaam na nimepita shule mbalimbali na sasa nipo Efforts, nikiwa mwalimu na meneja wa shule.

Hivyo, hapa nilipo, mimi ni mwalimu, mwanasheria na mjasiriamali na ninaamini kwamba kwa umri nilio nao, Mungu akinijalia, nitaendelea kujipanga zaidi kwa ajili ya maisha yangu ya baadaye, kwani kawaida ya mjasiriamali anafikiria namna ya kubuni biashara mpya, bidhaa mpya.

Kwa hiyo na mimi kama mjasiriamali, sina budi kufanya hivyo kwa ajili ya kupiga hatua zaidi kwenda mbele.

**SWALI: Unazionaje shughuli za ujasiriamali nchini?**

**JIBU:** Katika mazingira ya sasa, ni muhimu watu kuwa wajasiriamali, kwa sababu kumekuwapo mabadiliko makubwa ya kiuchumi, ambayo yametoa nafasi kwa watu kuweza kuingia kwenye ujasiriamali na kufanikiwa.

Ukosefu wa ajira, pia changamoto zinazowapata watu na kusababisha wengine kujiingiza katika ujasiriamali, kwani katika ulimwengu wa sasa, ambao ajira zimekuwa ngumu na shida kupatikana, ujasiriamali na biashara vimekuwa ndio kimbilio la wengi kama njia kuu ya kujipatia kipato ingawa inawezekana wapo ambao bado hawajafanikiwa.

Sababu kubwa zinazoelezwa na wataalam wa mambo ya uchumi, ni kwamba biashara nyingi zinakufa kutokana na ukosefu wa elimu inayohusu ujasiriamali. Lakini, ninaamini kwamba elimu imekuwa ikitolewa kwa wingi, kinachotakiwa ni sisi wajasiriamali kuizingatia ili iweze kutunufaisha huko tunakoelekea.

BIASHARA

WADAU WAFUNGUKA

# Biashara mahindi ya kuchoma, vipi msimu mvua, mawingu tu?

• Wasifia kiungo wa 'pasi ndefu' • Mauzo yanalipa; ina afya tele • Ya kuchoma wanaume kona zote



Biashara ya mahindi ikiendelea. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Tatu Tambile**

UNAPOFIKA msimu ni jambo la kawaida katika kila mji kunashuhudiwa kushamiri biashara ya uuzaji mahindi mabichi yaliyochomwa, huku kukiwapo wateja wanaomiminika kununua.

Pia, inashamiri katika msimu wa mvua mawingu, baridi kama ilivyo sasa katika maeneo mengi nchini. Ni kawaida kuona mahindi yakiuzwa pembezoni mwa barabara na hasa katika vituo vya mabasi au penye mikusanyuko ya watu.

Aidha, kuna kinamama ambao wanauza bidhaa hiyo kwa njia ya kuzitembeza mtaani. Hapo mara nyingi ni mahindi ya kuchemsha.

Biashara hii imekuwa ikishamiri katika mikoa mbalimbali, ikiwamo jijini Dar es Salaam, wafanyabiashara wa mahindi ya kuchoma ni wengi.

Kuhusu wateja wao inaelezwa wanaume ni wengi wanaochangamkia biashara hiyo ya mlo na wauzaji mahindi ya kuchoma wengi ni wanaume.

Japokuwa kuna kinamama wachache wanaojitokeza kununua, bado wengi huziandalia nyumbani na hata ya kuchemsha, Wanapouza hutumia staili ya ama kutega pembezoni mwa barabara au kutembeza mitaani, huku wakiyapigia debe kuita wateja.

Pia, limekuwa suala la kawaida kuwaona watu wakiwa wamesimama na kufunga miamvuli mikubwa ya kuzuia mvua na kutenga majiko yao yaliyokolezwa moto wa mkaa na kuanza kuchoma mahindi.

> “Wateja hupenda kutafuna mahindi ya kuchemsha yaliyokuwa ya moto, huku akitamba ni biashara inayomletea mara mbili ya msingi aliyonunulia bidhaa sokoni.



Na kama ilivyo uchuuzi wa aina nyingine, muuzaji huyu hupatikana mahali hapohapo, maarufu kama 'kijiwe chake.' Hiyo ipo sana katika mji mkubwa wenye hadhi ya jiji na manispaa au mji inayokua.

Kuna staili nyingi ya kumfikishia mteja bidhaa. Mahindi hayo yakishachomwa, hukatwa katika vipande vidogo na vikubwa wanavyouziwa wateja kwa bei ya Sh. 100 hadi Sh. 300, kutegemea na ukubwa wa vipande.

Lakini, mhindi mzima huuzwa kwa bei kati ya Sh.500, hadi Sh. 800 kutegemea na ukubwa wake. Kwa ukubwa wowote unaambatana na vinogesho pembeni, ikiwamo ndimu, pilipili na chumvi.

Hata hivyo, sio ajabu ya kuwapo tofauti ya bei, kutegemea na eneo na upatikanaji wa bidhaa, mathalan si ajabu kukuta tofauti ya bei kati ya Dar es Salaam na mkoa wa Tabora.

Inaelezwa kuwa biashara yenye faida kubwa, kwani kwa makadirio ya jijini Dar es Salaam, hindi hununuliwa kwa Sh.200 na linapochomwa linaingiza kati ya Sh.500 hadi 800 kwa hindi, hivyo inakadiriwa kuingiza faida mara mbili ya ilivyonuliwa.

Katika jiji la Dar es Salaam, madereva wa bodaboda wanatajwa kuwa wateja wakuu, wakiambatana na wapita njia.

Hili ni zao lilalolimwa katika kipindi chote, yaani kipindi cha masika na kiangazi, ambacho mfumo wa umwagiliaji unatumika zaidi.

**KWA NINI MASIKA TU?**

Swali ni kwamba ni kwanini mahindi ya kuchoma na ya kuchemsha huuzwa msimu wa mvua tu? Mosi wadau wake wanaeleza kwamba, inapofika kipindi cha mvua, wafanyabiashara hufumuka kwa wingi na kuanza kuichangamkia fursa ya kuuza mahindi ya kuchoma na baadhi ya kinamama mahindi ya kuchemsha.

Elisha Hassan, mfanyabiasha ya mahindi ya kuchoma na kuchemsha eneo la Kigamboni, anasema wateja wake wengi ni wanaume na wanapenda sana mahindi ya moto ya kuchoma na sababu kuu ni kwamba husaidia kutia nguvu na joto mwilini wao, kuwachangamsha hasa katika kipindi cha mvua, baridi na mawingu.

"Pia, nimegundua mtu akila hindi zima la Sh. 600 husaidia kuzima njaa, hivyo akinywa na maji hupiga pasi ndefu" anasema Hassan.

Nipashe iliamua kudadisi tafsiri ya 'pasi ndefu' ndipo ikafafanuliwa kwamba, mtu asipokula mchana' hivyo akila hindi zima moja, akinywa na maji anashiba na kujikuta anasubiri mlo wa jioni.

Muuza mahindi huyo anasimulia kwamba, mtu akiwa ambaye ameshakula chakula kikamilifu, ni nadra kumkuta anatafuna mahindi ya kuchoma zaidi ya vipande viwili au hindi zima.


Mwanamama Hadija Juma, ni muuzaji mahindi ya kuchemsha anayesema katika msimu wa mvua huwa anaenda sokoni kununua mahindi, anayachemsha na kuyauza.

Anasema, wateja hupenda kutafuna mahindi ya kuchemsha yaliyokuwa ya moto, huku akitamba ni biashara inayomletea mara mbili ya msingi aliyonunulia bidhaa sokoni.

Hapi ndipo Nipashe ikahamisha udadisi kwa mnunuzi, ambaye alinunua hindi na kuanza kulitafuna mara moja, ambaye alitoa ufafanuzi wa kulikoni amenunua bidhaa hiyo.

Bila ya kutaja jina lake, anasema yeye anapendelea kutafuna mahindi ya kuchoma hasa katika kipindi cha baridi akifafanua:"Napendelea kutafuna mahindi ya kuchoma, nachangamsha mdomo si unajua meno yanashika ubaridi tukitafuna mahindi yanachangamsha mdomo."

Kitaalamu inafafanuliwa, kujenga tabia ya kula mahindi ya kuchoma au kuchemsha mwili unapata faida kubwa ikiwamo haja kubwa katika mtiririko unaofaa, mahindi yana maganda na kiini tete, hivyo ina kiwango kikubwa cha mafuta, protini, madini, vitamini na nyuzinyuzi (fibre) na kufanya ulaji wa mahindi ya kuchoma au ya kuchemsha huimarisha zaidi afya ya mlaji.





Wananchi wa Kijiji cha Bulyaga Juu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, ambao ni wanufaika wa mpango wa kuzinusuru kaya maskini unaotaribiwa na Mpango wa Maendeleo ya Jamii nchini (Tasaf), wakisikiliza maelekezo kutoka kwa uongozi na wajumbe wa mfuko huo (hawapo pichani). **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wanufaika kaya maskini watakiwa kupisha wengine

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

WANUFAIKA wote wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF) kupitia mpango wa kuzinusuru kaya maskini ambao wamewezeshwa kumudu gharama za kuendesha maisha, wametakiwa kujiandaa kuondokana ili kuwapisha wengine.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Tasaf, Ladislaus Mwamanga, ambaye aliambatana na wajumbe wa kamati ya taifa ya uongozi Tasaf makao makuu, wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Bulyaga Juu Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ambao ni wanufaika wa mpango wa kuzinusuru kaya maskini.

Mwamanga alisema lengo la Tasaf ni kuziwezesha kaya maskini, hatua ambayo ilifanikiwa kwani wanufaika walipatiwa fedha za kufungua miradi na kuendesha maisha yao.

Alisema awamu ijayo ya Tasaf ambayo ni sehemu tatu mzunguko wa pili utazisaidia kaya zote maskini nchini ambazo hapo awali hazikunufaika na mpango huo.

"Awamu ijayo tunakuja na utaratibu mwingine wa kuzisaidia kaya ambayo mwanzo hazikufikiwa na tutafika maeneo yote nchini kwa hiyo nawaomba walionufaika awamu iliyopita mjiandae kuondoka kwani sasa mnaweza kujisimamia na kuendesha yenu," alisema Mwamanga.

Alipongeza taarifa ya Tasaf Wilaya ya Rungwe kwa kuwa kufanya vizuri katika utekelezaji wa mpango wa kuzinusuru kaya maskini kwa kuanzisha miradi ya maendeleo ikiwamo uzalishaji wa miche ya parachichi na mradi wa maji.

Katika taarifa yake Mratibu wa Tasaf Wilaya ya Rungwe, Lydia Mwakatumbula, alisema tangu mwaka 2015 hadi 2019 kati ya vijiji 126 vya wilaya hiyo jumla ya kaya 164 ambayo ni sawa na asilimia 77 vilinufaika na kati ya hizo, vijiji 117 vinapata ruzuku na vingine tisa havipati ruzuku kwa kuwa vinatumika kama vijiji vya mlinganisho.

Alisema mpango huo umesaidia kutengeneza ajira za muda ambao katika vijiji hivyo tisa ndivyo vinatekeleza uhimilishaji fedha bila kuwa na miradi ya ajira za muda.

Aliongeza kuwa jumla ya kaya maskini 6,132 ziliandikishwa ambayo ni sawa na asilimia 57 ya zilizokuwa zimetambuliwa.

Kaimu Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Tasaf nchini, Dk. Naftali Ng'ondi, aliishauri Wilaya ya Rungwe kuweka utaratibu wa kuhabarisha jamii kupitia vyombo vya habari mafanikio ya mradi wa Tasaf.

"Taarifa ya utekelezaji wa mpango wa Tasaf wilayani Rungwe imekuwa ya mfano kwa sababu imegusa walengwa na kuanzisha programu mbalimbali ambazo zimeleta manufaa kwa wananchi tuahidi kuendelea kupanua wigo zaidi walengwa walete tija," alisema Dk. Ng'ondi.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Challya, aliishukuru Tasaf kwa kupokea na kuridhika na taarifa hiyo na kuwaomba kufikia kaya nyingine maskini ambazo awali hazikunufaika.

Aliwashauri wananchi wake kutumia vizuri fursa wanazozipata kupitia mpango huo ili waweze kujikwamua na umaskini kwa kuhakikisha fedha wanazozipata wanaanzisha miradi endelevu.

# Watoa masharti kushiriki uchaguzi wa serikali mitaa

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

ZAIDI ya wakazi 1,000 wa Kijiji la Msesule, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, wamedai hawatashiriki uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24 mwaka huu, endapo serikali haitaingilia kati mgogoro wa shamba la mpunga kati ya wakazi hao na kikundi cha watu 30 cha Mahalala.

Waliyasema hayo wakati wakizungumza na waandishi wa habari kijijini hapo, ambapo walisema mgogoro huo wa kugombea mashamba umesababishwa na kikundi cha Mahalala ambao wana lengo la kuwadhulumu shamba lenye ukubwa wa ekari 1,700 ambalo linamilikiwa na wanakijiji kwa miaka mingi.

Miongoni mwa wananchi hao, James Katembo, alisema endapo serikali haitawasaidia kutatua mgogoro huo hawatakuwa tayari kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kuanza hivi karibuni.

"Wananchi wote wa kijiji cha Msesule wanategemea shughuli za kilimo cha mpunga kuendesha maisha yao, hivyo kitendo cha kikundi cha Mahalala kutaka kuny'ang'anya mashamba yao ambayo wanayatumia miaka yote ni cha uonevu na hawapo tayari kuyaachia mashamba," alisema Katembo.

Riziki Mbilinyi alisema mgogoro huo umechangia ukosefu wa chakula kijijini hapo na kukwama kwa ujenzi wa miradi ya kijiji Madarasa na nyumba ya daktari kwa sababu ya mivutano.

Hata hivyo, uongozi wa Serikali ya Kijiji hicho chini ya mwenyekiti wake, Adamson Mwasubila, umeeleza kuunga mkono uamuzi wa kususia uchaguzi wa serikali za mitaa endapo mgogoro huo wa mashamba hautatatuliwa.

Akiwa ziarani mkoani Mbeya Mei 2, mwaka huu, Rais John Magufuli aliagiza viongozi wa serikali kutatua migogoro ya ardhi katika Wilaya ya Mbarali.

Lakini Septemba 11, mwaka huu, kuliibuka mapigano baina ya wananchi wa Kijiji cha Msesule na Kikundi cha Mahalala na kusababisha watu 11 kujeruhiwa kwa kukatwa mapanga na kuchomwa na vitu.

# Wanafunzi kulindwa kwenye daladala

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya kitengo cha Dawati la Jinsia, limeanzisha kampeni ya kupinga ukatili kwa wanafunzi wanaotumia usafiri wa daladala ili waweze kuhudhuria masomo kwa wakati.

Hayo yalisemwa jana na Mratibu wa Dawati la Jinsia Mkoa, Janeth Masangano, alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusiana na hali ya vitendo vya ukatili wa kijinsia katika Mkoa wa Mbeya.

Alisema wameamua kuanzisha kampeni ya kupinga ukatili wa kijinsia kwenye vyombo vya moto hususan daladala dhidi ya watoto wa shule kutokana na manyanyaso wanayoyapata kutoka kwa makondakta na abiria.

Alisema wanafunzi hupokea matusi au kuondolewa kwenye viti kwa sababu kulipa nauli kidogo ukilinganisha na watu wazima, hivyo makondakta hawana faida na kulazimika kuwanyanyasa.

"Tunaanzisha kampeni ya kupinga ukatili wa kijinisia kwenye daladala dhidi ya wanafunzi kuanzia kwenye vituo hadi kwenye magari yenyewe tutatoa elimu kupinga vitendo hivyo," alisema Masangano.

Aliwaomba wananchi na wadau wengine kuingua mkono kampeni hiyo, ili iweze kufanikiwa na kusaidia watoto kuhudhuria vipindi vya masomo kwa wakati na kutumiza ndoto zao.

Alisema kampeni hiyo itakuwa endelevu mpaka hapo vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vitakapokoma na kwamba watakaokaidi maagizo na elimu hiyo watachukuliwa hatua za kisheria kwa sababu watoto wana haki pia ya kutumia usafiri huo.

Mmoja wa makondakta wa daladala katika Jiji la Mbeya, Jackson Mwaipopo, alisema vitendo vya ukatili kwa wanafunzi ndani ya magari vinasababishwa na wao wenyewe kwa sababu wengi wao hawana nidhamu.

Alisema baadhi ya wanafunzi wanakaa kwenye viti wakati wazee au watu wazima wamesimima ndani ya gari ilhali wanalipa nauli kidogo.

Aliwasihi wanafunzi kuwa na nidhamu na kuheshimu watu wazima kwenye vyombo vya usafiri na kwamba kwa kufanya hivyo kutapunguza ukatili unaolalamikiwa.

Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Meta, Veronica Juma, alisema makondakta na madereva walio wengi hasa nyakati za asubuhi na jioni huwakatilia kupanda kwenye daladala bila nauli kubwa, lakini pia hubana nafasi.





# Zimamoto kununua magari ya kisasa

Na Renatha Msungu, DODOMA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji nchini limetenga Sh. bilioni 4.5 katika mwaka wa fedha 2019/20, kwa ajili ya kununua magari matano ya kisasa yenye mitambo ya kuzimia moto ili kuimarisha utendaji wa jeshi hilo.

Jeshi hilo pia limeanza ukarabati wa magari mengine sita ili liweze kufanya kazi kwa ufasaha.

Akizungumza jana jijini Dodoma, Kamishna wa Fedha na Utawala wa jeshi hilo, Baraka Semwanza, alisema bajeti hiyo imetengwa na serikali katika mwaka wa fedha ili kuhakikisha sekta hiyo inaboreshwa na kukabiliana na majanga ya moto pindi yanapotokea.

Alisema magari hayo ambayo ni mitambo yatasambazwa mikoa mbalimbali ikiwamo Dodoma.

Semwanza alisema hatua hiyo itasaidia kuweka jamii salama kwenye majanga ya moto.

"Tumetenga bajeti ili kuhakikisha tunakuwa na magari ya kutosha ambayo yatasambazwa katika vituo mbalimbali ili yakafanye kazi pale majanga ya moto yanapotokea," alisema.

Alisema, lengo ni kuona wanawajibika ipasavyo katika sehemu husika ambazo wanatakiwa kwenda pale wanapoitwa kusaidia majanga ya moto.

Aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo pale wanapoona sehemu limetokea tatizo la moto kupitia namba ya jeshi hilo ambayo imetolewa.

Kamishna Semwanza alisema mara kwa mara watu huchelewa kutoa taarifa mpaka moto unateketeza vitu vyote ndipo wanatoa taarifa katika jeshi hilo.

"Tunaomba wananchi wawe wanatoa taarifa haraka wanapoona janga la moto limetokea sehemu hiyo, itaturahisishia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kufika eneo hilo kwa wakati," alisema Kamishna Semwanza.

Alisema ushirikiano kati ya wananchi na jeshi utasaidia jamii isiathirike kiasi kikubwa na majanga ya moto yanapotokea.

Pia alisema Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kutoa elimu kwa wananchi jinsi ya kujikinga na majanga ya moto maeneo mbalimbali.

Alisema lengo la kutoa elimu hiyo ni pamoja na kutaka kuiweka jamii sawa ikiwamo kujua hatua za awali za uzimaji moto.




Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mukunda (kulia), akiwasikiliza wanafunzi wa Shule ya Msingi Mpalanga, wilayani humo, mkoani Dodoma, alipotembelea shule hiyo, juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Posta kuongeza huduma kwa wateja

Na Augusta Njoji, DODOMA

SHIRIKA la Posta Tanzania limejipanga kuongeza utoaji huduma na usambazaji wa barua, nyaraka, vipeto na vifurushi ili kuwafikia wananchi wa Jiji la Dodoma kwa haraka.

Kauli hiyo ilitolewa jijini hapa na Ofisa Mwandamizi Mkuu wa Posta Dodoma, Michael Mwanachuo, kwenye maadhimisho ya miaka 145 ya Umoja wa Posta Duniani.

Katika maadhimisho hayo, shirika hilo lilitoa msaada wa vyakula na vinywaji kwa kituo cha kulea watoto wenye mtindio wa ubongo cha Miyuji Cheshire, jijini hapa.

Akizungumza shirika hilo lilivyojipanga, Mwanachuo alisema, limejizatiti kuhakikisha linasambaza kwa haraka barua, nyaraka vifurushi na vipeto katika jiji hilo.

"Katika kuunga mkono juhudi za serikali za kuhamia Dodoma, tumejipanga ipasavyo kuhudumia Jiji la Dodoma na kwenye mji wa serikali ulioko Mtumba," alisema.

Alisema hatua hiyo inalenga kwenda na kasi ya awamu ya tano katika kuchangia kukuza uchumi wa kati nchini ifikapo 2025.

"Tumejipanga sasa tunatekeleza hili kwa kusambaza kwa haraka barua, vifurushi na vipeto kwa mtu mmoja mmoja, taasisi na zaidi kwenye mji wa serikali," alisema.

Vile vile, alisema usambazaji wa barua umekuwa rahisi kwa shirika hilo hasa kutokana na eneo kubwa la Mkoa wa Dodoma kuwa na majina ya mitaa au anuani za makazi.

"Dodoma ilikuwa ni mikoa mitatu ya mwanzo ambayo ilianza utekelezaji wa anuani za makazi, hivyo mji una mitaa yenye majina hata kule ambako hakujaendelea tayari kuna mitaa," alisema.

Aliongeza kuwa anuani za makazi imeliwezesha shirika na wateja wenye anuani sahihi za makazi kufikishiwa barua, vifurushi na vipeto kwa urahisi.

Kuhusu msaada huo kwa watoto wenye mahitaji, Mwanachuo alisema wameamua kuadhimisha maadhimisho hayo na watoto hao.

Akipokea msaada huo, Sista Theresia Cosmas wa kituo hicho, alilishukuru shirika hilo kwa kuona umuhimu wa kutoa msaada huo wa vyakula ambao alisema utasaidia kwa kiwango na kwa kuonyesha moyo wa upendo kwa watoto hao wenye mahitaji maalum.

Alisema kuwa kwa sasa kituo chake kinakabiliwa na tatizo la nishati hususan uhaba wa kuni na dawa kwa ajili ya kuwatibia watoto.

Alisema siku za nyuma watoto walikuwa wanatibiwa kwa msamaha katika Hospitali ya Milembe, lakini sasa hilo limeondolewa hivyo zinahitajika dawa kwa ajili ya watoto hao.

Alitoa wito kwa taasisi nyingine kujitokeza kuwasaidia watoto hao hata kufika katika kituo hicho na kushiriki michezo na watoto wao ili nao wajione ni sehemu ya jamii.

# Bahi watakiwa kulinda ardhi

Na Augusta Njoji, DODOMA

UONGOZI wa Wilaya ya Bahi umeombwa kupanga mikakati kabambe ya kulinda na kuhifadhi mazingira ikiwamo Mbuga ya Sulungai na Bwawa la Nondwa ili kuondokana na uharibifu wa mazingira.

Ombi hilo lilitolewa jana na mmoja wa wakazi wa wilaya hiyo ambaye ni mwanaharakati wa utunzaji mazingira Damian Chilala, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema kama maeneo hayo yakitunzwa na kuwekewa mikakati kabambe yataleta tija kwa wakazi wa eneo hilo.

Chilala alieleza kuwa katika Tarafa ya Chipanga kuna Bwawa la Nondwa lililochimbwa enzi za ukoloni mwaka 1958 na hutunza maji mwaka mzima likiwa na vyanzo vya mito inayoingiza maji ndani ya bwawa hilo.

Alisema pia kuna uvuvi wa samaki mwaka mzima ambao walishapandikizwa kwa miaka mingi na kuendelea kuzaliana pamoja na shughuli za kilimo cha mbogamboga kama vile, vitunguu, nyanya na mahindi ya kumwagilia ambazo huuzwa jijini Dodoma na maeneo mengine.

Hata hivyo, alisema tatizo kubwa ni misitu iliyopo kwenye vyanzo vya maji hailindwi na inaendelea kutelekezwa huku mito hiyo inazidi kukauka.

"Mvua nazo zinazidi kuhama katika kunyesha ni hatari kwa bwawa kukosa maji, ni hatari kwa uvuvi na kilimo cha kumwagilia ni hatari kwa mifugo," alisema.

Aliwataka viongozi wa kiserikali kulishughulikia jambo hilo kwa kutoa elimu pamoja na kuhakikisha sheria zinafuatwa ili kuliokoa eneo hilo.

Alibainisha kuwa endapo mazingira ya vyanzo vya maji vitalindwa na kuhifadhiwa yataleta manufaa katika eneo hilo kwa kuwa kwa sasa kumejengwa chuo cha Veta, shule ya msingi na sekondari na vyote vinategemea bwawa hilo.

Kuhusu mbuga ya Sulungai, alisema kama ikitunzwa itasaidia shughuli za kilimo cha mpunga na uvuvi wa samaki.

Chilala alisema mbuga hiyo ina vyanzo vya mito mikubwa zaidi ya 10 na midogo zaidi ya nane, vyanzo vya mito hivyo viongozi wanapaswa kuangalia na kulichukulia uzito suala la utunzaji wa mazingira.



# Asisitiza sayansi kupata wataalamu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema taifa linahitaji wataalamu wake wenyewe na hilo litawezekana iwapo wanafunzi wataelekeza nguvu zao katika taaluma hasa masomo ya sayansi.

Balozi Iddi aliyasema hayo jana wakati wa hafla maalum ya kuwazawadia wanafunzi wa Chuo cha Kiislamu Micheweni Pemba, zawadi zilizotolewa na mfanyabishara maarufu nchini, Said Nassir Nassor Bopar, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi aliyotoa kwa wanafunzi hao miezi michache iliyopita.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, imejipanga kuendelea kuimarisha miundombinu ya elimu ili mtoto afaidike na matunda ya elimu bila malipo iliyotangazwa na mwasisi wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Mwaka 1964, Mzee Abeid Amani Karume.

Balozi Iddi alisema wakati umefika sasa kwa wanafunzi wote nchini kuacha mzaha na kujikita zaidi katika kuisaka elimu mahali popote kwa vile fursa za kufanya hivyo zipo.

Makamu wa Rais alisisitiza umuhimu wa kuimarishwa kwa ushirikiano baina ya wanafunzi wa jinsia zote, walimu na wazazi ili kazi ya upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi wote iwe rahisi na kufikia mafanikio yaliyokusudiwa.

"Jukumu letu serikali limeshakamilika la kukutandikieni jamvi la kupata taaluma kwa njia mwafaka. Sasa kazi ni kwenu kuchangamkia fursa hizo," alisema Balozi Iddi.

Pia alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado ina nia ya kumwona mtoto wa visiwa vya Zanzibar mwenye kipaji anakamilisha kiu yake ya kujipatia elimu kwa mujibu wa matakwa yake.

Alisema Rais wa Zanzibar katika kutilia mkazo suala hilo, kila mwaka amekuwa akiongeza ufadhili kwa wanafunzi wanaofaulu vyema daraja la kwanza kuendelea na masomo yao ya juu iwe ndani au nje ya nchi.

Balozi Iddi alisema mchango mkubwa unaotolewa na mfanyabiashara huyo mzalendo utaendelea kuthaminiwa na serikali kwa vile hulenga moja kwa moja kwa jamii katika kupunguza changamoto zinazowakwaza katika maisha yao ya kila siku hasa katika sekta za elimu na afya.

Kwa upande wake, Nassor aliwatahadharisha wanafunzi hao kwamba bila elimu mwanadamu hawezi kujifanyia chochote cha uhakika katika maisha yake.

Alisema elimu hiyo iwapo haitazingatia hekima na busara, mwanafunzi hasa mtoto wa kike inaweza kumletea shaka hasa kipindi hiki kilichokumbwa na mfumuko wa matendo maovu ya udhalilishaji wa kijinsia.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, alisema wizara hiyo itaendelea kushirikiana na wadau wa sekta ya elimu katika kuona vijana wa Zanzibar wanajikomboa kielimu.

Wakati huo huo, Balozi Iddi alikabidhi chakula kwa uongozi wa Hospitali ya Vitongoji na kugawa miwani kwa wanafunzi 119 vyote vikiwa vimetolewa na mfanyabiashara Said Nassir Nassor kukamilisha ahadi aliyotoa miezi miwili iliyopita.

Alisema vifaa na misaada inayotolewa na wahisani lazima vilengwe na kuwafikia wale walinaokusudiwa.

# Wafanyakazi wa meli wanusurika kifo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAFANYAKAZI watatu wa meli ya mafuta ya MT. Ukombozi wamenusurika kufa baada ya meli hiyo kupata hitilafu ya moto katika sehemu ya kisima cha kuhifadhi mafuta katika Bandari ya Wesha, Pemba.

Ajali hiyo ilitokea jana asubuhi wakati wafanyakazi hao wakifanya usafi katika meli baada ya kushusha mafuta.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mustafa Aboud Jumbe, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kusema imesababishwa na hitilafu katika kisima cha kuhifadhi mafuta.

Kutokana na hitilafu hiyo, wafanyakazi hao walisafirishwa kwa ndege kutoka Pemba kwenda Unguja kwa matibabu na kupokewa na uongozi wa wizara.

"Wafanyakazi wetu watatu katika meli ya MT. Ukombozi wamejeruhiwa na moto baada ya kutokea hitilafu wakati wakifanya usafi kwenye meli katika Bandari ya Wesha," alisema na kuongeza kuwa moto huo ulidhibitiwa kabla ya kuleta athari.

Meli ya MT. Ukombozi inamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambayo hivi karibuni ilinunuwa meli mpya ya mafuta kutoka China iliyopewa jina la MT. Ukombozi namba mbili.

Meli hiyo hufanya safari zake katika Bandari ya Mombasa kwa ajili ya kubeba mafuta na kusambaza katika Bandari ya Wesha iliyoko Pemba na Mtoni kwa upande wa Unguja.

Majeruhi hao walitajwa kuwa ni Ali Juma Ame, Hafidh Slime Kona na Issa Daudi Omar.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akiwapungia mkono wananchi wa Wilaya ya Mkoani Kisiwani Pemba, alipowasili katika viwanja vya ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Mohamed Juma Pindua, kuzungumza na wazee wa chama hicho, jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Ataka uchunguzi wanaoshabikia ukatili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, ameitaka taasisi za kiraia zinazopambana na vitendo vya udhalilishaji, kufanya utafiti kama kuna mashirika ya nje ya nchi yanayounga mkono kuwapo kwa vitendo vya kingono.

Mahmoud aliyasema hayo jana, wakati akizindua mradi wa kuwawezesha wanawake na watoto wa kike kujua haki zao mradi ambao unatekelezwa na Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (Zafela) katika Ofisi za Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa) upande wa Zanzibar.

Alisema anashangazwa kuona vitendo hivyo vimekuwa vikiongozeka licha ya juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na serikali na asasi za kiraia.

"Ni vyema kukafanya utafiti ili kujua kama hakuna mashirika ya nje yanayounga mkono kuendelea kuwapo kwa vitendo hivi vya udhalilishaji ambavyo ni kinyume cha maadili, mila na silka za Watanzania," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa alisema ataendelea kushirikiana na asasi za kiraia kupunguza changamoto za kijamii katika taifa ikiwamo udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema kuna haja ya kutoa elimu ya udhalilishaji kwa mabaraza ya watoto ili kujua athari za vitendo hivyo na kujiepusha navyo.

"Tuko tayari kushirikiana na Zafela kutoa elimu katika dhana ya udhalilishaji ili kupunguza vitendo hivyo," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Zafela, Jamila Mahmdoud, alisema mradi huo utafanya kazi katika mikoa ya Kusini Unguja na Mjini Magharibi ili kupunguza vitendo vya udhalilishaji.

Alisema bado hali hairidhishi kutokana na kushamiri kwa vitendo vya udhalilishaji wanavyofanyiwa wanawake na watoto na kwamba kama hali hiyo haitadhibitiwa, taifa litakosa wataalamu.

# WWF yasaidia udhibiti wa ujangili

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

KATIKA kukabiliana na ujangili wa faru na tembo nchini, Shirika la Uhifadhi Mazingira Duniani (WWF) limetoa vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 22 kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) mkoani Morogoro ili kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya ujangili wa wanyamapori.

Vifaa hivyo vilivyotolewa na WWF vimelenga kuimarisha TAWA katika eneo la ulinzi wa faru waliopo katika Pori la Akiba la Selous na mengine ambao wapo hatarini kutoweka kutokana na matishio ya ujangili.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA, msimamizi wa masuala ya wanyamapori wa WWF Tanzania, Prof. Noah Sitaki, alisema msaada huo ni sehemu ya kuunga mkono Serikali ya Tanzania ambayo imekuwa ikifanya jitihada kubwa za kupambana na vitendo vya ujangili nchini.

"Tunapongeza sana serikali ya sasa, tangu imeingia madarakani imeonyesha wazi kupambana na vitendo vya ujangili nchini na tunaona hivi sasa wanyama wanaongezeka, hivyo sisi kama WWF tumeona tuunge mkono kwa kuwapatia vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuendeleza mapambano hayo ya ujangili," alisema Prof. Sitaki.

Alisema WWF litaendelea kushirikiana na Tanzania kuhakikisha inaongeza idadi ya faru ambao wapo katika hatari ya kutoweka kwa kuwaongezea ulinzi wa kutosha katika Pori la Akiba la Selous ambalo linapita katika mikoa mingi kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Kamishna wa uhifadhi wa TAWA, Dk. James Wakibarwa, alisema msaada huo utakuwa chachu ya kuongeza nguvu kwa ajili ya mapambano dhidi ya ujangili wa faru pamoja na wanyama wengine pamoja na kusaidia kutoweka kwa wanyama hao.

Alisema TAWA itaendelea kushirikiana na WWF ambao wameonyesha nia ya kuhakikisha malengo ya kuongeza idadi ya wanyama Selous kutokana na umuhimu wake kuwa sehemu kubwa ya mazalio ya wanyama wanaohifadhiwa na hifadhi za taifa.

Kamishna wa Uhifadhi Wanyamapori wa TAWA, Mabura Misungwa, alisema kutokana na kuongeza ulinzi Selous, kwa sasa wanyamapori wanaishi kwa raha, na wamekuwa wakiongezeka kwa kasi na kwamba msaada huo utasaidia askari wa wanyamapori kuimarisha ulinzi.




Wananchi wa Mtaa wa Wapiwapi A, wilayani Masasi, mkoani Mtwara, wakimsikiliza Mkuu wa Wilaya hiyo, Selemani Mzee (wa tatu kushoto), wakati akitoa somo la umuhimu wa kujiandikisha katika daftari la wapiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa, baada ya kujiandikisha katika kituo hicho, jana. **PICHA: HAMISI NASIRI**

# Waziri: Marufuku kutumia kampuni binafsi Tehama

**Na James Mwanamyoeo,**
NAMTUMBO

SERIKALI imepiga marufuku taasisi za umma kutumia fedha za serikali kuzilipa taasisi binafsi ili kupatiwa huduma ambazo pia zinazotolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), George Mkuchika, alitoa agizo hilo kwa watumishi wa umma na waajiri serikalini, wakati wa kikao kazi chake na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kwa lengo la kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi hao.

Mkuchika alifafanua kuwa serikali imebadili Wakala ya Serikali Mtandao kuwa Mamlaka kwa sababu hivi sasa ina wataalamu wa kutosha wa Tehama, hivyo hakuna ulazima wa kuilipa kampuni binafsi ili kupata huduma ya Tehama.

"Kama serikali ina chombo chenye uwezo na weledi wa kutosha wa kutoa huduma za Tehama ikiwamo mifumo ya kielektroniki ya utoaji huduma, ni nini kinachoshinikiza Taasisi za Umma kuendelea kuomba kupatiwa huduma hiyo na kampuni za watu binafsi?" Mkuchika alihoji.

Waziri Mkuchika yuko katika ziara ya kikazi mkoani Ruvuma kwa lengo la kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa umma pamoja na kukagua utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini mkoani humo.

# Kabudi atamani Tanzania kuifikia China

**Na Enock Charles**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, amewataka Watanzania kufanya juhudi za kujiletea maendeleo ili kuzifikia nchi zenye uchumi mkubwa duniani kama China.

Waziri Kabudi mesema kwamba kuzifikia nchi hizo ni jambo linalowezekana. Waziri Kabudi aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa jengo jipya la wizara hiyo lililojengwa kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri ya China jijini Dar es Salaam juzi.

Alisema kujengwa kwa jengo hilo ni ishara kubwa ya ushirikiano wa China na Tanzania ambazo zilianzisha uhusiano wa kibalozi mwaka 1964 ambao umekuwa na manufaa makubwa.

"Katika miaka sabini ya uhuru wao China imefanya maendeleo makubwa sana ya mfano wa kuigwa kutoka nchi isiyokuwa na utajiri mkubwa nchi iliyokabiliwa na njaa watu kukosa mavazi na makazi leo ni nchi ya pili kwa ukubwa wa uchumi duniani," alisema.

Jengo hilo lenye ukubwa wa mita za mraba 19,040 lina ghorofa sita na vyumba 117 pamoja na maktaba ya kisasa na mgahawa. Pia ni jengo la pili kubwa zaidi kujengwa na Serikali ya China baada ya kujengwa kwa maktaba kubwa ya kisasa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Balozi wa China nchini, Wang Ke, alisema Serikali ya China iliwekeza dola milioni 22 ili kujenga jengo hilo ambalo linaweza kuhifadhi watu 400 lililoanza kujengwa Aprili mwaka 2016 akiipongeza Wizara ya Mambo ya Biashara ya Jamhuri ya Watu wa China kwa ushirikiano mzuri na Tanzania.

"Hili jengo limekuja wakati mzuri na kwa maoni yangu lina faida tatu.

Kwanza limesimama karibu na ukumbi wa Mikutano wa Mwalimu Nyerere ambalo nalo lilijengwa na kamuni kutoka China pili kutokana na Tanzania kuwa Mwenyekiti wa SADC litaiwezesha Wizara ya Mambo ya Nje kusimamia mikutano ya SADC na tatu, litakuwa kichocheo kwa wafanyakazi wa Wizara ya Mambo ya Nje kutokana na miundombinu bora," Balozi Ke alisema.

Balozi huyo alisema nchi hizo zimekuwa na ushirikiano mzuri na wa muda mrefu tangu mwaka 1964 wakati, hivyo kuwa na mafanikio makubwa kwa miaka 55 ya ushirikiano na kuiomba Tanzania kuendeleza ushirikiano huo.

HABARI KIMATAIFA

# Daktari aliyesaidia kupatikana Osama Bin Laden akata rufani

**ISLAMABAD,** Pakistan

DAKTARI wa Pakistani, Shakil Afridi, ambaye aliisaidia Marekani kumpata kiongozi wa kundi la Al-Qaeda Osama Bin Laden amekata rufani dhidi ya hukumu yake jela.

Ni mara ya kwanza kesi ya Afridi inasikilizwa katika mahakama ya wazi ambapo Jaji aliiahirisha hadi Oktoba 22, kutokana na ombi la waendesha mashtaka.

Kinachodaiwa kufanywa na Dk. Afridi kilikuwa aibu kubwa kwa Pakistani. Lakini yeye mwenyewe anadai ya kwamba alinyimwa haki yake wakati wa kusikilizwa kwa kesi hiyo, ambapo alihukumiwa miaka 33 jela.

**Makomando wa Jeshi la Wanamaji la Marekani walisafiri kwa helikopta kutoka Afghanistani mpaka Pakistani na kumuua.**

Hakushtakiwa rasmi kwa jukumu lake katika operesheni hiyo ya mwaka 2011 ya kumsaka na kumuua mtu aliyekuwa akitafutwa sana duniani.

Kufungwa kwake jela kulisababisha hisia kali hatua iliyosababisha Marekani kufutilia mbali msaada wake kwa Pakistan wa takriban dola milioni 33, ikiwa ni dola milioni moja kila mwaka kwa hukumu yake katika mahakama ya Peshawar.

Rais wa Marekani, Donald Trump, aliahidi katika uchaguzi wa 2016 kwamba atamwachilia huru Afridi baada ya dakika mbili iwapo atachaguliwa lakini hilo halijafanyika.

Huku daktari huyo akionekana kuwa shujaa Marekani, nchini Pakistani anaonekana kama msaliti ambaye aliliitea aibu kubwa taifa hilo.

Makomando wa Jeshi la Wanamaji la Marekani walisafiri kwa helikopta kutoka Afghanistani mpaka Pakistani na kumuua aliyepanga njama za mashambulizi ya Septemba 11 na kuondoka na mwili wake bila kuzuiwa.

Hatua hiyo ilizua maswali mengi ya iwapo Jeshi la Pakistani lilikuwa linajua iwapo Bin Laden alikuwa nchini humo.

Pakistani imesalia kuwa mshirika asiyeaminika katika vita vya Marekani dhidi ya wapiganaji wa Kiislamu. **BBC**



Mishumaa na maua ikiwekwa kuwakumbua waliouawa mji wa Halle Mashariki mwa Ujerumani. **PICHA: REUTERS**

## Mshambuliaji sinagogi atoa msimamo

**BONN,** Ujerumani

SHIRIKA linalofuatilia shughuli za mitandaoni za makundi ya jihadi na sera kali za kizalendo limesema mshambuliaji katika sinagogi la Halle, Ujerumani alichapisha mtandaoni msimamo wake kuhusu chuki dhidi ya Wayahudi.

Shirika hilo linalojulikana kama SITE pamoja na vyombo vya habari vya Ujerumani, vimesema mshambuliaji huyo mwenye silaha aliyewaua watu wawili kwenye mji wa Halle, Mashariki mwa Ujerumani alichapisha mtandaoni azimio linaloelezea msimamo wake kuhusu chuki dhidi ya Wayahudi wiki moja iliyopita.

Mkurugenzi wa SITE inayofuatilia pia makundi ya uhalifu wa chuki, Rita Katz ameandika katika ukurasa wa Twitter kwamba nyaraka, ambazo ni dhahiri zinaonyesha azimio la mtuhumiwa huyo zimeonekana mtandaoni zikionyesha picha za silaha na risasi alizotumia.

Pia zilionyesha lengo lake la kuwaua raia wa kigeni wakiwamo Wayahudi.

Gazeti la Ujerumani la Die Welt limeripoti kuwa nyaraka hizo zenye kurasa 10 zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza na zinataja hasa mpango wa kulishambulia sinagogi la Halle kwenye Jimbo la Saxony-Anhalt wakati wa sikukuu takatifu ya Wayahudi ya Yom Kippur. **DW**

## Wino kwa maharage kwampaisha

**TOKYO,** Japan

MWANAFUNZI Eimi Haga (19) wa Japan amefaulu mtihani wake kwa kiwango cha juu kwa kutumia mbinu za kihistoria za ninja kwa kuandika insha kwa wino usioonekana.

Haga alitumia mbinu alizotumia ninja "aburidashi", kwa kutumia muda mwingi kutengeneza wino kwa maharage ya soya na maneno yake yalionekana wakati Profesa wake alipoliungua karatasi katika jiko la gesi.

"Ni kitu ambacho nilijifunza nikiwa mdogo," Haga aliiambia shirika hilo la habari. "Ninadhani kuwa hakuna mtu mwingine ambaye anaweza kuja na wazo la aina hiyo."

Haga amekuwa akivutiwa na simulizi za 'ninja' katika vipindi vya televisheni tangu alipokuwa mdogo.

Baada ya kujiunga na Chuo Kikuu cha Mie nchini Japan, alichagua darasa la historia ya ninja na alitakiwa kuandika kuhusu makumbusho ya Ninja ya Igaryu aliyowahi kuyatembelea.

"Wakati profesa aliposema kuwa atatoa alama nzuri kwa mwanafunzi atakayekuja na ubunifu wa aina yake, nilijikita kuwa insha yangu lazima niiandike vizuri zaidi ya wengine," alisema mwanafunzi huyo.

"Nilifikiria kwa muda na kuamua kuandika kuhusu wazo la ninja aburidashi."

Haga aliloweka maharage ya soya usiku mzima na baadaye kuyasugua na kuyapondaponda kwenye nguo.

Alichanganya maharage na maji na kusubiri kwa saa mbili kabla hajaanza kuweka umakini katika kuandika insha yake kwa kutumia brashi kwenye karatasi nyembamba ya jadi ijulikanayo kama 'washi'. Kipindi ambacho maneno yalikuwa yamekauka yalikuwa hayaonekani lakini profesa hakutupa karatasi kwenye takataka, kwa sababu kulikuwa na ujumbe ulioandikwa kawaida kuwa liweke karatasi kwenye moto. **BBC**

## China, Marekani kuanza mazungumzo ya biashara

**BEIJING,** China

WAZIRI wa Biashara wa Marekani, Wilbur Ross, ameshambulia utendaji wa China katika biashara na kusifu uhusiano wa kiuchumi kati ya Marekani na Australia huku vita vya biashara vikiendelea kati yake na China.

Ross aliuambia mkutano wa biashara mjini Sydney jana kuwa Rais Donald Trump hakutaka kutumia ushuru kuilazimisha China kubadili utendaji wake lakini anahisi ilikuwa muhimu.

Matamshi hayo yanakuja wakati maofisa wa Marekani na China wanajitayarisha kurejea katika mazungumzo ya biashara mjini Washington jana.

Uamuzi wa Rais Trump mwaka jana kuweka ushuru dhidi ya bidhaa za China umetikisa masoko ya dunia na kuongeza hali ya wasiwasi kuhusiana na mwelekeo wa uchumi wa dunia. **DW**

# Mahakama kusikiliza kesi 60 kwa 'video conference'

**Na Enock Charles**

MAHAKAMA ya Rufani inatarajia kusikiliza kesi 60 kwa mfumo mpya wa mawasiliano kwa njia ya picha maarufu kwa jina la Video Conference kuanzia Oktoba 9 hadi 16 mwaka huu.

Imeelezwa mfumo huo utapunguza gharama na kuokoa muda wa kusikiliza kesi hizo.

Msemaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Nurdin Ndimbe ,ameeleza kuwa mfumo huo mpya unalenga kuokoa muda na kupunguza gharama kutokana na usikilizwaji wa kesi hizo.

"Changamoto zinaweza kuwapo lakini la muhimu ni kushukuru kwanza kwa kuanzishwa kwa mfumo huo ambao utaokoa muda na kupunguza gharama za majaji na mawakili kusafiri huku na kule kufuata kesi ilipo" Ndimbe alisema

Wakichangia maoni yao katika ukurasa wa twitter wa Mahakama hio, baadhi ya watu wamekuwa na maoni tofauti kuhusu mfumo huo wa Mahakama wengine wakiunga mkono na kuipongeza Mahakama ya Tanzania kwa kupiga hatua hiyo, huku wengine wakikosoa.

Mchangiaji mmoja kwa jina la Kusekwa aliitaka Mahakama ijikite kutoa elimu kuhusu Katiba na Sheria za Mitandao ili kuondoa sintofahamu kwa wananchi katika masuala yahusuyo sheria mbalimbali za nchi.

"Pia mjikite kwenye kutoa elimu kuhusu Katiba mfano sheria za mitandao na haya yote ambayo yanaleta sintofahamu katika vichwa vya watu," alisema katika sehemu ya ujumbe wake.

Mchangiaji mwingine aliyefahamika kama Vitabu vya Sheria, aliipongeza Mahakama hiyo kwa kupiga hatua hiyo na kueleza kuwa imesaidia kurahisisha mazingira ya utendaji kazi mahakamani hapo na kuwa itawafaa wananchi.




Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Dk. Jim Yonazi, akimkabidhi zawadi mshindi wa kwanza wa shindano la uandishi wa barua kimataifa nchini, Joan John Erasto (wa pili kushoto), wa Shule ya Sekondari Binza, mkoani Simiyu, katika maadhimisho ya Siku ya Posta Duniani, jijini Dar es Salaam jana. Wa tatu kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika hilo, Dk. Haruni Kondo, Kaimu Postamasta Mkuu, Mwanaisha Said (kulia) na Mwalimu wa shule hiyo, Japhet Kilela. **NA MPIGAPICHA WETU**

# TRA yasisitiza matumizi stempu kielektroniki

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Dk. Edwin Mhede, amewataka wazalishaji wanaotakiwa kutumia stempu za kodi za kielektroniki - Electronic Tax Stamp (ETS) kuendelea kuzitumia kama ilivyoelekezwa na sheria na taratibu za kodi.

Amesema faida yake ni kwa wazalishaji kufahamu bidhaa halisi zinazoingia sokoni ili kulinda viwanda vyao.

Dk. Mhede aliyasema hayo alipotembelea Kiwanda cha Bia, mkoani Mbeya ili kujionea namna stempu za kodi za kielektroniki zinazofanyakazi katika kiwanda hicho.

Alisema ETS inasaidia kukusanya taarifa sahihi si kwa matumizi ya kukadiria kodi pekee bali inamsaidia pia mzalishaji kujua kiasi alichozalisha na kwa muda gani, lakini itamsaidia kuona kama kuna changamoto yoyote kuifanyia kazi mapema kitu ambacho ni muhimu sana katika shughuli za uzalishaji.

"Ujumbe wangu kwa wazalishaji wengine ni kwamba waendelee kutumia stempu za kodi za kielektroniki kama tulivyoelekezwa na sheria na taratibu na kodi kwa kuwa inasaidia kuongeza ufanisi katika uzalishaji na kuweka taarifa sahihi za uzalishaji," alisema.

Hata hivyo, alisema katika matumizi ya mifumo, changamoto hazikosekani, lakini ni vema kutumia na kufahamu na kuzifanyia kazi," alisema.

Naye Meneja wa Kiwanda cha Bia mkoani Mbeya, Godwin Fabian, alisema Kiwanda cha Bia Tanzania kinaamini kwamba ETS ni msaada mkubwa kwa wazalishaji kwa kuwa inawezesha kugundua bidhaa zisizo halali na zinazoingia sokoni bila kufuata taratibu za uzalishaji na ulipaji kodi.

Matumizi ya stempu za kielektroniki za kodi kwa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa yalianzishwa kuchukua nafasi ya matumizi stempu za karatasi ambazo matumizi yake yalihusishwa na vitendo vya ukwepaji kodi pamoja na bidhaa bandia kwa kiasi kikubwa. Hii ni mojawapo ya hatua ya serikali inayolenga kuboresha usimamizi wa kodi nchini.

Wanufaika wa mfumo huo ni serikali, wazalishaji, waagizaji na watumiaji na faida zake ni kulinda mapato ya serikali kwa kuzuia bidhaa bandia, kumwezesha mtumiaji kutambua bidhaa yenye stempu halali kwa kutumia simu ya mkononi pamoja na kuongeza uhiari wa ulipaji kodi kwa kutengeneza wigo sawa wa ushindani kwa wafanyabiashara wote wanaozalisha na kuingiza bidhaa nchini.

Faida nyingine ni kuwezesha ufuatiliaji wa bidhaa kutoka viwandani, mipakani, bohari zilizoruhusiwa, majengo ya kutunzia bidhaa, sokoni hadi kwa mlaji na kuwezesha usimamizi wa bidhaa zinazotengenezwa au zinazoingizwa kutoka nje ya nchi.

# NMB yaahidi makubwa kwa wateja wakubwa

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya NMB imesema itaendelea kuboresha huduma kwa wateja wake wakubwa nchini kulingana na mahitaji yao ya kifedha na kuwa na uhakika na huduma unaotokana na ukubwa wa mtaji wa benki hiyo unaofikia zaidi ya Sh. bilioni 700.

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Ofisa Mkuu wa Idara ya Wateja Wakubwa wa NMB, Aziz Chacha, wakati akifungua Jukwaa la wateja wakubwa lililofanyika jijini Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya huduma.

Chacha alisema uwezo wa kipesa unaotokana na ukubwa wa mtaji katika benki ya NMB ni mkubwa, unaowawezesha kuwahudumia wateja wa aina zote, wakiwamo wakubwa ili kuwawezesha kumudu mahitaji yao ya kifedha.

Meneja Uhusiano wa Kitengo cha Wateja Wakubwa wa benki hiyo, Amour Muro, alisema Jukwaa la wateja wakubwa limekutana kubadishana mawazo katika wiki hiyo ya huduma kwa wateja ili kupata uzoefu wa mambo mbalimbali ya kibiashara.

"Hili ni moja ya majukumu yetu katika wiki hii, inatusaidia kuzungumza nao kujua namna ya kuongeza thamani ya huduma tunazowapatia na litatusaidia kupanua uelewa na kuongeza thamani kupitia majadiliano tutakayofanya," alisema Muro.

Alisema benki hiyo inaamini katika utoaji bora wa huduma na kwamba watahakikisha wanaendelea kufanya marekebisho ya mara kwa mara kwa kusikiliza changamoto za wateja wao.

Magdalena Magali, mwakilishi wa Kampuni ya Saruji ya Tanzania Potland, aliishukuru NMB kwa kuwaandalia jukwaa hilo na kuwapa nafasi ya kubadilishana mawazo.

Aliipongeza kwa mabadiliko chanya ya kimfumo kutoka analogia kwenda dijitali, na kwamba umesaidia kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa haraka, wepesi na usalama na kuwataka Watanzania kuchangamkia huduma hizo ili kuokoa muda na kwenda na wakati.

Naye Steven Gideon, ambaye ni Ofisa Mipango na Bajeti wa Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), aliwataka Watanzania kuchangamkia fursa mbalimbali zinazotolewa na benki hiyo.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA** NYUMBA INAUZWA SINZA LION KUELEKEA KWA MWAIBULA NYUMA YA DEFRANCE HOTEL, BLOCK E PLOT No. 665, 288 SQM. MAWASILIANO: 0713 525954 / 0787 822000.


**VIWANJA/NYUMBA.** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Nyumba inauzwa Kaloleni Arusha ina frame za biashara,nyenye SQ 59 mil 800. Nyumba inauzwa Usariver ya bedroom4 mil 70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.

**SHAMBA LINAUZWA**, Hekari 25@ Tshs 800,000/= ziko Miono Kijiji cha Mkange Wilaya ya Chalinze (kuelekea Sadani Game Reserve) mwendo dakika 40 toka barabara kuu iendayo Tanga. Wasiliana na 0713 604049 / 0784 604049.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA


## KUPOTEA KWA CHETI



115456402

**HOSEA NDITIYE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0731-0376** kilichotolewa na MAKONGO SEKONDARI November, 1997. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MTB/RB/398/99.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



115456702

**HADIJA BAKARI JUMA** anatangaza kupotelewa na Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba **S.1611/0504** kilichotolewa na KALENGE HIGH SCHOOL mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No. **9910810225287.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MOHAMMED ENTERPRISES (T) LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya PIKIPIKI aina ya **BAJAJI BOXER** yenye namba za usajili **MC240CDP**. Chassis na **MD2B15BYOJWJ90185** Engine namba. **JVZWJJ34554** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/365074/2019.**

115456902

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**Simba Drilling Co. Limited** Inatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA LAND CRUISER STATION WAGON** yenye namba za usajili T 110 AFP Chassis No. **JT711PJA507000862** Engine No. **IHZ0259423** Yenye rangi NYEUPE. Yeyote atakayeiona atoe taarifa Polisi. Taarifa ya Polisi: **MWA/NY/RB/342745/2019**

215455802

## KUPOTEA KWA PASSPORT/ HATI TA KUSAFIRIA



115456002

**Thabit Badi Lema** anatangaza kupotelewa na Passport/hati ya kusafiria yenye namba **AB251073** iliyotolewa na Ofisi za Uhamiaji ar es Salaam mwaka 2007.Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/SEL/RB/370913/2019**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**VICTOR BAHATI OSEPHAT** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE PAMOJA NA ACADEMIC CERTIFICATE CHENYE NAMBA YA **MTIHANI S.2178/0163** KILICHOTOLEWA MWAKA 2014 KATIKA SHULE YA SEKONDARI GOLDEN RIDGE SECONDARY SCHOOL.

KWA YOYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI
**MAS/RB/3078/2019.**

115457102


***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0767 223311***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie


0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# SOLSKJAER AHOFIA KUTIMULIWA MAN UNITED




**MANCHESTER,** England

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer amesema ameingia hofu ya kupoteza kazi Manchester United endapo watafungwa na Liverpool.

United na Liverpool zitavaana Oktoba 20 mwaka huu katika mchezo wa Ligi Kuu England, utakaochezwa kwenye Uwanja wa Anfield.

Solskjaer ametoa kauli hiyo akiwa na maumivu ya kufungwa bao 1-0 dhidi ya Newcastle United katika mchezo uliopita.

Makamu Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu wa United, Ed Woodward, hajatoa tamko kuhusu hatima ya kocha huyo licha ya kufanya vibaya msimu huu.

Kocha huyo alisema njia pekee ya kunusuru kibarua chake ni kupata ushindi dhidi ya watani wao wa jadi.

United ilifungwa mabao 3-1 kwenye uwanja huo Desemba mwaka jana na matokeo hayo yalichangia kumng'oa Jose Mourinho.

## 'United watashuka daraja'

**LONDON,** England

KOCHA wa zamani wa Timu ya Taifa ya England, Sam Allardyce, amesema kwamba Manchester United, watashuka daraja kama hawatafanya haraka kusajili mshambuliaji wa kuja kuwafungia mabao.

United wapo pointi mbili tu juu ya kuangukia kwenye shimo la kushuka daraja baada ya kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa kwa Newcastle United.

Wababe hao wa Old Trafford wamefunga mabao tisa tu msimu huu, manne waliyapata kwenye mechi yao ya kwanza dhidi ya Chelsea, lakini sasa straika aliyeaminiwa, Marcus Rashford, amekuwa ovyo, hajui hata goli lilipo.

Big Sam, ambaye amepata umaarufu wa kuwa mtu anayefuatwa kuokoa jahazi timu inapokuwa kwenye hali ya kushuka daraja, anasema kwamba kocha Ole Gunnar Solskjaer anatakiwa kutafuta suluhisho la haraka, la sivyo mambo yatamchachia.

"Hili jambo halipo nje ya uwanja wake na kwamba wapo kwenye hali hiyo kutokana na kusumbuliwa na majeruhi wengi. Wachezaji wanaonekana kushindwa kuwa fiti kwa wakati na hilo ndio tatizo," alisema Big Sam na kuongeza.

"Kuna usumbufu pia wa huyu (Paul) Pogba kutaka kuondoka. Nadhani hakuchagua njia nzuri ya kuliwasilisha hilo na si kusema, nataka kuondoka. Shida yao kubwa Manchester United haipati mabao, wakimaliza hilo, wamemaliza kazi."





## Mourinho atajwa kutua Spurs

**LONDON,** England

JOSE Mourinho ameripotiwa kuwa yupo kwenye rada za kutakiwa na klabu ya Tottenham Hotspurs, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Imeelezwa kwamba, kocha huyo ameweka kwenye orodha ya kutakiwa na klabu hiyo ili kuchukua nafasi ya Mauricio Pochettino ambaye kwa sasa nafasi yake inaonekana kufikia mwisho.

Kinachoelezwa kwa sasa ni kuwa, kocha huyo Mreno, aliyejipachika jina la The Special One, ameanza kuifukuzia nafasi ya kwenda kuwa kocha kwenye kikosi cha Tottenham Hotspur baada ya kuona Pochettino anataabika na timu yake.

Kwa sasa, Mourinho hana kazi tangu alipoondolewa huko Manchester United, Desemba mwaka jana.

Mara kadhaa, kocha huyo amekuwa akisema kwamba anasubiri kibarua mwafaka na sasa anaona Spurs inaweza kuwa kazi sahihi kwake baada ya kuona mpango wake wa kwenda Real Madrid kuchukua mikoba ya Zinedine Zidane hauonekani kukamilika.

Mourinho amekuwa akizitazama Spurs na Real Madrid zinavyokwenda huku mpango wake wa kwenda Bernabeu ukitegemea zaidi ukaribu wake na rais wa klabu hiyo, Florentino Perez.

Pochettino yupo kwenye presha kubwa ya kuhusu kibarua chake huko Spurs baada ya timu hiyo kushinda mechi tatu tu kati ya 11 ilizocheza msimu huu.

# Kauli chafu yamponza Dembele

**BARCELONA,** Hispania

SHIRIKISHO la Soka la Hispania limetangaza adhabu ya kumfungia michezo miwili mshambuliaji wa Barcelona, Ousmane Dembele, baada ya kuonyeshwa kadi nyekundu wakati wa mchezo wa La Liga dhidi ya Sevilla mwishoni mwa juma lililopita.

Dembele alionyeshwa kadi nyekundu ya moja kwa moja na mwamuzi Antonio Mateu Lahoz, baada ya kutokea majibishano baina ya wawili hao.

Dembele alikumbwa na adhabu hiyo dakika chache baada ya kuifungia Barcelona bao la pili, ambalo ni miongoni mwa mabao manne yaliyoipa ushindi klabu hiyo ya Camp Nou dhidi ya Sevilla.

Taarifa ya shirikisho hilo imeeleza kuwa, mshambuliaji huyo kutoka nchini Ufaransa, alimtolea lugha chafu mwamuzi Lahoz, baada ya kujiridhisha kupitia ripoti iliyowashilishwa mara baada ya mchezo huo.

Kwa uamuzi huo, Dembele atakosa mchezo dhidi ya Real Madrid 'El Clasico', ambao utatanguliwa na ule dhidi ya Eiber, utakaochezwa mwishoni mwa juma lijalo.

Barcelona watakuwa wenyeji wa Real Madrid katika mchezo wa La Liga, uliopangwa kuchezwa Oktoba 26 mwaka huu.



# MBAPPE AIPA PIGO UFARANSA



**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI Kylian Mbappe ameondolewa kwenye kikosi cha timu ya taifa ya Ufaransa, kinachoendelea na maandalizi ya michezo ya kufuzu fainali za mataifa ya Ulaya (Euro 2020), dhidi ya Iceland na Uturuki.

Taarifa zilizotolewa na Shirikisho la Soka Ufaransa (FFF) zimeeleza kuwa, mshambuliaji huyo aliondoka juzi kambini na kurejea kwenye klabu yake ya PSG kwa ajili ya kuanza matibabu.

Mbappe, alipatwa na majeraha ya paja akiwa katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya juma lililopita dhidi ya Borussia Moenchengladbach ya Ujerumani, na iliaminiwa hakuumia sana na ndio maana aliitwa kwenye Timu ya Taifa ya Ufaransa.

Hata hivyo, hali ya mshambuliaji huyo haikuridhisha, alipofika kambini mwanzoni mwa juma hili na ameshauriwa kurejea jijini Paris, kufanyiwa matibabu ya jeraha lake.

Ufaransa wataanza kukipiga dhidi ya Iceland ugenini leo Ijumaa katika mchezo wa Kundi H na kisha watarejea nyumbani kuwakabili Uturuki katika mpambano unaotarajiwa kuwa na vuta nikuvute siku ya Jumatatu.

Mabingwa hao wa dunia wanashika nafasi ya pili katika msimamo wa Kundi H wakiwa na alama 15, nyuma ya Uturuki ambao katika mchezo wa kwanza uliochezwa mjini Konya Juni mwaka huu, waliwabanjua Ufaransa.

Iceland wanakamata nafasi ya tatu katika kundi hilo, kwa kufikisha alama 12 zilizotokana na michezo sita waliyocheza mpaka sasa.

# *Pique ajipa kadi asiwakose Madrid*

**BARCELONA,** Hispania

BEKI Gerard Pique anashutumiwa kujisababishia kadi ya njano makusudi ili asikumbane na adhabu ya kukosa mechi ya El Clasico.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 32 alionyeshwa kadi ya njano ya tano msimu huu baada ya kupiga mpira makusudi mbali kwenye mchezo wa ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Sevilla kwenye La Liga, Jumapili.

Kutokana na hilo, sasa atakosa mechi dhidi ya Eibar baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa, lakini atakuwa na ruhusa ya kuikabili Real Madrid huko Nou Camp, Oktoba 26 mwaka huu.

Gazeti la Marca linafichua kwamba Pique kwa makusudi alimfanya mwamuzi Miguel Antonio Mateu Lahoz amwonyeshe kadi ya njano ili tu asiwe kwenye hatari ya kuikosa Madrid kama atakwenda kuonyeshwa kadi kwenye mechi dhidi ya Eibar.

Februari mwaka huu, nahodha wa Los Blancos, Sergio Ramos alipewa adhabu ya mechi mbili na Uefa baada ya kuonekana kwamba alijifanyisha makusudi ili apewe kadi ya njano kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya 16 dhidi ya Ajax, akiamini kwamba timu yake itakwenda kushinda mechi ya marudiano na kuwatupa nje Wadachi hao.

Ramos alimchezea rafu ya makusudi Kasper Dolberg.

Baadaye mwenyewe alisema: "Ningekuwa muongo kama sitasema kwamba nililazimisha kuonyeshwa kadi ile ya njano."

Kinachoelezwa ni kwamba Pique ametumia ujanja huo kujiondoa kwenye hatari ya kukosa mchezo wa El Clasico kwenye La Liga.



DON A SOKA
MAG




# HATIMAYE MESUT OZIL KUONDOKA ARSENAL

●●● Ni baada ya Waturuki Fenerbache kuonyesha nia ya kumsajili Mjerumani huyo huku...

**LONDON,** England

MCHEZAJI ambaye analipwa kiasi kikubwa zaidi katika kikosi cha Arsenal, Mesut Ozil, anajiandaa kuondoka katika klabu hiyo kwenye dirisha dogo la usajili la Januari, huku Fenerbache ikitajwa inamhitaji kiungo huyo.

**Ozil, ambaye alitua Emirates akitokea kwa vigogo wa La Liga Hispania, Real Madrid mwaka 2013, amekuwa si chaguo na hayuko kwenye mipango ya kocha wa timu hiyo, Unai Emery msimu huu.**

Kocha huyo wa Arsenal amekuwa akiwatumia zaidi wachezaji chipukizi wakiwamo, Reiss Nelson, Dani Ceballos na Joe Willock na sasa klabu hiyo maarufu kwa jina la The Gunners inajiandaa kuokoa kiasi cha fedha ilichokuwa inatumia kumlipa Mjerumani huyo kwa kumtoa kwa mkopo ifikapo Januari.

Kwa mujibu wa gazeti moja la Uturuki liitwalo Takvim, klabu ya Fenerbache imeweka wazi kwamba inataka kumsajili mshindi huyo wa Kombe la Dunia mara moja kwa mkopo ifikapo Januari ili kuongeza nguvu katika kikosi chake.

Imeelezwa kuwa, tayari Arsenal imesema kwamba iko tayari kulipa sehemu ya mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki anazolipwa Ozil, ili kuhakikisha kuwa mchakato huo wa uhamisho unafanikiwa.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 30, ambaye alionekana ana nafasi ya kutangazwa kuwa nahodha mpya wa timu hiyo baada ya Laurent Koscielny kuondoka, amebainika kwamba hana nafasi ya kuwamo kwenye kikosi cha Emery, ambaye alirejea kikosini akiwa na kiwango duni huku mechi za msimu huu zikiendelea.

Mjerumani huyo ambaye alipewa mapumziko mapema mwanzoni mwa msimu baada ya kuwapo kwa tukio la kutekwa akiwa pamoja na mchezaji mwingine wa timu hiyo, Sead Kolasinac.

Lakini tangu hapo, Ozil ameshindwa kuwapo katika kikosi chochote cha timu hiyo na kumfanya Emery kumteua kiungo, Granit Xhaka kuwa nahodha, na viwango vya wachezaji chipukizi akiwamo Matteo Guendouzi vimemfanya Ozil kuwa kwenye wakati mgumu wa kupata nafasi ya kurejea uwanjani.

Kuendelea kumlipa kiasi kikubwa cha fedha kiungo huyo, ndio jambo ambalo klabu hiyo inafikiria kuachana nalo na mchakato wa kutakiwa na klabu hiyo ya Uturuki, unaonekana utamfanya Mjerumani huyo kuondokana na hali ya kutosa benchi.

Ozil amecheza mechi mbili tu tangu kuanza kwa msimu huu, na kati ya hizo, aliacha katika mechi dhidi ya Watford, lakini hakumaliza mchezo huo baada ya Emery kuamua kumfanyia mabadiliko.

Baada ya kumalizika kwa kalenda ya kimataifa ya Fifa, Arsenal itashuka dimba kuikabili Sheffield United, mchezo utakaofanyika Oktoba 21 mwaka huu.

## ZISIKUPITE

### UNITED, MANDZUKIC SAFI

MANCHESTER United imefikia katika hatua nzuri ya mazungumzo ya kumsajili straika wa Timu ya Taifa ya Croatia, Mario Mandzukic, 33, kutoka Juventus hapo mwakani. ***(Tuttosport, via Mirror)***

### SOLSKJAER YUKO SALAMA

HATIMA ya Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, iko salama licha ya klabu hiyo kuwa katika wakati mgumu wa kusaka matokeo mazuri na vile vile ikitabiriwa kupokea kichapo kikubwa kutoka kwa mahasimu wao Liverpool katika mchezo unaokuja. ***(Times - subscription required)***

### LYON YAMKOSA MOURINHO

LYON wamekwama kuendelea na mchakato wa kumshawishi Kocha wa zamani wa Chelsea na Manchester United, Jose Mourinho, kuwa kocha wake mpya baada ya Mreno huyo mwenye umri wa miaka 56 kuonyesha nia ya kurejea kwenye Ligi Kuu England. ***(Mirror)***

### MUSTAFI KUONDOKA ARSENAL

BEKI wa Arsenal, Shkodran Mustafi, amesema kuwa vitendo vya unyanyasaji na kutengwa vimemfanya kuanza mazungumzo ya kutaka kuondoka klabuni hapo na kueleza kwamba anaweza kuelekea katika Ligi ya Bundesliga. ***(Der Speigel , via Guardian)***

### UNITED YAMWINDA DIAS

MANCHESTER United imeweka wazi nia yake ya kumsajili beki wa kati wa Benfica, Ruben Dias, lakini nyota huyo anajiandaa kupewa mkataba mpya ambao utamfanya thamani yake ya kuuza kufikia pauni milioni 79. ***(Express)***

### MADRID, SPURS KUTETA

MABOSI wa Real Madrid wanatarajia kuanza mazungumzo na Tottenham kwa ajili ya kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen (27), katika kipindi cha dirisha dogo la usajili ifikapo Januari. ***(Marca)***

### GUARDIOLA: FODEN HAUZWI

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema kuwa kiungo wa Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 21 ya England (U-21), Phil Foden (19), ni mmoja kati ya wachezaji ambao hawatauzwa na klabu hiyo hata kama watapokea dau la pauni milioni 450. ***(Sun)***

### BAYERN YAMKERA MULLER

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Thomas Muller (30), amesema hana furaha baada ya kupunguziwa majukumu katika kikosi cha Bayern Munich na kuweka wazi kwamba anaweza kujiandaa kuondoka katika klabu hiyo ifikapo Januari. ***(Kicker, via Mail)***

### CAVANI, SILVA NJIA MOJA

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Edinson Cavani (32) na beki wa Brazil, Thiago Silva (35), wameweka wazi kwamba wataondoka Paris St-Germain wakiwa wachezaji huru mwishoni mwa msimu huu. ***(ESPN)***

### RAKITIC AJIANDAA KUONDOKA

KIUNGO wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Croatia, Ivan Rakitic (31), ambaye alikuwa anahusishwa na mipango ya kujiunga na Manchester United katika kipindi cha majira ya joto mwaka jana, hameweka wazi kwamba anataka kujiunga na klabu nyingine ili kupata nafasi katika kikosi cha kwanza. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

# Mafunzo wajinoa kurejesha makali

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Mafunzo, Abdallah Bakari, amesema kuwa ataendelea kukiimarisha kikosi chake ili kuhakikisha kinafanya vizuri katika mechi zinazoendelea za Ligi Kuu Zanzibar, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Bakari, alisema kuwa licha ya kutopata matokeo mazuri katika michezo iliyopita kama alivyotarajia, lakini tayari ameshagundua changamoto iliyokuwa inakikabili kikosi chake.

Kocha huyo alisema kuwa ameshaanza kurekebisha mapungufu hayo aliyoyabaini, hasa katika safu ya ushambuliaji na ulinzi.

"Timu yangu inacheza mpira mzuri sana, lakini kutokana na aina ya mtindo tunaotumia, washambuliaji wanashindwa kupachika mabao, hii inatokana na kutokuwa na umakini wanapokaribia katika lango la wapinzani, nataka wachezaji wabadilike na wacheze mpira kwa nia ya kushinda, ligi ya Zanzibar ni ngumu tofauti na watu wanavyoiyona," alisema Bakari.

Mafunzo ambayo imecheza mechi tano, ina pointi tano, zilizotokana na kushinda mchezo mmoja, sare mbili na imefungwa mechi moja, katika msimamo wa ligi hiyo iko katika nafasi ya nane.

# UCHAGUZI BODI YA LIGI KUFANYIKA DESEMBA 7

**Na Shufaa Lyimo**

UCHAGUZI Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), umepangwa kufanyika ifikapo Desemba 7, mwaka huu, hapa jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Ally Mchungahela, alisema kuwa nafasi ambazo zitagombewa katika uchaguzi huo ni sita na alizitaja kuwa ni za Wajumbe Wawakilishi Klabu za Ligi Kuu (tatu), Wawakilishi Ligi Daraja la Kwanza (mbili) na nafasi moja ya Mjumbe Mwakilishi Ligi Daraja la Pili.

Mchungahela alisema kuwa mchakato wa kuanza kutoa fomu kwa ajili ya viongozi wanaotaka kuwania nafasi hizo utaanza kesho na unatarajiwa kumalizika Jumanne Oktoba 16, mwaka huu.

**"Kati ya Oktoba 17 hadi 19 mwaka huu, kutakuwa na kikao cha kufanya mchujo wa awali moja kwa moja na kuwapa barua wagombea," alisema Mchungahela.**

Alisema pia kati ya Oktoba 20 na 21 mwaka huu, kamati hiyo itatangaza orodha ya majina yote ya wagombea waliopitishwa kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi huo na Oktoba 22 hadi 24 mwaka huu, itakuwa ni kipindi cha kupokea na kuweka pingamizi kutoka kwa wagombea husika.

Alieleza pia usaili wa wagombea watakaokuwa wamepitishwa utafanyika kati ya Oktoba 27 na 29 mwaka huu, huku kuanzia Oktoba 30 hadi Novemba Mosi itakuwa ni kipindi cha Kamati ya Maadili kuwasilisha masuala ya kimaadili endapo yatakuwapo.

Kiongozi huyo alitaja muda wa kufanya kampeni utakuwa ni kati ya Desemba 2 hadi 6 mwaka huu na wagombea watatakiwa kunadi sera zao kistaarabu.

Kwa sasa Bodi ya Ligi inaongozwa na Mwenyekiti wa Coastal Union, Stephen Mguto, ambaye ni Makamu wa Pili wa TFF, aliyechaguliwa katika uchaguzi mdogo kujaza nafasi iliyoachwa na Clement Sanga wa Yanga, ambaye alipoteza sifa za kuendelea kushikilia nafasi hiyo.



Mchezaji wa timu ya Mchenga, Baraka Sadik (kulia), akiwania mpira dhidi ya Stephano Mshana wa Tamaduni katika mechi ya mashindano ya Sprite Bball yanayoendelea kwenye Uwanja wa Ndani wa Taifa jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara Ndogo na Kati wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (kushoto), akikabidhi vifaa vya michezo kwa Mkurugenzi wa Michezo na Utamaduni wa JWTZ, Kanali Erasmus Bwegoge, kwa ajili ya timu zinazokwenda kushiriki mashindano ya majeshi ya dunia huko China. **NA MIPIGAPICHA WETU**

# *NMB yatoa vifaa timu ya Majeshi*

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuongeza hamasa kwa timu ya Majeshi inayotarajiwa kwenda kushiriki mashindano ya dunia, Benki ya NMB imekabidhi vifaa mbalimbali vya michezo vyenye thamani ya Sh. milioni 18.

Tanzania inatarajiwa kuwakilishwa na timu ya ngumi, riadha na mieleka, katika mashindano hayo yatakayofanyika kuanzia Oktoba 18 hadi 27 mwaka huu nchini China.

Msafara wa watu 32 utakaojumuisha wachezaji, viongozi na makocha utaondoka nchini Jumatatu kuelekea katika mashindano hayo.

Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara Ndogo na za Kati wa NMB, Filbert Mponzi, alisema wameamua kuisaidia timu hiyo kutokana na ushirikiano uliopo baina ya pande hizo mbili.

Mponzi alisema anatarajia msaada huo walioutoa, utaongeza hamasa ya kufanya vizuri kwa wawakilishi hao wa Taifa katika mashindano hayo ya dunia.

Naye Mkurugenzi wa Michezo na Utamaduni wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Kanali Erasmus Bwegoge, aliishukuru NMB kwa msaada huo na kusisitiza kuwa ushirikiano baina yao utaongeza chachu ya mafanikio.

"Tumejiandaa vizuri, timu yetu ya riadha iko kambini Arusha ambapo itachuana katika mbio za mita 1,500, mita 5000, mita 10,000 na marathoni wakati wale wa mieleka wanaendelea na mazoezi huku timu ya ngumi itakuwa chini ya kocha Hassan Mzonge," alisema Bwegoge.

# Michezo

Ijumaa Oktoba 11, 2019

Nipashe



Hatimaye Ozil kuondoka Arsenal

UKURASA 30




Wachezaji wa Simba wakiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Bandari FC kutoka Kenya itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam. **PICHA NA JUMANNE JUMA**

## Simba kwenda Kigoma Jumapili

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kikosi cha Simba kitaondoka jijini Dar es Salaam Jumapili ili kuelekea Kigoma kwa ajili ya kucheza mechi mbili za kirafiki, mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara wamejipanga kuonyesha soka la kiwango cha juu watakapoikaribisha Bandari kutoka Kenya.

Simba inatarajia kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Bandari kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kukutana na Azam FC hapo Oktoba 23 mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kuwa wanatarajia kwenda Kigoma na wachezaji wote waliobakia kikosini na lengo ni kuwapa nafasi mashabiki wao wa mkoa huo na jirani kuiona timu yao.

Rweyemamu alisema kuwa mbali na faida za kiufundi, ziara za mikoani zimekuwa zikiwajenga wachezaji wao na kufahamu thamani halisi ya klabu wanayoitumikia.

"Tunatarajia kuonyesha kiwango kizuri katika mchezo dhidi ya Bandari na mingine miwili tutakayocheza huko Kigoma, ni mechi ambazo hatuna presha, hivyo tunaamini wachezaji wataonyesha utulivu na ukomavu," alisema Rweyemamu.

Ikiwa Kigoma, Simba inatarajia kucheza mchezo wa kwanza dhidi ya Mashujaa utakaofanyika Jumatatu Oktoba 14 mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma na baada ya siku mbili itakutana na Warundi Aigle Noir kwenye uwanja huo huo.

Wakati huo huo, kiungo wa kimataifa wa mabingwa hao watetezi kutoka Kenya, Francis Kahata, amesharejea nchini akitokea kwao ambapo alikwenda kwa ruhusa maalumu kutoka kwa uongozi wa klabu hiyo.

# Maxime awapa mchongo Yanga

**Na Somoe Ng'itu**

## ●●● Ni namna watakavyowasulubu Pyramids na kusonga mbele katika Ligi ya Mabingwa Afrika...

BAADA ya Yanga kupangwa kukutana na Pyramids ya Misri katika mechi ya hatua ya mtoano ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, amewataka wawakilishi hao wa Tanzania kujiamini na kutowaogopa Waarabu hao.

**Yanga itaanza kwa kuwakaribisha Pyramids Oktoba 27 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, kabla ya kusafiri kuwafuata Waarabu hao Novemba 2 mwaka huu, na mshindi wa jumla atatinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).**

Akizungumza na gazeti hili jana, Maxime, alisema kuwa wanachotakiwa kukifanya Yanga ni kujiandaa vema kuwakabili wapinzani wao na kuondoa mawazo kwamba timu za Waarabu ni bora zaidi yao.

Maxime alisema kuwa Yanga inatakiwa kurekebisha makosa ya kiufundi yaliyobainika katika mechi zake zilizopita za Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara, na hapo watakuwa wamejiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele.

"Kikubwa wanatakiwa wakapambane, wasikate tamaa mapema, hakuna sababu ya kuanza kuwaogopa Pyramids mapema, wasiweke mawazo ya kufungwa mbele, wanatakiwa kujipanga na hakuna soka lolote linaweza kutokea," alisema nahodha huyo wa zamani wa Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Beki huyo wa zamani wa Mtibwa Sugar, aliwataka wawakilishi hao pekee wa Tanzania waliobakia kwenye mashindano ya kimataifa kujiimarisha zaidi katika kila idara endapo itafanikiwa kusonga mbele kwenye michuano hiyo. Kocha Msaidizi wa Yanga Mzambia Noel Mwandila, alisema kuwa hawana wasiwasi wowote kuelekea mechi hizo mbili watakazocheza dhidi ya Pyramids na wanaamini kikosi chao kina nafasi ya kuwaondoka Waarabu hao.

"Timu zote zilizofika hatua hii ni nzuri, tutajiandaa vizuri kuhakikisha tunapata matokeo bora, hatuwezi kurekebisha historia ya nyuma, lakini tunaweza kujiandaa kuweka historia mpya ya baadaye," alisema Mwandila.

Mfaransa Sebastien Desabre, Kocha Mkuu wa zamani wa Timu ya Taifa ya Uganda (The Cranes), ndiye anayeiongoza Pyramids (zamani Al Assiouty Sport), ambayo ilianzishwa mwaka 2008.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Misri, Pyramids iko katika nafasi ya pili ikiwa na pointi saba baada ya kucheza mechi tatu, wakati Yanga ambayo iko katika nafasi ya 14 na imeshuka dimbani mara tatu, ina pointi nne.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002